# Nipashe

Alhamisi Oktoba 20, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581104

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAM

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 70

LIKE & FOL



SUPA JACKPOT

TZS.1,042,026,796

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#





## Wauguzi wafutiwa leseni kusababisha kifo cha mjamzito

UKURASA 3



## NEYMAR AMPONGEZA BENZEMA

UKURASA 30



# Mchujo wagombea CCM waanza rasmi

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### TANZANIA YAMWAGIWA BILIONI 5/- UENDELEZAJI WA SEKTA YA KILIMO

DENMARK na Sweden zimetoa zaidi ya Sh. bilioni tano katika kuendeleza kilimo hasa katika uzalishaji wa alizeti...

UKURASA WA 4

### MKUTANO KUMUENZI MAALIM SEIF JUMAMOSI

MKUTANO wa pili wa kumuenzi aliyekuwa Makamu wa kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, unatarajiwa...

UKURASA WA 7

### WAZAZI WADAIWA KUTISHA WATOTO WASIFAULU MITIHANI

BAADHI ya wazazi wilayani Makete, mkoani Njombe, wamedaiwa kuwatisha watoto wao wanaohitimu elimu ya...

## Hofu kwa wafanyakazi mia sita kupoteza ajira uwanja ndege Z'bar

UKURASA 3




Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo, akitoa maoni yake kuhusu muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, katika Ukumbi wa Msekwa Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**



# Wadau wataka wake wenza wawepo Bima Afya kwa Wote

UKURASA 2


**MICHEZO** SIMBA, YANGA HAKUNA KULALA UK.32 **KABWELA** UK.7




Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura (kushoto), akiwa na Mkuu wa Upelelezi wa nchi ya Thailand, Meja Jenerali Khemmarin Hassir, baada ya kufanya mazungumzo kuhusu ushirikiano kati ya jeshi hilo na Thailand, wakiwa New Delhi, nchini India jana, wanakohudhuria Mkutano Mkuu wa 90 wa INTERPOL. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Mchujo wagombea CCM waanza rasmi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

VIKAO vya mchujo wa wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), walioomba kuwania nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chama na jumuiya zake, vimeanza.

Jumuiya za chama hicho ni Umoja wa Vijana (UVCCM), Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) na Jumuiya ya Wazazi.

Ratiba ya vikao vya uchaguzi mkuu ndani ya chama ilitolewa Oktoba 10, mwaka huu na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Oganaizesheni, Dk. Maudline Castico, kwa makatibu wakuu wa jumuiya na makatibu wa CCM mikoa.

Oktoba 10 hadi 12, kwa mujibu wa ratiba hiyo, kamati za utekelezaji za jumuiya za CCM ngazi ya taifa ziliketi kutoa mapendekezo kwa Mabaraza Makuu ya Jumuiya za CCM ngazi hiyo.

Ratiba hiyo inaonyesha Oktoba 13 hadi 15, mwaka huu, Mabaraza Makuu ya Jumuiya yalitoa mapendekezo kwa Kamati Kuu na Kamati Maalum ya NEC Zanzibar kuhusu wanachama walioomba kuwania nafasi mbalimbali.

Nafasi hizo ni wenyeviti wa jumuiya za CCM ngazi ya taifa, makamu wenyeviti, wajumbe wa NEC wanaotokana na jumuiya za CCM.

Pia wenyeviti wa jumuiya za CCM ngazi ya mkoa, wajumbe wa Baraza Kuu la kila jumuiya ngazi ya taifa, wanachama wanaoomba nafasi za uongozi za jumuiya zisizokuwa za uwakilishi katika vikao vya CCM.

Kadhalika, Oktoba 17 hadi 18, mwaka huu, ratiba hiyo inaonyesha Kamati Maalum ya NEC Zanzibar ilitoa mapendekezo ya walioomba kugombea uenyekiti wa CCM wa mikoa, wajumbe wa NEC kupitia mikoa, makatibu wa siasa na uenezi wa mikoa, wenyeviti wa jumuiya za CCM taifa na makamu wenyeviti wa jumuiya.

Pia wajumbe wa NEC wanaotokana na jumuiya, wenyeviti wa jumuiya za CCM ngazi ya mkoa, wajumbe wa Baraza Kuu la kila jumuiya ngazi ya taifa na wanachama wanaoomba nafasi za uongozi za jumuiya za CCM, zisizokuwa za uwakilishi katika vikao vya CCM.

Ratiba inaonyesha kuanzia Oktoba 24 hadi Novemba 2, mwaka huu, vitafanyika vikao vya ngazi ya taifa kwa ajili ya kuchambua, kupendekeza na kuteua majina ya wagombea watakaowania nafasi hizo.

# Wadau wataka wake wenza wawepo Bima Afya kwa Wote

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU wametoa maoni kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote pamoja na mambo mengine wakitaka kupanuliwa kwa wigo wa wategemezi hususan watoto na wenza.

Maoni hayo walitoa jana kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ambapo pia walipendekeza kuwapo mfuko maalum wa kikodi ambao fedha zake zitatumika kusaidia wasio na uwezo wa kuchangia.

Mwenyekiti wa Mfuko Binafsi wa Bima ya Afya, Aaron Nelson, alisema ni muhimu kuangalia kipengele cha wategemezi kwenye muswada kuhusu idadi ya watoto na wenza ili kuondoa hali ya sasa inayolazimisha kuwa na watoto wanne na mwenzi mmoja.

Alipendekeza kitita cha msingi kishikiliwe na serikali na pale mtoa huduma anapotaka kuongeza huduma, asiwekewe ukomo.

"Sambamba na hilo, kunatakiwa kuwe na bodi huru itakayosimamia watoa huduma, serikali na watumiaji katika uendeshaji wa huduma za bima ya afya kwa wote," alisema.

Mwakilishi wa Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU), Dk. Leons Mjwahuzi, alisema wanapendekeza kusiwapo na ukomo wa umri wa uanachama kwa wategemezi na wigo wa wanufaika uongezwe.

"Kadi za bima zipatikane kielektroniki, mchangiaji awe na uhuru wa kuchagua wategemezi na asibanwe kuweka watoto wake pekee. Pia bima ihusishe vipimo vyote, isibague vipimo vingine yaani ihusishe na magonjwa yasiyo ya kuambukiza na miwani ipatikane kupitia bima ya afya,"alisema.

### VIWANGO VIPUNGUZWE

Dk. Chakupewa Joseph kutoka THTU, alisema mfuko unatakiwa uwe na uwazi na viwango vilivyopendekezwa vipunguzwe kwa kuwa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ilikuwa Sh.30,000 lakini wananchi walishindwa kumudu na kwamba viwango vya Sh.340,000 kwa kaya na Sh.84,000 kwa mtu mmoja ni fedha nyingi.

Alisema kutokana na viwango vilivyowekwa kwenye muswada huo kuna hatari ya wananchi wasiokuwa na uwezo kukimbilia kwenye papo kwa papo (matumizi ya fedha taslimu).

Naye mwakilishi wa Chama cha Watoa Huduma Binafsi Tanzania, Isaac Mayala, alisema watumishi wa umma waruhusiwe kuchagua aina ya mfuko wa bima ya afya wanaotaka kujiunga ili kuondoa ujimilikishaji.

Alishauri katika muswada huo kuwepo na chombo huru ambacho kitashughulika na malalamiko kutoka kwa pande zote zinazohusika na bima ya afya kwa wote.

"Kwenye muswada inaonyesha kwamba TIRA (mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania) ndiyo itakayodhibiti huduma ya bima. Tunaona ili kuwa na uhuru kwenye suala hili ni muhimu kuwa na chombo huru ambacho kinasimamia usawa," alisema.

Katibu wa Sera na Utafiti wa ACT- Wazalendo, Idrisa Kweweta, alisema kutokana na watu wengi kutokuwa na uwezo wa kulipia vitita vilivyopendekezwa, ni vyema kuanzishwa mfumo mbadala, hivyo wanashauri uwasilishwe muswada wa hifadhi ya jamii kwa wote ambapo asilimia 20 ya michango itakwenda kwenye kuhudumia afya.

Mwakilishi wa Idara ya Dharura Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dk. Patrick Shayo, alipendekeza gharama za vipimo zisitofautiane kwenye ngazi za vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuwa huduma zinazotolewa ni sawa.

"Ni muhimu muswada utafsiri maskini ni nani? Na gharama zimeelekezwa kwa nani? Kwenye vitita kikiwemo kile cha msingi, iwekwe pia huduma ya dharura (ambulance) hata kama mtu atakuwa nje ya hospitali apate huduma," alisema.

### CHOMBO HURU

Meneja Programu za Uboreshaji wa Huduma za Afya kutoka Taasisi ya Benjamini Mkapa, Hendry Samky, alishauri kwenye muswada kianzishwe chombo huru ambacho kitatoa mapendekezo yake kwa Wizara ya Afya ya kuelekeza namna ya utoaji huduma sahihi na gharama.

Pia alipendekeza vitita vya mafao ya msingi vipitiwe upya huku akishauri Waziri kufanya mapitio ya kanuni zitakazotungwa kwa ajili ya vitita kila baada ya miaka mitatu.

Alisema taasisi hiyo inashauri mfuko maalum wa kutoa fedha kusaidia wasiojiweza ambao miongoni mwa vyanzo vya mapato ni asilimia 50 ya fedha za mapato ya bidhaa zinazosababisha madhara mwilini kama vile tumbaku na vilevi.

Kuhusu bima kufungamanishwa na huduma za msingi, alipendekeza kutozuia haki za msingi kwa wananchi na zuio lililowekwa kwenye muswada liondolewe.

"Mfumo wa uchangiaji uwe pia wa kikodi kama inavyofanyika nchini Ghana hii itasaidia kupunguza kelele za gharama zilizopendekezwa, kwa kuwa serikali ya Ghana yenyewe hutoa asilimia 2.5 kuchangia kwenye mfumo huo ili kusaidia wasio na uwezo," alisema.

### ZUIO LA HUDUMA

Katibu wa mtandao wa kampuni za simu, Esther Wangoi, alipendekeza liondolewe zuio ambalo linataka mtu kama hana bima asisajiliwe kwenye mitandao ya simu kwa kuwa litaathiri utoaji huduma na ukuaji wa sekta ya mawasiliano.

Dk. Herenia Sambua kutoka Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA), alishauri muswada huo uhusishe na Tanzania Zanzibar kutokana na wategemezi wengine wako visiwani humo.

Mkurugenzi wa Tanzania Rural Health Movoment (TRHM), Augustino Mhanga, alipendekeza baadhi ya huduma ikiwamo ya tohara iwekwe kwenye kitita ili kuondoa malalamiko yaliyokuwapo kwenye vitita vya NHIF ambavyo vilikuwa havijumuishi huduma hiyo.

Pia alipendekeza kwenye utambuzi wa watu wasio na uwezo wasisahau watoto wanaoishi katika mazingira magumu na mitaani kwa kuwa hawapo kwenye kaya.

### KAMATI YA BUNGE

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Stanslaus Nyongo, alisema kamati hiyo imepokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali ambayo yatatumika kuboresha na kuishauri serikali ili kuwa na sheria bora itakayosaidia kulinda afya ya mtanzania.

"Ni muhimu kanuni baada ya kuandaliwa tuzione maana unaweza kuwa umepita muswada mzuri na sheria nzuri lakini kanuni ikawa tatizo, tumeona hapa kuna mambo mengi yatakwenda kwa Waziri kwenye kanuni inatakiwa iwe rafiki isijeyenyewe ikawa ni tatizo tukakosa nafasi ya kurudi kusema hapa tumekosea," alisema.

"Tuna asilimia 26 ya watu ambao hawana uwezo kabisa, tukisema sheria inasema bima kwa watu wote. Je, hawa wasio na uwezo nani ana wagharamia, tumepata mawazo hapa nchi zingine wanafanyaje. Kuna kodi haya ni mawazo mazuri itasaidia kushauriana na serikali," alisema.

# Hofu wafanyakazi 600 kupoteza ajira Z'bar

**Na Mwandishi Wetu,**

ZANZIBAR

CHAMA cha Waendeshaji Ndege Tanzania (TAOA) kimetoa siku saba kwa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) kusitisha uamuzi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) wa kuiteua Kampuni ya DNATA toka nchini Dubai kuwa mtoa huduma pekee katika Jengo la tatu la (Terminal III) la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

Kwa mujibu wa notisi ya Septemba 14, mwaka huu ya Mkurugenzi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar na Kampuni ya DNATA kutoka Dubai, ndiyo itakuwa mtoaji huduma pekee katika jengo la tatu la (Terminal III) pamoja na huduma ya mizigo na marhaba Lounge kuanzia Desemba mosi, mwaka huu.

Kutokana na hatua hiyo wafanyakazi karibu 600 wapo katika hatari ya kupoteza ajira kutoka katika Kampuni ya huduma za Uwanja wa Ndege (ZAT) pamoja na Kampuni ya Trans Word zinazotoa huduma uwanja huo wa kimataifa wa AAKIA.

TAOA imechukua hatua hiyo kwa mujibu wa indhari (notisi) ya Oktoba 10, mwaka huu, waliyoitoa kupitia Kampuni ya huduma za sheria ya B/E AKO LAW kabla ya kuchukua hatua za kisheria za kufungua kesi mahakamani kupinga uamuzi uliofanywa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa madai ya kufanyika kinyume na sheria.

Waraka uliotolewa na Chama cha TAOA umeeleza hayo kisiwani hapa.

Sehemu ya waraka huo umesema unaelewa kuwa zabuni ya ununuzi wa utoaji wa huduma umechapishwa kinyume na Sheria ya manunuzi na kanuni zilizopo za huduma za utunzaji wa ardhi jambo ambalo linaandika historia ya hatari katika sekta ya Anga Tanzania.

TAO imesema kwa mujibu wa sheria ya usafiri wa anga Tanzania sura ya 80 R.E ya mwaka 2020 kifungu cha 30(e)(II), Mamlaka ya Anga Tanzania (TCAA) ina majukumu ya kuwajengea maarifa kwa umma, ufahamu na uelewa ili kudhibiti sekta na kushughulikia migogoro.

TAOA wamekiita kitendo cha DNATA kuteuliwa kuwa watoa huduma pekee katika Jengo la tatu (Terminal III) ni sawa na serikali kukaribisha sheria za ukiritimba na kuvunja ushindani.

Aidha, kifungu cha 45(2) cha Sheria TCAA, kinataja mamlaka ya kufanya uchunguzi kabla ya mamlaka ya kutoa, kufanya upya au kufuta leseni.

TAOA ilitaja kifungu cha 46 cha sheria kinachotaka TCAA kuzingatia na kusimamia masharti ya ushindani mzuri, yanakuwapo katika soko kwa ajili ya kuepusha mambo yoyote yanayoweza kuathiri ushindani na kuleta madhara kwa umma na maendeleo ya sekta ya anga.

Vile vile, imetajwa kanuni ya 20 ya usafiri wa Anga (Ground handling services) ya mwaka 2012, taratibu za uteuzi zinahitajika ili kushughulikia ardhi katika viwanja vya ndege na kuzingatia kanuni za uwazi, zisizo na ubaguzi wa utoaji wa zabuni ya ushindani wa kimataifa na kuepuka upendeleo.

Juhudi za kumpata Mkurugenzi Mkuu wa Mmalaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Hamza Johari kupitia simu yake ya mkononi hazikufanikiwa licha ya indhari ya siku saba ya TAOA kumalizika Oktoba 19, mwaka huu.

# Wauguzi wafutiwa leseni kwa kusababisha kifo cha mjamzito

**Na Ally Hengo,**

KIBAHA

BARAZA la Wauguzi na Ukunga Tanzania (TNMC), limewafutia leseni wauguzi wasaidizi wawili wa Hospitali ya Wilaya ya Mkomaindo, Masasi mkoani Mtwara, baada ya kupatikana na hatia ya uzembe uliosababisha kifo cha majamzito na mtoto wake.

Wauguzi hao Elizabeth Njenga na Pascal Mnyalu, walishtakiwa kwenye baraza hilo pamoja na wauguzi wengine watatu na madaktari wawili, wote wa hospitali hiyo kuhusika na uzembe uliopoteza maisha ya mjamzito Aisha Romanus.

Wauguzi wengine waliofikishwa katika baraza hilo ni Joyce Nkane na Tumaini Milanzi ambao walipewa onyo kali na Lucia Liababa, ambaye alifutiwa shtaka lake baada ya kuonekana kutohusika moja kwa moja.

Kabla ya hukumu hiyo iliyotolewa na Mwenyekiti wa Baraza hilo, Lilian Msele, pia aliwatia hatiani madaktari wawili wa hospitali hiyo, Amina Mushi na Hashimu Chiwaya, ambao taarifa zao zitapelekwa kwenye Baraza la Madaktari ili hatua stahiki zichukuliwe.

Awali dada wa marehemu Agnes John, alilieleza Baraza hilo kuwa Novemba mosi, mwaka jana, mdogo wake Aisha, alishikwa na uchungu wa uzazi na kuamua kumfikisha zahanati ya Lukuledi na muuguzi wa zahanati hiyo baada ya kumpima aliwaeleza waende hospitali ya Wilaya ya Mkomaindo.

Alisema, hata hivyo alipopiga simu hospitali hiyo ya wilaya wauguzi walimjibu hawakuwa na mafuta ya kutumia kwenye gari la wagonjwa na kulazimika kukodi bajaji ambayo pia iliharibika njiani na baada ya matengenezo walifika saa moja usiku hospitali ya Mkomaindo.

Agnes alisema baada ya kupokewa mgonjwa wake hakupata huduma haraka na kuambiwa aondoke jambo alilolipinga na muda mfupi alimuona mdogo wake akiomba msaada kwa wauguzi hao, lakini hawakumjali na ilipofika usiku wa saa tano akaaga dunia.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001:2015

## TAARIFA KWA UMMA

### USAJILI WA NAMBA YA UTAMBULISHO WA MLIPAKODI (TIN) KWA WAAJIRIWA

***Dar es salaam, Oktoba 18, 2022***

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuukumbusha umma kuhusu waajiriwa kuwa na Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) ikiwa ni matakwa ya Kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438 R.E 2019. Matumizi ya TIN sahihi ni muhimu katika kuweka kumbukumbu sahihi za waajiriwa na kuwezesha uwasilishaji wa ritani ya kodi za waajiriwa yaani Pay as You Earn (PAYE) kwa kutumia mfumo wa a uwasilishaji wa ritani kielekroniki (e-filing).

Ikumbukwe kuwa, Mamlaka iliagiza waajiri wote wahakikishe waajiriwa wao wana TIN na kuanza kuzitumia kikamilifu ifikapo tarehe 31 Desemba 2020. Pamoja na ukweli kwamba waajiri wengi wameonesha mwitikio chanya bado kuna kundi dogo la waajiri ambao wameshindwa kusimamia matakwa hayo ya kisheria na wamekuwa hawatumii TIN sahihi za waajiriwa au kutumia TIN 999 999 999 ambayo ilikua ni ya mfano katika kipindi cha mpito.

kufuatia hilo, Mamlaka inapenda kuwakumbushwa waajiri na waajiriwa wote kuhakikisha kuwa wanazingatia takwa hili la kisheria la kuhakikisha matumizi sahihi ya TIN. Ikumbukwe kuwa TIN hutolewa bure na Mamlaka na upatikanaji wake ni rahisi. Kwa waajiriwa wenye namba za usajili (NIN) inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), wanaweza kuomba TIN kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa online TIN Registration unaopatikana kwenye tovuti ya TRA (ambayo ni **www.tra.go.tz**). Waajiriwa wasio na NIN wanalazimika kutembelea Ofisi za TRA ili kufanya maombi na kupatiwa TIN.

Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizo Karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo:

**Tovuti** : **www.tra.go.tz**
**Namba za Simu bila malipo** : **0800 750 075 / 0800 780 078 au 0800110016**
**WhatsApp** : **0744 23 33 33**
**Barua pepe** : **huduma@tra.go.tz**

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**Imetolewa na:**

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**
**TRA MAKAO MAKUU**

217098402

# Serikali yashauriwa kushirikisha wataalamu wa miradi ya ujenzi

**Na Romana Mallya**

UTELEKEZAJI wa miradi katika viwango duni ikiwamo ya serikali unatokana na kutokushirikishwa wataalam wa fani husika wakiwamo wabunifu majengo na wakadiriaji ujenzi.

Akizungumza katika mkutano wa tatu wa mwaka, jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Dk. Ludigija Bulamile, aliishauri serikali kila mradi wa ujenzi ushirikishe wataalam wa aina zote wa ndani ili iweze kudumu muda mrefu.

Alisema lengo la mkutano huo ni kuwanoa wataalam ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia ya ujenzi na mada kuu ikiwa ni 'Uhifadhi wa Majengo kwenye Miji ya Afrika kwa sasa'.

Dk. Bulamile alisema, mada hiyo inakumbusha umuhimu wa uhifadhi wa urithi wa majengo na maeneo ya kihistoria katika kazi zao za kila siku na ubora wa ujenzi unahitajika ili majengo yaweze kuwa himilivu na endelevu.

"Tukumbuke majengo tunayojenga kwa sasa kwa vizazi vijavyo yatakuwa ya kale, tunapojenga lazima tukumbuke kufuata au kutumia wataalam wanaostahili ili yaishi.

"Kwa sasa tunajenga majengo mengi sana, lakini ukiangalia ubora wake haufikii unaotegemewa jengo kuishi muda mrefu, kimsingi mpango miji una kipindi cha mpito kilichogawanyika sehemu tatu, majengo yanayoishi miaka 33, 66 na 99."

Alisema wanapojenga jengo la miaka 30 linatakiwa kutumia gharama ndogo linaloweza kuishi miaka 33 ili baada ya hapo serikali iweze kubadili matumizi ya ardhi na kutaka majengo mengine yenye umri zaidi.

"Kwa sasa miji inazidi kupanuka kwa kuwa hatufuati sheria ya muda maalum ya utoaji maeneo, unakuta maeneo kama Mwananyamala au Sinza kipindi cha mpito kilikuwa ni miaka 33 na ilishaisha hivyo kwa sasa ni wakati wa kuibadilisha Sinza ili eneo liwe na majengo makubwa zaidi yanayochukua watu wengi badala ya kuupanua mji kwenda nje.

"Matokeo yake gharama za usafiri kuja kufanya kazi mjini inakuwa kubwa zaidi na ukarabati wa mji ukipanuka unakuwa mgumu zaidi, jengo la serikali lazima liishi zaidi ya miaka 66 au miaka 99."

Alitoa mfano barabara ya njia nane kutoka Kimara hadi Kibaha lengo lilikuwa ni kuhakikisha magari yaende mwendo kasi kutokana na foleni, lakini kwa sababu haukushirikisha watalaam wote wanaotakiwa kushiriki kila baada ya mita 500 au kilometa moja kunakuwa na eneo la wavuka kwa miguu.

"Ukitaka kwenda hospitali ya Mlongazila ilikuwa ufike kwa urahisi, lakini kwa sababu ya kutoshirikisha wataalam, mnakwenda kujenga daraja kwenye mlima mnatumia gharama kubwa zaidi unaacha bonde ambalo mngelitumia kupita chini watu wakaenda Mlongazila," alisema.

Alisema serikali kupitia Sheria ya Manunuzi ya Umma imeruhusu taasisi za umma kutekeleza miradi ya ujenzi kwa kutumia watalaam wake wa ndani kwa lengo la kupunguza gharama za uendelezaji wa miradi.

Aidha, alisema changamoto za miradi iliyojitokeza kwa utaratibu huo ni baadhi ya taasisi za umma kutekeleza miradi mikubwa bila kutumia wataalam wote wa ndani.

"Unakuta mkuu wa taasisi kama daktari anajenga jengo hospitali tunakupa fedha kiasi hiki anajenga, matokeo yake mnampa adhabu wakati hamstahili ushauri wetu wa bodi taasisi zinazotekeleza miradi kwa mfumo wa manunuzi wawe na wataalam wote wanaotakiwa katika majenzi," alisema.




Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba (wa nne kulia), akipokea msaada wa madawati 100 kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu (wa nne kushoto), ikiwa ni jitihada za benki hiyo katika kuboresha elimu mkoani humo jana. Wanaoshuhudia ni pamoja na Katibu Tawala Mkoa huo, Pili Mnyema (kulia), Ofisa Elimu wa Mkoa huo, Newaho Mkisi na baadhi ya maofisa waandamizi wa mkoa na benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania yamwagiwa bil. 5/- uendelezaji kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

DENMARK na Sweden zimetoa zaidi ya Sh. bilioni tano katika kuendeleza kilimo hasa katika uzalishaji wa alizeti, maharage na mbaazi katika msimu wa kilimo wa mwaka huu.

Nchi hizo ambazo ni washirika wakubwa na wa muda mrefu wa Tanzania, kupitia ufadhili huo, zimelenga kuboresha sekta hiyo kupitia mazao hayo kupitia wakulima wadogo na mpango huo unalenga kuwafikia zaidi ya wazalishaji 100,000.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari, ufadhili huo utahusisha miradi tisa ya maendeleo ya masoko ya kilimo katika mikoa 11 chini ya taasisi za sekta binafsi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Masoko ya Kilimo (AMDT).

Taarifa hiyo ilisema ufadhili huo wa Denmark na Sweden unatoa mchango katika vipaumbele vya serikali ya Tanzania katika mageuzi ya sekta ya kilimo. Kilimo ni mwajiri mkubwa kwa Tanzania.

Miongoni mwa maeneo ambayo ufadhili huo unalenga ni kuimarisdha upatikanaji wa mbegu bora, upatikanaji wa fedha katika mazao husika, huduma za maendeleo ya biashara na matumizi bora ya kanuni za kilimo ikiwamo uzimamizi wa mazao baada ya kuvuna.

Sambamba na hayo, mradi huo pia utasaidia kuboresha upatikanaji wa huduma za ushauri vijijini na uongezaji wa thamani katika alizeti na mikunde.

Akizungumzia ufadhili huo jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa AMDT, Charles Ogutu, alisema mpango huo unatarajia kuinufaisha mikoa ya Manyara, Singida, Dodoma, Morogoro, Arusha, Lindi, Mtwara, Songwe, Ruvuma, Njombe na Rukwa.

"Ufadhili huu ni kwa ajili ya msimu wa kilimo wa mwaka 2022/23 na inatarajiwa kuwa miradi itakayofanya vizuri kupitia ufadhili huu, itaongezewa ufadhili hadi mwaka 2024.

"Zaidi ya hayo, matumizi sahihi ya hali ya hewa na teknolojia katika kilimo vitaimarishwa katika sekta zote ikiwa ni jitihada za kupambana na mabadiliko ya tabia nchi," alisema.

Ogutu pia alisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi kwa ajili ya maendeleo ya kilimo Tanzania. Mageuzi ya sasa ya kidunia yanatoa wito kwa nchi zinazoendelea na kuibuka kiuchumi kuunganisha nguvu na kutumia fursa zinazojitokeza kwa ajili ya kipato na usalama wa chakula kutokana na maafa yanayoyakabili mataifa yakiwamo vita, ukame na changamoto za masoko.

Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Kilimo, imekuwa ikitilia mkazo kuonyesha njia katika kutenga bajeti kubwa huku ikiweka wazi vipaumbele vya kimaendeleo kupitia sekta ya kilimo.

## Mkutano wa kumuenzi Maalim Seif kufanyika Jumamosi na Jumapili

**Na Elizabeth Zaya**

MKUTANO wa pili wa kumuenzi aliyekuwa Makamu wa kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, unatarajiwa kufanyika Oktoba 22 na 23, mwaka huu, Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwenye vyombo vya habari na Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa taasisi ya Maalim Seif Foundation, Ismail Jussa Ladhu, mkutano huo unatarajiwa kufunguliwa na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Masoud, na kufungwa na Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana.

"Mkutano wa kila mwaka ndiyo tukio kuu katika shughuli zinazoandaliwa na taasisi hii kwa ajili ya kumuenzi Maalim Seif ikiwa na malengo ya kukuza demokrasia kupitia majadiliano na diplomasia, kuendesha programu zinazolenga kujenga na kustawisha maridhiano, kuishi katika haki, amani na kuheshimiana, utatuzi wa migogoro, utengamano baina ya watu na jamii mbalimbali," alisema Jussa akibainisha kuwa maudhui ya mkutano huo ni elimu na ukuzaji vipaji, ubunifu na uwezeshaji.

"Maudhui haya yamechaguliwa ili kwenda sambamba na mjadala wa umma unaoendelea kuhusu haja ya kufanyika mabadiliko katika mfumo wa elimu Zanzibar na duniani kwa ujumla kwa kuhusisha maisha na dira ya Maalim Seif.

"Mkutano huu utawaleta pamoja wahusika wakuu kutoka sekta ya umma na binafsi ili kuzungumza kuhusu hali ya elimu ilivyo Zanzibar hivi sasa, na kwa pamoja kuainisha fursa zilizopo katika kuleta maendeleo ya sekta hii kwa kuangalia uzoefu wa nyuma na mitindo pamoja na mifumo ya kisiasa iliyothibitika kuwa na manufaa katika nchi za Afrika na duniani," alisema Jussa.

Alisema miongoni mwa wageni mashuhuri walioalikwa katika mkutano huo ni pamoja na Waziri wa Elimu wa zamani wa Zimbabwe, David Coltart na wasomi mbalimbali kutoka hapa nchini wakiwamo Prof. Issa Shivji na Prof. Kitila Mkumbo.

Waalikwa wengine ni Balozi mstaafu wa Marekani nchini, Mark Green na Balozi mstaafu wa Umoja wa Ulaya (EU), Roeland Van de Geer ambao watazungumza katika mkutano huo kwa njia ya mtandao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TNMC kuwafutia leseni wauguzi kwa uzembe ni sahihi

**WAUGUZI** waliofutiwa leseni na Baraza la Wauguzi na Ukunga Nchini (TNMC) kwa uzembe uliosababisha mjamzito kupoteza maisha na mtoto wake, ni hatua nzuri ya kukomesha uzembe kazini.

Wauguzi hao ni wa Hospitali ya Mkomaindo, wilayani Masasi mkoani Mtwara.

Hatua iliyofikiwa na baraza hilo imetoka na maelezo yaliyotolewa na ndugu wa mjamzito aliyefariki na baraza hilo kuridhishwa na ushahidi huo.

Wauguzi waliofutiwa leseni zao ni Elizabeth Njenga na Pascal Mnyalu ambao walishtakiwa kwenye baraza hilo pamoja na wauguzi wengine watatu na madaktari wawili, wote wa hospitali hiyo kuhusika na uzembe uliopoteza maisha ya mjamzito Aisha Romanus.

Wauguzi wengine Joyce Nkane na Tumaini Milanzi walipewa onyo kali na mwingine Lucia Liababa, alifutiwa shtaka lake baada ya kuonekana kutohusika moja kwa moja na uzembe huo.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Lilian Msele, aliwatia hatiani madaktari wawili wa hospitali hiyo, Amina Mushi na Hashimu Chiwaya, ambao taarifa zao zitapelekwa kwenye Baraza la Madaktari ili hatua stahiki zichukuliwe.

Adhabu waliopewa wauguzi hao iwe fundisho kwa wengine wenye tabia ya kupuuza wagonjwa wanapokuwa na uhitaji hasa kwenye jambo la dharura.

Kilio cha wagonjwa wengi, hasa wajawazito ni unyanyasaji au kupuuzwa wanapokuwa kwenye hali ya uchungu na kujibiwa lugha zisizostahili au kuachwa wakihangaika wenyewe mpaka wengine kufikia hatua ya watoto kutoa bila kupata msaada wa muuguzi.

Katika hukumu iliyotolewa na baraza hilo, ilielezwa kuwa dada wa marehemu Agnes John, alilieleza Baraza kuwa Novemba mosi, mwaka jana, mdogo wake Aisha, alishikwa na uchungu wa uzazi na kuamua kumfikisha zahanati ya Lukuledi na muuguzi wa zahanati hiyo baada ya kumpima aliwaeleza waende Hospitali ya Wilaya ya Mkomaindo.

Hata hivyo alipopiga simu hospitali hiyo ya wilaya wauguzi walimjibu hawakuwa na mafuta ya kutumia kwenye gari la wagonjwa na kulazimika kukodi bajaji ambayo pia iliharibika njiani na baada ya matengenezo walifika saa moja usiku Hospitali ya Mkomaindo.

Agnes alisema baada ya kupokewa mgonjwa wake hakupata huduma haraka na kuambiwa aondoke jambo alilolipinga na muda mfupi alimuona mdogo wake akiomba msaada kwa wauguzi hao, lakini hawakumjali na ilipofika usiku wa saa tano akaaga dunia.

Wajumbe wa baraza hilo ambao waliwahoji madaktari na wauguzi hao walishangazwa na maelezo ya wauguzi hao kuwa tofauti kiasi cha mjumbe mmoja wa baraza kukerwa kutokana na maelezo waliyoyawasilisha awali baada ya kutakiwa kuandika taarifa kutofautiana na waliyokuwa wakiyatoa.

Baraza hilo liliamua wauguzi hao kutotakiwa kufanya shughuli zozote za kiuguzi kutokana na kukiuka kanuni na viapo vyao walivyokula, pia ililaumu uongozi wa hospitali hiyo kutokuwa na ufuatiliaji wa watumishi wake ambao kama ungekuwa mzuri maafa kama hayo yasingeweza kutokea.

Msajili wa Baraza hilo, aliwataka wananchi kufikisha malalamiko yao waonapo hawatendewi haki na wauguzi na madaktari ili wachukue hatua stahiki huku akibainisha kuanza kusikiliza kesi nyingine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Elimu ya malezi itolewe kwa wazazi kuepuka madhila haya ya kutisha

Na Halfani Chusi

**KUNA** haja wazazi kupewa elimu juu ya malezi, ili kupunguza vifo vya wazazi kuwaua watoto wao kwa kuwapa adhabu zisizo stahili au kuwakatili wakiamini kama wanawaonya.

Matukio mengi ya wazazi kuwapiga watoto hadi kuwajeruhi kwa kipindi hiki, yameongezeka hii inawezekana ni kutokana na baadhi yao kuwa na uelewa mdogo namna ya kulea.

Katika matukio hayo, ukitazama makosa unakuta mtoto wa miaka minne kadokoa mboga au amevunja glasi au wakati mwingine kafanya kosa ambalo pengine halistahili hata adhabu lakini mtoto anaadhibiwa.

Kupitia hilo, naishauri serikali na wadau wengine wa maendeleo kuanza kutoa elimu kwa wazazi juu ya malezi ya watoto, naamini hii itawaongeza uelewa katika kujua namna bora ya kumdhibiti mtoto akifanya kosa kinyume na kipigo.

Au hata kama kosa lake linahitaji kipigo basi wataelekezwa maeneo yapi ni sahihi kupiga ili yasitokee madhara ikiwamo kuwapa ulemavu watoto.

Siku chache zilizopita, gazeti Nipashe limekuwa likiripoti matukio mengi wanayofanyiwa watoto na wazazi wanapoadhibiwa, kitu ambacho kinabeba tafsiri kwamba yawezekana wengi wao hawana uelewa juu ya kuadhibu na kulea.

Ikumbukwe, kumuadhibu mtoto sio njia pekee ya kumfunza bali zipo njia nyingi za kutumia kumfundisha mtoto anapokuwa amekosea, kinyume na kumuadhibu

Mtoto ni mtu anayekariri kitu kwa haraka zaidi kuliko mtu mzima. Hii ni kutokana na kutokuwa na mrundikano wa mambo mengi kichwani kwa hiyo kupitia hali hiyo inawezekana kabisa akaelekezwa na akaelewa na kukariri mapema.

Ni dhahiri kwamba, taasisi nyingi za kiserikali na binafsi hazijagundua upande wa pili wa sarafu, kuwa wazazi wengine wana uelewa mdogo na hivyo

**Lakini, katika kuchunguza nilibaini kuwa hata wazazi ambao wameikuta wameingia kwenye kashfa ya kuua wakiadhibu watoto baadhi yao ni wale ambao walizaa mapema katika umri usiostahiki.**

kuunda tume ya kuwapatia elimu kama ilivyo kwenye mambo ya haki za watoto, ukatili wa kijinsia, semina za magonjwa na rushwa ya ngono.

Hivyo, kuna haja ya kuundwa kwa taasisi mahususi itakayolitazama hilo ili kuipeleka elimu, hiyo mbali hadi kupunguza vifo vya watoto vinavyotokana na kipigo, kutoka kwa wazazi pale wanapowaadhibu.

Hilo linabeba taswira hasi, kutokana na kile kitendo cha mtoto aliyeadhibiwa na mama yake huko kwa kudokoa dagaa na kuiba Sh.250, adhabu hiyo inaweza kumpa mtoto ulemavu wa kudumu.

Ukiangalia kwa muktadha huo, huoni sababu ya mama kuwasha moto na kumchoma mtoto wake mikono ikiwa ni sehemu ya kumuonya aache wizi.

Lakini, katika kuchunguza nilibaini kuwa hata wazazi ambao wameikuta wameingia kwenye kashfa ya kuua wakiadhibu watoto baadhi yao ni wale ambao walizaa mapema katika umri usiostahiki.

Hali iliyowasukuma kuingia katika majukumu ni bila kujua namna kuishi ndani ya majukumu hayo, mambo kama haya yameenea sehemu nyingi hasa uswahilini, unakuta mtoto ana mtoto. Bila shaka, katika muktadha huo, sio rahisi huyo mwanamke kujua namna bora ya kulea.

Kwa vyovyote vile, lazima itakuwa tofauti tu kwa hiyo ili kukikomboa kizazi kijacho kwa manufaa ya kutengeneza taifa bora na kizazi chenye usawa kuna haja ya kulibeba hili na kulifanyia kazi kikamilifu.

Ikiwa ni pamoja na kuwaeleza wazazi adhabu watakazokumbana nazo, pale watakapobainika na kosa la kuadhibu mtoto kinyume cha sheria, kwa sababu, pia wengi wao wanafanya bila kujua nini madhara yake baadaye.

Likishawakuta, wanaanza kujuta na wengi hudhani kumwadhibu mtoto, hakuna kesi hata kama utamwadhibu kinyume na sheria za nchi zinavyotaka.

## HABARI KITAIFA



Daktari wa Magonjwa ya Saratani wa Hospitali ya Saratani ya Ocean Road, Dk. Masoud Mwangoma (kulia), akimtoa damu mfanyakazi wa kiwanda cha mabati cha ALAF, Adrian Sigalla, wakati wa semina maalum iliyoandaliwa na kiwanda hicho, kwa ajili ya kuwapima wafanyakazi wake magonjwa ya saratani jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wazazi wadaiwa kutisha watoto wasifaulu mitihani

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

BAADHI ya wazazi wilayani Makete, mkoani Njombe, wamedaiwa kuwatisha watoto wao wanaohitimu elimu ya msingi kufanya vibaya kwenye mitihani kwa madai wakifaulu wao watafariki dunia.

Hayo yalielezwa jana na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Lupila, Tumwanukye Ngakonda, na kukiri kuwapo kwa wazazi hao baada ya wanafunzi kuhojiwa kutokana na mabadiliko yao ya kitaaluma kuelekea wakati wa kufanya mtihani wao wa mwisho na kueleza kushinikizwa kufanya vibaya kwa kuhofia kuwapoteza wazazi wao.

Alidai wanafunzi wanajifelisha kutokana na kusongwa na wazazi kwa kigezo kwamba wakifaulu watashindwa kuwasomesha kutokana na uchumi mgumu.

"Utafiti tulifanya kwa sababu kuna baadhi ya watoto unakuta darasa la kwanza la pili, nne, tano na sita, pengine na baadhi ya mitihani ya nyuma ile ya darasa la saba kabla ya taifa anakua amefanya vizuri, lakini yanapokuja matokeo ya darasa la saba wanafeli," alisema Tumwanukye na kuongeza:

"Kwa sababu ya changamoto hiyo Wilaya ya Makete tumejiwekea mikakati ya kusimamia ipasavyo elimu kwa kuhakikisha kila mwanafunzi aliyefaulu anaripoti shuleni na kuendelea na masomo ya sekondari."

Alisema baada ya kugundua tatizo hilo, wamechukua hatua ikiwamo kutoa elimu kwa wanafunzi kutokubali kufeli na katika elimu hiyo wanakutana na shuhuda mbalimbali, ikiwamo wazazi kuwaambia watoto wao kuwa wakifaulu watafariki dunia au hawatakuwa watoto wao.

Aliwaomba wafanyabiashara na wadau wengine wa maendeleo kutokubali kuwa sehemu ya kuwatorosha wanafunzi kwa kigezo cha kwenda kuwapa ajira na badala yake waungane kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu.

Naye Ofisa Elimu Kata ya Lupila, Gabriel Sanga, alimuagiza Mkuu wa Shule ya Sekondari Lupila kufanya tathmini kwa kila kijiji cha kata hiyo wanafunzi wangapi walianza kidato cha kwanza na wangapi wamehitimu kidato cha nne.

"Wangapi wamejiunga na kuhitimu kidato cha sita na kwenda chuo kikuu ili wadau wa elimu wafahamu hali ilivyo, na kama mambo hayaendi waone chakufanya kwa sababu kata hiyo ni yao wote hivyo hawategemei kuona kijiji kimoja kiwe na wasomi na vijiji vingine kukosa wasomi," alisema Sanga.

## Raia China mahakamani madai ya kukutwa na nyara za serikali

**Na Grace Gurisha**

RAIA wa China Yu Bo, amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu akikabiliwa na shtaka la kukutwa na vipande 81 vya meno ya tembo na kakakuona wawili wenye thamani ya Sh. 3,044,130.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Adolf Lema, jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate, alidai kuwa mshtakiwa anatuhumiwa kwa mashtaka mawili yakukutwa na nyara za serikali.

Alidai, Desemba 30, 2013 katika Bandari ya Dar es Salaam, mshtakiwa huyo alikutwa na vipande 81 vya meno ya tembo vyenye thamani ya Sh. 975,076,350.

Ilidaiwa kuwa katika tarehe na eneo hilo, mshtakiwa huyo pia alikutwa na kakakuona wawili wenye thamani ya Sh. 3, 044,130 mali ya serikali bila kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Hakimu alimweleza mshtakiwa kwamba mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo na haruhusiwi kujibu lolote.

Upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kuiomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu alikubali ombi hilo na kuipanga Novemba 11, 2022 kwa kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ulipofikia.


FARM AFRICA

JOB OPPORTUNITIES

| | |
|---|---|
| Job Opportunities: | (4) Field Associate (Field Officer) and (2) Monitoring, Evaluation and Learning (MEL) Associate |
| Duty Station: | Babati/Singida/Dodoma |
| Duration: | All positions are full time, fixed term contract |
| Salary: | Attractive salary & benefit package |

Farm Africa is a leading international NGO specialising in Agriculture, Natural Resource Management and Market Engagement in Tanzania and across Eastern Africa.

Farm Africa is currently recruiting for six staff to join our team in the implementations of current projects in Manyara, Dodoma, Singida and Morogoro regions at different capacities.

For further details of any of the available positions, please visit our website at **www.farmafrica.org/jobs/jobs**.

If you believe you have the skills and experience required for any of the above positions, please submit a CV (maximum 3 pages) and a covering letter (maximum 1 page) that explains how you meet the job requirements and your preferred duty station, to **Tanzaniarecruitment@farmafrica.org** by 11:59pm (EAT) on Monday , **31st of October 2022**.

Farm Africa is an equal opportunities employer and we welcome applications from a diverse range of candidates.


## KABWELA



# Sumukuvu bado tishio afya ya binadamu

**Na Elizabeth Zaya**

MRATIBU wa Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANPAC), Khassim Msuya, ameeleza namna sumukuvu inavyoathiri afya ya binadamu kwa muda mfupi na mrefu, huku akitaja ini na figo kuwa ni miongoni mwa vinavyoathiriwa zaidi na sumukuvu hiyo.

Kwa mujibu wa Msuya, vitu vingine vinavyoathirika ni mfumo wa fahamu, uwezo wa damu kuganda na kusababisha kifo.

Athari nyingine alisema ni pamoja na kupungua kwa kinga ya mwili na upungufu wa damu.

Msuya alisema athari hizo hutokea hususani pale mtu anapokula kiasi kingi cha sumukuvu na kwamba ni hatari kwa sababu hata baada ya chakula kupikwa huendelea kubaki na kuleta athari kwa mtu anayekitumia kwa kipindi cha muda mfupi au mrefu kulingana na kiwango cha sumukuvu kilicholiwa.

"Sumukuvu ni hatari kwa sababu inapokuwapo kwenye mazao au bidhaa huwa haionekani kwa macho, na huendelea kubaki hata baada ya chakula kupikwa au kusindikwa," alisema Msuya.

"Baada ya mtu kula chakula hicho, madhara ya kiafya huanza kujitokeza kwa muda mfupi au muda mrefu kutegemeana na kiasi cha sumukuvu kilichopo kwenye chakula chenye uchafuzi kilicholiwa, idadi ya milo, umri na hali au kiafya ya mlaji husika."

Alielezea namna mazao yenye dalili ya sumukuvu yanavyoonekana kuwa ni pamoja kuonyesha ukungu, kuvu na harufu ya uvundo.

Nyingine alisema ni punje kutengeneza vumbi, kugandamana au kubadilika rangi kutoka ya asili na kuwa nyeusi iliyochanganyika na kijivu, kijani, chungwa au njano.

"Na vichochezi vya sumukuvu kwenye mazao ya chakula ni hali ya hewa ya jotoridi, unyevunyevu, ukame, mafuriko na mvua zisizotarajiwa wakati mazao yanapokaribia kukomaa na wakati wa kuvuna," alisema Msuya.

Aliwataka wakulima kuzingatia kanuni bora za uzalishaji wa mazao ya chakula, ili kuidhibiti sumukuvu na kuepusha madhara zaidi kwa walaji.



Balozi wa Comoro nchini, Dk. El Badaoui Fakih, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akilishukuru Shirika la Ndege la Precision Air, baada ya kuanza kutoa huduma ya usafiri wa ndege kati ya Comoro na Tanzania kwa wiki mara tatu. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, Patrick Mwanri. **PICHA: JUMANNE JUMA**






## Wadau wakutanishwa kubaini fursa Mfuko wa Akiba

**Na Beatrice Moses**

WADAU wa sekta ya fedha kutoka benki mbalimbali nchini na madalali wa soko la fedha wamekutanishwa kubaini fursa kwenye Mfuko wa Akiba wa uwekezaji kiuchumi kwa wananchi wa kipato cha chini na kati.

Uwekezaji huo unasimamiwa na Watumishi Housing Investment (WHI) iliyoko chini ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mkurugenzi Mtendaji wa WHI amesema Akiba Fund ni fursa ya uwekezaji mkubwa wa pamoja wa fedha kwa kiwango kidogo cha kuanzia Sh. 10,000 hadi 5,000 hatua ambayo inampa nafasi mwekezaji kuimiliki vipande ambavyo anaweza kuviuza au kuendelea kupokea faida kulingana na uwapo wa mfuko huo.

Alisema ni uwekezaji katika vipande ili kupata mapato shindani kupitia ukuaji wa mitaji na kutengeneza utamaduni wa kuwekeza katika masoko ya fedha na mitaji ambayo yana uhakika wa kipato kwa mwekezaji.

"Mfuko huu ni salama umethibitishwa na mamlaka ya mitaji na masoko (CMSA), kwa watakaoanza nao kuwekeza Novemba mosi, mwaka huu hawatalipa gharama za kuingia kutakuwa na faida kadhaa za kujiunga na mfuko huu kubwa ni kuwekeza kwa uhakika," alisema.



Dk. Msemwa alisema wawekezaji wanaokaribishwa ni wananchi wote wa ndani na nje ya nchi, unahusisha watu binafsi na wawekezaji wasio watu binafsi, benki/mashirika, taasisi za serikali na binafsi.

Mkuu wa Kitengo cha fedha wa WHI, Pascal Masawe, alisema malipo ya mfuko huo yanafanywa kwa mfumo wa serikali, mtu anaweza kujiunga kupitia simu na sio rahisi kufanyika udanganyifu wa aina yoyote.

Alisema hatua za uuzaji wa vipande utafanyika kila siku, mfuko utatuma taarifa ya malipo ya vipande ndani ya saba za wiki, mapato ya mfuko hatayakuwa na kodi ya mapato kwa wawekezaji.

Akizungumzia usalama wa uwekezaji huo, Mkuu wa Idara ya Mtaji na Masoko wa Benki ya CRDB, Masumai Ahmed (pichani) ambao ndiyo wasimamizi wa uwekezaji huo, aliwahakikishia wananchi Akiba Fund ni mahali salama kwa uwekezaji.

# Jela maisha kwa kumnajisi mtoto

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MAHAKAMA ya Wilaya Nkasi mkoani Rukwa, imemhukumu kifungo cha maisha jela mfanyabiashara wa mjini Namanyere, Athanas Exavery (32), kwa kosa la kumnajisi mtoto wa kike wa miaka saba.

Hukumu hiyo iliyotolewa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Nkasi, Denis Luwungo, ilisema mtuhumiwa huyo amekutwa na hatia kwa kutenda kosa hilo.

Alisema mahakama imejiridhisha pasipo shaka na kwamba ni baada ya upande wa mashtaka kupeleka mashahidi sita na vielelezo sita ambavyo vilipitiwa na kujiridhisha alitenda kosa hilo na kustahili kifungo cha maisha jela.

Awali, upande wa mashtaka ukiongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Jeshi la Polisi Mkaguzi Msaidizi, Denis Chagike, ulidai mtuhumiwa alitenda kosa hilo Septemba 11 na 12, mwaka huu, kwa kumnajisi mtoto huyo katika soko la Majengo mjini Namanyere.

Aidha, Mwendesha Mashtaka aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mtuhumiwa huyo ili iwe fundisho kwa wengine.

Wakili wa mshtakiwa, Peter Kamyalile, aliiomba mahakama impunguzie adhabu kwa sababu mtuhumiwa Athanas Exavery bado ni kijana na taifa linamhitaji na anategemewa na familia yake.

Hakimu alitupilia mbali utetezi huo na kumhukumu kifungo cha maisha jela.

HABARI KITAIFA

# Hakimu apata udhuru kesi ya raia wa Guinea

**Na Grace Gurisha**

KESI ya kukutwa na vipande 660 vya meno ya ndovu inayomkabili mfanyabiashara Ally Anguzuu, raia wa Guinea na wenzake 10 imeshindwa kuendelea na kusikilizwa kutokana na hakimu anayeisikiliza kupata udhuru.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Caroline alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Avodia Kyaruzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuwa kesi ililetwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa, lakini hawaoni mawakili wa utetezi na kesi ilipangwa asubuhi.

Pia, alidai kuwa wamepata taarifa kwamba hakimu husika anayesikiliza kesi hiyo, Hakimu Mkazi Mwandamizi Rhoda Ngimilanga, hayupo na kuomba tarehe nyingine ya kukutana na mawakili wa utetezi ili wapange kesi isikilizwe mfululizo.

Hakimu Kyaruzi aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 31, 2022 kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa.

Awali, Ofisa wanyamapori kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Kiza Yusuph, alidai kuwa alibaini vipande 660 vya meno ya tembo vimetokana na kuuawa kwa tembo 143 wenye thamani ya Sh. bilioni 4.6.

Alifafanua kwamba alibaini kama vipande hivyo ni meno ya tembo baada kuchukua kipande kimoja kimoja kuangalia umbo lake, rangi za mpangilio zenye nyeupe, uwazi uliyokuwapo, uzito na harufu yake, ambayo aliibaini kutokana na uzoefu aliyokuwa nao wa miaka zaidi ya 20.

Pia, alidai aligundua ni vipande 660 baada ya kuvihesabu na pia alipima uzito kila jino kwa kutumia mzani aliotumia ambao ulikuwa ni wa ghala la serikali na alirekodi uzito wa kila jino.

Alidai tembo mmoja ana thamani ya Dola za Marekani 15,000, na kwa kipindi hicho Shilingi ya kubadilisha ilikuwa 2,171 kwa dola moja. Tembo 143 thamani yake ni Sh. 4,656,795,000.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mfanyabiashara Victor Mawala, Haruni Abdallah, Abbas Hassan, Solomoni Mtenya, Khalfani Kahengele, Ismail Kassa, Juma Buguma, Kassim Saidi, Peter Nyachiwa, John Buhanza na Mussa Abdallah, wote wakazi wa Dar es Salaam.

Katika kesi hiyo, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka ya kujihusisha na nyara za serikali bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa wanyamapori, ambazo ni meno hayo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 4.6.

Washtakiwa hao wanadaiwa kuwa na mtandao mkubwa wa uhalifu wa ujangili ambao unajihusisha na kuuza na kununua, kupokea na kuhamisha, kusafirisha nyara za serikali ambazo ni meno ya tembo.

# Mavunde ataka mpango matumizi ya ardhi kujumuisha mashamba makubwa

**Na Munir Shemweta,** SHINYANGA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, ameagiza watendaji wa serikali kuhakikisha maeneo yote ambayo migogoro ya ardhi imetatuliwa, yapangiwe mipango ya matumizi ya ardhi kwa kujumuisha mashamba makubwa ya kilimo badala ya kupanga maeneo ya makazi pekee.

Mavunde alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akizungumza na wananchi wa kijiji cha Lyamidati mkoani Shinyanga wakati Kamati ya Mawaziri Wanane wa Wizara za Kisekta wanaoshughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi ya vijiji 975 walipofika eneo hilo.

“Nitoe rai yale maeneo ambayo migogoro yake ya matumizi ya ardhi imetatuliwa basi iwekewe matumizi bora ya ardhi ili mashamba makubwa yasisahaulike na wakulima wapate maeneo ya kutosha walime na hatimaye waisaidie nchi kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja, kaya na taifa kwa ujumla,” alisema.

Badala ya maeneo ambayo utatuzi wake umefanyika kutengwa kwa ajili ya makazi peke yake, ni lazima wataalamu wasimamie mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa kuhakikisha wanaingiza maeneo makubwa ya mashamba ya kilimo.

“Rais Samia Suluhu Hassan amekuja na mpango wa kuwa na mashamba makubwa ya pamoja (block farms) ili kusaidia kukuza sekta ya kilimo kufikia malengo yake ya kukua kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030,” alisema.

Kwa mujibu wa Mavunde, mashamba hayo makubwa ya pamoja yatasaidia kurahisisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima hasa katika mbinu bora za kilimo cha tija na usambazaji wa teknolojia mbalimbali za kilimo ili kusaidia kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo.

“Serikali ina mpango wa kuwa na mashamba makubwa ya pamoja 10,000 kufikia mwaka 2030 na kwa sasa hivi nchi nzima ina jumla ya mashamba makubwa ya pamoja zaidi ya 110,” alisisitiza.

Kamati ya Mawaziri Wanane wa Wizara za Kisekta iko katika ziara ya kutembelea mikoa mbalimbali kwa lengo la kutoa mrejesho wa Maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975.

Tayari katika awamu hii ya pili kamati hiyo imeshatembelea mikoa ya Rukwa, Katavi, Kigoma, Simiyu na Shinyanga.




Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde (katikati), akimsikiliza mmoja wa wananchi katika kijiji cha Lyamidati, mkoani Shinyanga, wakati kamati ya mawaziri nane wa kisekta wanaoshughulikia migogoro ya ardhi ya vijiji 975 walipofika katika eneo hilo, jana. **PICHA: WANMM**

# Mradi maji Mjimpya kukamilika karibuni

**Na Mwandishi Wetu**

MRADI wa Maji wa Mjimpya Kata ya Kawawa, Kibaha mkoani Pwani, unatarajia kukamilika Machi, mwakani na unatarajiwa kuwanufaisha zaidi ya wakazi 2,000.

Akizungumza juzi, Meneja Mkoa Kihuduma DAWASA Mlandizi, Mhandisi Damson Mponjoli, alisema mradi umegharimu Sh. bilioni moja na umehusisha uchimbaji na ulazaji wa mabomba.

“Mabomba yaliyolazwa ni yenye ukubwa wa inchi nane, sita na nne kwa umbali wa Km 26.3,” alisema.

Mhandisi Mponjoli alisema kukamilika kwa mradi huo kutamaliza changamoto ya ukosefu wa huduma ya maji kwa wananchi wa Kaloleni, Makazi Mapya, Ngeta, Janga, Mitimirefu, Mwembe Baraza na Msongola.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Makazi Mapya, Shabani Mwakatogo, alisema kwa miaka mingi wananchi wa Mjimpya wamekuwa wakitumia maji ya chumvi na waliyapata kwa tabu kutoka kwa watu binafsi waliochimba visima.

“Tunaishukuru serikali kupitia DAWASA kwa kushughulikia changamoto ya huduma ya maji na sasa wananchi wamepata matumaini makubwa ya huduma hii,” alisema Mwakatogo.

“Tunakiri kuwa serikali ya awamu ya sita inatusikiliza, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan anao watendaji wanaomsaidia kutatua changamoto ya huduma DAWASA wamesikia kilio chetu na sasa mradi unatekelezwa kwa nguvu zote,” aliongeza.

Mradi wa maji wa Makazi Mapya Mjimpya unatekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa gharama zaidi ya Sh. bilioni moja.

# Shirika lawaokoa wanafunzi kupata magonjwa ya mlipuko

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Nyanhembe, Kata ya Kilago Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, wameondokana na magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu, kuhara damu na kuumwa matumbo baada ya kujengewa vyoo vya kisasa na Shirika lisilo la kiserikali la World Vision Tanzania.

Aidha, shule hiyo inajumla ya wanafunzi 570 kati ya hao wanafunzi wa kike 301 na wakiume 269, awali matundu ya vyoo yaliyokuwa yakitumika ni nane hali ambayo ilifanya baadhi ya wanafunzi kujisaidia vichakani.

Adha hiyo imetatuliwa kwa shule kujengewa matundu nane ya vyoo kati ya hayo manne ya wanafunzi wa kiume na manne pia ya wanafunzi wa kike wakiwa na miundombinu kwa wanafunzi wenye ulemavu na chumba maalumu cha kubadilishia taulo za kike vikiwa na thamani ya Sh. milioni 39.3.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Mwalimu Clement Nelson aliyabainisha hayo jana wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi ya maji, elimu na afya iliyotekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la World Vision Tanzania katika kata za Iyenye na Kilago kwa kushirikisha viongozi wa Manispaa, watumishi wa shirika hilo na watendaji wa vijiji na kata.

Alisema wanafunzi walikuwa wakiugua matumbo mara kwa mara na kulazimika kuomba ruhusa na kwenda nyumbani kujitibia hali ambayo ilikuwa inawafanya kukosa masomo yao darasani hususani watoto wa wakike na wale wanafunzi wenye umri mkubwa hawakuweza kutumika vyoo kwa kuona aibu.

Nelson alisema, kwa sasa hali hiyo imetoweka baada ya kupata msaada wa vyoo vya kisasa vikiwa na sehemu ya kubadilisha taulo za kike na wanafunzi hawapati tena ugonjwa wa kuumwa tumbo na wanahudhuria masomo yao na wanatarajia kufanya vema katika mitihani yao ya mwisho.

Awali akitoa taarifa ya ujenzi wa vyoo hivyo, Mratibu wa mradi wa Iyenze-Kilago kutoka World Vision Tanzania, Domick Mbamba, alisema wamejenga matundu nane ya vyoo katika shule hiyo kwa ajili ya wanafunzi wa kike na kiume yakiwa na chumba maalumu ya kubadilishia taulo za kike vikiwa vimegharimu Sh. milioni 39.3.

Alisema vyoo vya namna hiyo pia wamejenga katika shule nane za msingi katika Kata ya Iyenze na Kilango, shule hizo ni pamoja na Kawe, Wame, Ilungu, Gilime, Iyenye, Tulole pamoja na Shule ya Msingi Isalenge vikiwa na mifumo ya huduma ya maji.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi Agnes Mabula alisema vyoo vilivyokuwapo vilikuwa havitosherezi mahitaji na walikuwa wakijisaidia kwa awamu hali ambayo yaliibuka magonjwa ya mlipuka na kusababisha kukosa masomo ila sasa hali hiyo imetoweka baada ya kupata vyoo vya kisasa na maji.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Robert Kwela, alipongeza shirika hilo kwa kutekeleza miradi hiyo kama vipaumbele vya wananchi na kuwataka wananchi kata hizo kuhakikisha wanakarabati vyumba vya madarasa chakavu, ili wanafunzi wapate mazingira mazuri ya kujisomea.



Naibu Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Joseph Rwegasira (wa tatu kulia), akikata utepe kuzindua kitabu kilichoandaliwa kwa ajili ya kuwajengea watoto uelewa na uwezo wa kujieleza na kupinga ukatili dhidi ya watoto, wakati wa hafla ya kuwaaga wanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Kilimani, mkoani Dar es Salaam. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Watakiwa kufuatilia nyendo watoto wao

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imewataka walimu na wazazi kuwa karibu na watoto na kufuatilia nyendo zao ili kupinga unyanyasaji dhidi yao, huku ikiwataka walimu na wamiliki wa shule kuanzisha majukwaa huru yatakayosaidia kuwajengea uelewa, ujasiri wa kujieleza na kujitambua.

Wito huo ulitolewa juzi mkoani Dar es Salaam na Naibu Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Joseph Rwegasira, wakati akihutubia hafla ya kuwaaga wanafunzi wanaomaliza darasa la saba katika Shule ya Msingi Kilimani.

Alisema katika utafiti walioufanya kwa watoto wachache walifanikiwa kubaini mambo yanayosikitisha ambayo walidai kuwa yanafanyika mazingira ya shuleni, ambapo alitoa wito kwa wazazi kuwalea watoto vizuri na kutambua mienendo yao, ili miaka ijayo wawe na watoto imara na wenye faida na tija kwa taifa.

"Ili vijana hawa wawe bora na wazuri katika taifa letu wanahitaji malezi bora, na malezi bora yanaanzia nyumbani na shuleni kwa sababu ndiyo sehemu ambazo wanakuwapo kwa muda mwingi, unaweza kukuta mwalimu anaijua tabia ya mtoto vizuri kuliko mzazi," alisema na kuongeza:

"Serikali inawahimiza walimu pamoja na wamiliki wa shule wahakikishe kwamba vijana wetu wanapata malezi bora katika mazingira yao ya shule, juzi Wizara ya Maendeleo ya Jamii ilizindua kampeni ya kupiga vita unyanyasaji wa kijinsia na ukatili kwa watoto," alisema Rwegasira.

Aliongeza kuwa kuna tafiti nyingi zimefanyika zinaonyesha kwamba ukatili mwingi kwa watoto unafanyika katika sehemu za shule na kwenye ngazi ya familia, hivyo alisisitiza walimu na walezi kuwafanya watoto hao marafiki ili waweze kuweleza yale yanayowasibu.

Aidha, alieleza kuwa suala la unyanyasaji kwa watoto na ukatili wa kijinsia serikali inaliangalia kwa jicho la tatu, huku akitoa rai kwa uongozi wa shule kuweka utaratibu wa kuwa na makongamano ya kuwawezesha watoto kujielezea ili waweze kujitambua wao ni nani.

"Tunawashukuru sana Kilimani wakiwa kama wadau wetu na serikali tunaahidi kutoa ushirikiano wa aina yoyote na kuhakikisha wao pamoja na taifa kwa ujumla tunafikia malengo yetu ya kupata vijana imara na watakaolisaidia taifa letu kupiga hatua," alisema Rwegasira.

Mwalimu Mkuu Msaidizi katika Shule ya Msingi ya Kilimani, Neema Charles, alisema shule hiyo inakuza vipaji vya wanafunzi ili waweze kujiajiri baadaye.

"Sisi Kilimani tunawalea watoto kuanzia miaka miwili, tunawaona na vipaji vyao tangia wakiwa wadogo tunavigundua mapema, hivyo tunaviendeleza tukiwa na imani kubwa kwamba mbeleni vitakuja kuwasaidia," alisema Neema.

# Balozi Mlima aeleza manufaa ushirikiano Tanzania, Uganda

**Na Maulid Mmbaga**

BALOZI wa Tanzania nchini Uganda, Dk. Aziz Mlima, amesema ushirikiano wa nchi hizo umesaidia ukuaji wa nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki kwa njia ya mtandao, alisema kuna majukwaa mawili ambayo ni tume ya ushirikiano wa pamoja kati ya nchi hizo mbili ambayo hutatua matatizo mbalimbali ya kisiasa, uchumi, ulinzi na usalama na vikwazo visivyo vya kiforodha.

Jingine ni la biashara lililoanzishwa mwaka mwaka 2019, kwa dhumuni la kuwaleta pamoja wafanyabiashara wa Tanzania na Uganda kushirikiana na kujadiliana maoni mbalimbali, vikwazo na matatizo yanajitokeza katika biashara na kuyapatia ufumbuzi.

"Kupitia majukwaa hayo tumeweza kutatua na kuimarisha ushirikiano wetu, kukuza fursa za kiuchumi, biashara na ujirani mwema katika nchi zetu mbili, pia kwa miaka mitatu iliyopita kati ya Tanzania na Uganda kumekuwa wa ongezeko la ukuwaji wa biashara," alisema na kuongeza:

"Bidhaa tunazouziana kati ya nchi zote mbili karibu zinafanana, ikiwamo madini ya chuma, ya dhahabu, mafuta za plastiki na samaki, lakini kubwa ni biashara ya mchele ambayo inathamani kubwa kwa watu wa Uganda, hii ni fursa nzuri kwa Watanzania kwasababu unapokuja hapa unapendwa."

Aliongeza kuwa Tanzania na Uganda wanashirikiana pia katika miradi mikubwa ikiwamo bomba la mafuta ghafi lenye urefu wa kilamita 1442 na kwamba kwa zaidi ya asilimia 80 litapita nchini, huku akieleza kuwa fursa kubwa ya mradi huo iko nchini.

Aidha, alikanusha taarifa zilizotolewa na wabunge wa Umoja wa Ulaya kupinga mradi huo kwamba haukuzingatia utunzaji wa mazingira na wananchi hawakulipwa fidia.

Alisema wabunge hao hawakuwa na taarifa za kutosha juu ya mradi wa bomba hilo la mafuta ghafi, na kwamba walikuwa na ajenda tofauti ya kutaka kuwachelewesha, huku akieleza kuwa wote walioguswa na mradi wamepatiwa stahiki zao, na maeneo ya hifadhi za wanyama ziko salama.

Balozi Mlima alisema ushirikiano mwingine baina ya nchi hizo ni reli ambayo itatumika kusafirisha mizigo mbalimbali, na kwamba kutaisaidia kukuza Bandari ya Dar es Salaam.

Pia alisema reli ya kati na SGR utatoa uhakika wa usafirishaji wa mizigo ya biashara.

Aidha, alisema serikali iko katika mazungumzo ya kuwa na mradi wa bomba la gesi litakalotoka Mtwara kwenda Uganda ambao utanufaisha nchi hizo kiuchumi.

Ushirikiano mwingine ni uzalishaji na ufuaji wa umeme wa megawati 14, akieleza kuwa makubaliano yao kati ya hizo saba zitakuwa za Tanzania na zingine za Uganda.

HABARI KASKAZINI

# Wakulima wafurahia 'bima pima' kukabiliana ukame

**Na Cynthia Mwilolezi,** HAI

WAKULIMA wa mahindi wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, wamemweleza Malkia wa Uholanzi, Maxima kuwa bima ya mazao ya bima pima inayotolewa na Taasisi ya Kutengeneza Bima ya Mazao na Mifugo (ACRE Afrika), imewasaidia kukabiliana na athari zinazotokana na majanga ya ukame.

Aidha, wameeleza mfumo wa 'bima pima' umewaunganisha na kampuni ya mbegu ya SeedCo ambayo imewawezesha kuongeza uzalishaji kutoka gunia nne hadi tano kwa ekari moja mpaka wastani wa kati ya gunia 25 na 40 kwa eneo hilo.

Wakulima hao waliyasema hayo jana wakati Malkia Maxima alipokuwa akitembelea maonyesho yaliyoandaliwa kwenye chama cha msingi cha ushirika cha Uduru Makoa kilichoko kata ya Machame Kaskazini wilayani humo.

Walisema kabla ya ACRE Afrika kuanza kutekeleza mradi wa kutoa bima ya kilimo na kuwaunganisha na kampuni hiyo ya mbegu, walikuwa wakitumia debe moja kupanda ekari moja ya shamba ambayo mavuno yake yalikuwa hafifu.

**Nimewahi kupata malipo ya bima ya Sh. 120,000, mimi nimeona faida ya huu mradi kwa sababu hizo fedha nilitumiwa kwenye simu yangu wakati wa maandalizi ya msimu mwingine wa kilimo.**

"Kwa sasa tunapanda mifuko minne ya mbegu ya mahindi ya kilo moja moja kutoka kampuni ya SeedCo, kama mvua ziko za kutosha na ukifuata kanuni bora za kilimo unaweza kuvuna mpaka gunia 40 kwenye ekari moja.

Lakini kukiwa na majanga unaweza kupata walau gunia 25 kwenye ekari moja," alisema mmoja wa wakulima hao wakati akitoa maelezo kwa Malkia Maxima.

Kwa upande wake, Malkia Maxima alieleza kuridhishwa na namna mfumo huo wa bima ya kidigitali ya 'bima pima' ulivyowawezesha wakulima kupata fidia ya mazao kutokana na janga la ukame.

Kwenye majadiliano hayo, Mkulima mhamasishaji, Cleopa Mushi, ambaye ameajiriwa na kampuni ya ACRE Afrika kwa ajili ya kuhamasisha wakulima kununua vocha (bima) ili kukabiliana na majanga ya ukame na uhaba wa mvua alisema msimu ujao yeye na wakulima wenzake wamejipanga kununua vocha nyingi zaidi kwa kuwa wameona mafanikio yake.

"Nimewahi kupata malipo ya bima ya Sh. 120,000, mimi nimeona faida ya huu mradi kwa sababu hizo fedha nilitumiwa kwenye simu yangu wakati wa maandalizi ya msimu mwingine wa kilimo.

Irene Ndenshao alisema alinunua vocha moja ambayo inauzwa Sh. 1000 kwa hofu kuwa huenda anaweza kutapeliwa na baada ya msimu kuisha mavuno hayakuwa mazuri.

Akimkaribisha Malkia kuzungumza na wakulima hao, Mkurugenzi wa Kampuni ya Acre Afrika, nchini Tanzania, Chrisopher Mazali, alisema kuwa wanatekeleza mpango wa kutengeneza bima hiyo ya kidigitali hapa nchini kuanzia mwaka 2015 ambapo wameanza na mikoa ya kilimanjaro na Arusha.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Mbegu ya SeedCo, Kanda ya Afrika Mashariki, Clive Mugadza, alisema wamejikita kuzalisha mbegu zinazohimili changamoto za tabianchi na kuwawezesha wakulima kupata mavuno mengi na bora.

Meneja wa CRDB Kanda ya Kaskazini, Chiku Issa, alisema benki yao inaongoza kwa kutoa mikopo ya kilimo nchini kwa kutoa asilimia 43 ya mikopo yote iliyotolewa.

Alisema hiyo inatokana na benki hiyo kuwajali wananchi kwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania ni wakulima na inaunga mkono juhudi za serikali kuwainua wananchi kiuchumi kupitia mikopo hiyo ya kilimo.

## RC Mongela awataka kuchangamkia fursa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa Arusha, John Mongela, amewaita wajasiriamali wilaya za pembezoni kuchangamkia fursa za uboreshaji wa bidhaa zao na kuinua uchumi wa familia na nchi kwa ujumla, baada ya kukutana na wataalamu wa viwanda vidogo, kati na vikubwa.

Wajasiriamali hao watanufaika na fursa hiyo, wakati wa maonyesho ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Kanda ya Kaskazini, yanayotarajiwa kuanza Oktoba 19 hadi 25 mwaka huu katika Viwanja vya Kumbukumbu ya Azimio la Arusha.

Alisema maonyesho hayo ni fursa kwa wajasiriamali, sababu watakutana na wataalamu wa viwanda vidogo, kati na vikubwa.

"Sekta hii ya viwanda vidogo inatoa ajira nyingi rasmi, kuliko nyingine na ndilo eneo linaloweza kutoa ajira kwa vijana, wanawake," alisema.

Mongela, alisema katika maonyesho hayo, wanatarajia kuwa na washiriki zaidi ya 200 na wazoefu wa uanzishaji wa viwanda vidogo, kati na vikubwa pamoja na taasisi za kifedha na benki, ambao watatoa elimu kwa wanaotaka kuingia kwenye ujasiriamali.

Alisema uchumi wa nchi nyingi zinazoendelea na zilizoendelea zinategemea viwanda na hiyo ni fursa kwa vijana kujikuta kwenye sekta hiyo ili kujiajiri na kujipatia kipato.

Kwa mujibu wa Mongela, bidhaa zitakazoonyeshwa ni za usindikaji wa vyakula, ngozi, sabuni na nyingine.

Meneja wa SIDO Mkoa wa Arusha, Jalphary Donge, alisema maonyesho hayo yatafunguliwa na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe na kaulimbiu ya mwaka huu ni "Pamoja tujenge viwanda kwa uchumi na ajira endelevu".

**Sekta hii ya viwanda vidogo inatoa ajira nyingi rasmi, kuliko nyingine na ndilo eneo linaloweza kutoa ajira kwa vijana, wanawake.**



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Foundation for Civil Society (FCS), Francis Kiwanga (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu Wiki ya Asasi za Kiraia itakayofanyika mkoani Arusha kuanzia Oktoba 24-28 mwaka huu. Kushoto ni Mkurugenzi Mkazi Norwegian Church Aid Actalliace (NCA), Berte Ulveseter na Mkuu wa Kitengo cha Sekta ya Umma cha Benki ya Stanbic, Doreen Dominic. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waonya matumizi vyakula vyenye viambata sumu

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WATAALAMU wa lishe katika Mkoa wa Arusha, wameonya kuhusu matumizi makubwa ya vyakula sokoni, ambavyo havikidhi ubora na kuzalishwa vikiwa na viambata vya sumu kuvu.

Wameshauri wakulima na wafanyabiashara wa bidhaa lishe, kufanya uzalishaji wa vyakula bora wenye lishe bora na vinavyokidhi afya ya mwananchi baada ya uzalishaji.

Ofisa Lishe wa mkoa huo, Rose Mauya, akizungumza na wadau mbalimbali wakati wa maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani, alisema iko haja kwa wakulima wa Tanzania kwa sasa, kujali zaidi ulaji wa mwananchi.

"Fanyeni uzalishaji unaotosheleza pamoja na wenye kuleta chakula ambacho kina lishe na virutubisho. Hivi sasa kumekuwa na uhaba wa chakula kwa kuwa chakula kingi kinachozalishwa kimeelekezwa kwenye masoko tu," alisema.

"Tunajua kwamba siku zinavyozidi kwenda tunaongezeka, watoto wanakua na wengine wapo shuleni. Ni vyema wakulima wanapozalisha wakumbuke kurudi kwenye jadi zetu za kuzalisha vyakula kwa ajili ya biashara pamoja na vyakula vya familia zetu.

"Tunaona kuna wimbi kubwa sasa, watoto wanapata shida katika lishe. Tujiulize wanapata shida kwa nini? Ni aina ya vyakula tunavyovizalisha? Je, ni utumiaji au matumizi sahihi ya vyakula hayafatwi?"

Mkoa wa Arusha kwa sasa uko na wastani wa asilimia 25 ya hali ya lishe, licha ya kuendelea kuimarika kutokana na tatizo kubwa la udumavu lililokuwa linasumbua.

Katika maadhimisho hayo, Meneja wa Kanda ya Kati wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Voda's Mwanakatwe, alisema walianzishwa na serikali kuhakikisha kuna utoshelevu wa chakula, pamoja na kuhakikisha sekta ya kilimo inakua kutoka kwenye kilimo cha kujikimu kwenda kwenye cha biashara.

Alisema malengo ya kuanzishwa yakiwa ni kuhakikisha uzalishaji unaongezeka na unakuwa na tija pamoja na kuhakikisha kwamba kunakuwa na upungufu wa upotevu wa mazao baada ya mavuno, ripoti zinaonyesha chakula kinapotea kati ya asilimia 10 hadi 30.

"Moja ya maeneo ambayo tunahakikisha yanakuwa na tija ni kwenye uhifadhi wa chakula, pamoja na hilo pia tumekuwa tunahakikisha kwamba tunawekeza zaidi kwenye kuongeza thamani kwenye mazao," alisema Mwanakatwe.

# Afariki dunia kwa kunywa pombe kupita kiasi

Na Steve William, LUSHOTO

MKAZI wa Bumbuli wilayani Lushoto, mkoani Tanga, Zahoro Athumani (40), amefariki dunia baada ya kunywa pombe kupita kiasi.

Kamanda wa Polisi mkoani Tanga, Henry Mwaibambe, alisema tukio hilo lilitokea katika Kijiji cha Mgome, wilayani Muheza alikokuwa akifanya kazi ya kibarua cha kuchunga mbuzi.

Alisema mchungaji huyo wa mifugo alifariki dunia usiku baada ya mtoto mwenye baa aliyokuwa anakunywa Athumani, kumkuta akiwa amelala wakati akienda shuleni.

**Hili linatokana na kuwapo kwa baadhi wanafunzi wenye maadili mabaya, ambayo yanaweza kuleta madhara kwa wanafunzi wengine.**

Alisema alipomwamsha bila mafanikio, alimwita baba yake na kuomba msaada kwa majirani.

Alisema mmoja wa majirani zake, Samwel Semgalawe, alimtambua marehemu na walitoa taarifa kwa Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mgome, Rashidi Baki, ambaye aliandika barua ya kwenda kutoa ripoti polisi.

Daktari Frank Gratian, kutoka Hospitali Teule Muheza alipouchunguza mwili wa marehemu, aligundua kuwa alikunywa pombe nyingi bila kula chakula na kusababisha kutapika na hatimaye kukosa pumzi na kukutwa na umauti.

Kaimu Mkuu wa Upelelezi wa Polisi Wilaya ya Muheza, Teodori Njawa, aliyefika eneo la tukio, alisema mtu huyo alikunywa pombe kupita kiasi.

Mkuu wa upelelezi wilaya ya Muheza na Kaimu OCD Charles Ntenga, aliwaagiza viongozi wa vijiji kuweka mfumo wa ulinzi shirikishi ili wanapomuona mtu ameingia kijijini haeleweki watoe taarifa polisi.

Aliwaonya wananchi wanapomkamata mtuhumiwa wasichukue sheria mkononi badala yake wampeleke kituo cha polisi ili abanwe na kutaja mtandao wa wenzake.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu (kushoto), akikabidhi mkataba wa lishe kwa Mkuu wa Wilaya ya Same, Edward Mpogolo, katika hafla ya utiaji saini mkoani humo jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Anastacia Tutuba. **PICHA: MARY MOSHA**

## Wapendekeza kundi la wanaume kuingizwa mikopo ya uwezeshaji

Na Anjela Mhando, HAI

JUMUIYA ya Maridhiano ya Mkoa wa Kilimanjaro, imeishauri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kupendekeza na kupeleka bungeni, mabadiliko ya sheria ya mikopo ya uwezeshaji kiuchumi makundi maalum ili kuongeza kundi la wanaume ambalo limeachwa.

Katika sheria ya sasa, makundi maalum yanayonufaika na mikopo ya asilimia 10 isiyo na riba inayotolewa na halmashauri za wilaya, miji, manispaa na majiji ni wanawake, vijana na jamii ya watu wenye ulemavu.

Hoja hiyo ilielekezwa jana TAMISEMI na Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Salma Kabwa, wakati wa kikao kazi chake.

"Wanaume kukosa mikopo hii, kumesababisha washindwe kupiga hatua za kimaendeleo kwenye familia zao, jambo ambalo limefanya wadharauliwe na familia zao na hata jamii," alisema.

Mwenyekiti wa Jumuhiya hiyo mkoani Kilimanjaro, Jonnes Mola, alisema maridhiano Tanzania ni Shirika linalofanya kazi kushirikiana na serikali, wanasiasa na viongozi wa dini, kazi yao ni kutoa upatanishi ambao unaweza kuleta umoja wa dini, kijamii na kiuchumi.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Juma Irando, alisema atashirikiana na jumuiya hiyo kwa lengo la kuleta maendeleo ndani ya wilaya hiyo.

**Wanaume kukosa mikopo hii, kumesababisha washindwe kupiga hatua za kimaendeleo kwenye familia zao, jambo ambalo limefanya wadharauliwe na familia zao.**

# Wananchi wachoshwa uuzaji dawa za kulevya mitaani

Na Mary Mosha, HAI

BAADHI ya wananchi wa Kijiji cha Uraa, Kata ya Masama Uroki, wamechoshwa na vitendo vya uuzaji gongo, mirungi na bangi, huku wakiwatuhumu viongozi wa vijiji na kata kufumbia macho biashara hiyo.

Viongozi hao wanatuhumiwa kupokea fedha ili kutowabughudhi na kutowachukulia hatua watuhumiwa hao.

Wananchi hao walifichua siri hiyo jana, baada ya kukutana na wanahabari kuelezea kero hiyo.

Harrison Nnko, alisema kumekuwapo na matukio yanayofanyika hadharani licha ya kuwa ni kinyume na sheria na taratibu za nchi.

"Tunaomba serikali ya mkoa kuangalia namna ya kutatua tatizo hili kwa sasa limekuwa sugu katika kijiji chetu, matukio ya uhalifu yanazidi kushika kasi, tunapowashika watuhumiwa na kuwapeleka kituo cha polisi Bomangombe kabla haujafika nyumbani wameachiwa.

"Hii inatukatisha tamaa, watoto wetu wanaangamia, inasemekana kila kiongozi ana mgao wake, tunaomba serikali ichukue hatua kwanza kutuondolea hawa viongozi kwa kuwachukulia hatua na baada ya hapo kufanya operesheni ya siri na ya wazi kuhakikisha tatizo hili linatokomezwa," alisema Edna Muro.

Alipoulizwa kuhusu tuhuma hizo, Mwenyekiti wa Kijiji Uraa, Hashimu Swai, alikiri kuwapo kwa matukio hayo katika kijiji chake.

"Wapo wengi na wanafanyabiashara hizo, lakini tunapowakamata na kuwapeleka vituo vya polisi kabla haujafika nyumbani, wameachiwa na wanakuja kukufanyia fujo, tumechoka na tumekata tamaa na ili kuokoa maisha yetu tunanyamaza tuu," alisema.

Aidha, akizungumzia madai hayo, Mkuu Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema kwa sasa matatizo katika vijiji yanaongezeka na inaonekana baadhi ya viongozi wa ngazi hizo hawawajibiki ipasavyo.

"Nimepokea taarifa katika Wilaya ya Hai, Kijiji cha Uraa kuna maeneo, mirungi, bangi na gongo zinauzwa hadharani na wapo viongozi wa vijiji na vitongoji wanatuhumiwa kushirikiana na hao vijana.

"Nimewaagiza wakuu wa wilaya wote pamoja na Jeshi la Polisi, wafanye operesheni maalamu kuwakamata na kuwachukulia hatua watu wote wanaofanya hiyo biashara pamoja wanaoshirikiana nao.

"Haiwezekani watu hawa wanafanya biashara hiyo na viongozi katika maeneo hayo wapo na wanatizama. Kila mmoja anajua madhara ya dawa za kulevya, hatutamvumilia kiongozi atakayeendelea kutajwa juu ya mambo haya."

ama
AFYA NA MAZINGIRA
ALHAMISI OKTOBA 20, 2022



**Bingwa tiba mapafu anyambua moshi kuni, mchikichi zinavyoua kimyakimya**

Ukurasa 14



**Unaujua ugonjwa Usonji, uhusiano wake na afya akili kwa mtoto?**

Ukurasa 16

# Dawa mwarobaini ilivyo tiba bora ya nywele, usalama afya

**Na Dk. Mussa Zaganzi**

INAJULIKANA mwarobaini ni dawa nzuri ya asili, ikiwa na faida kadhaa kiafya. Eneo mojawapo inatajwa ni katika kutunza nywele za mtu.

Ni nyenzo inayokabili bakteria, ikiwa na sifa ya kitabibu 'anti-bakteria', hata ikasababisha kwenda moja kwenye wadudu walipo na kupambana nao vyema, magonjwa nyemelezi ya kichwa, vilevile vidonda na kuwashwa.

Mwarobaini unachangia kuondoa athari (infections) mbalimbali kwenye kichwa, kama zilikuwepo, pia inalinda ngozi ya kichwa isipate athari, hata kama bado haijafikwa na madhara hayo.

Tiba hiyo inachangia nywele kukua kirahisi na kwa haraka zaidi, hata kama nywele hizo awali hazikuwa zinaongezeka na hata kama hazikui vizuri, kitaalamu inashauriwa mtu kutumia muarobaini kila mara, daima matokeo yatashuhudiwa ya nyewele kukua.

Mtu anaweza kupaka kwenye sehemu ya juu pekee au kwenye nywele zote, ikiwa na viini vya kutosha kunakishi nywele za mtu vyema.

Katika uhalisia wake, mwarobaini una harufu kali kidogo, hivyo kulingana na jinsi mtu anaweza kuchagua namna ya kuitumia.

**NAMNA YA TIBA**

Mba au kitaalamu 'Dandruff'' ni tatizo la kawaida la nywele na linaweza kuendelea kujirudia. Lakini, muhimu ni kwa mwarobaini unaweza kusaidia mengi. Dhana potofu ni kwamba, mba husababishwa na ukosefu wa usafi na inaweza kusababisha aibu ya kijamii kwa wengi.

Ingawa matibabu mengi ya mba yanapatikana, njia mbadala ya asili yanaweza kuwa bidhaa za mwarobaini, bado unajulikana kupambana na mba kwa kuwa una sifa kuu za antimicrobial.

Mara nyingi, hutumiwa katika tiba nyingi za nyumbani kuondoa mba inayosumbua na kukuza afya ya ngozi (scalp) ya kichwa na nywele.

Mwarobaini na bidhaa zake, zimetumika sana katika dawa za kale. Mmea huo ni nguvu ya kuzuia uchochezi unaoweza kusaidia kutibu mba.

Katika sehemu mbalimbali za mmea huo ni pamoja na gome lake, zimejaa viambato vya kuzuia ukungu vinavyoweza kuzuia mba kujirudia na kuweka kichwa cha mtu kikiwa safi na chenye lishe.



Sehemu ya maji ya mwarobaini na nywele katika picha tofauti. **PICHA: MTANDAO.**

**KIPIMO KIKOJE?**

Mtumiaji anaambiwa anatakiwa apate malighafi ya majani ya mwarobaini yanayotosha viganja viwili na lita moja ya maji safi.

Baada ya hapo, maji hayo yachemshwe na kisha inaondolewa kutoka kwenye moto. Baada ya hapo, majani ya mwarobaini kwenye maji na mchanganyiko huo unaachwa ukae usiku kucha.

Asubuhi ikifika, mtu anatakiwa kuosha nywele zake vizuri na maji hayo. Matokeo yake ni kwamba itapunguza mara moja kuwashwa na usumbufu unaosababishwa na mba.

Dawa hiyo ikitumiwa mara mbili hadi tatu kwa wiki, ni tiba kamili kwa mtu kuondokana na tatizo kabisa katika nywele na ngozi yake.

Muhimu, ni kwa mtumiaji kujenga utamaduni wa kupata ushauri wa utunzaji nywele toka kwa wataalamu.

- ***Mwandishi mbaye ni mtaalamu bingwa wa ngozi, anapatikana kwa simu: +255 713039875.***

AFYA

# Bingwa tiba mapafu anyambua moshi kuni, mchikichi zinavyoua kimyakimya

**Na Beatrice Shayo**

UTUMIAJI kuni na mkaa, kimsingi ni nishati chafu, moshi wake unatajwa kuwa na sumu inayomsababisha mtu kuugua magonjwa ya mfumo wa hewa, kupata saratani ya koo na hata kufariki.

Takribani watu 33,000 hadi 45,000 hupoteza maisha kila mwaka nchini, kutokana na magonjwa yanayotokana na nishati chafu za kupika zinazotumiwa nyumbani, ikiwemo kuni na mkaa.

Asilimia 72 ya nishati inayozalishwa Tanzania, inatajwa kutumika majumbani. Pia, asilimia 63.5 ya kaya zote hutumia kuni kupika na asilimia 26.2 hutumia mkaa.

Vilevile, inaelezwa kuwa sehemu iliyobaki inajumuisha asilimia 5.1 ya kaya zinazotumia gesi za mitungi, huku asilimia tatu ni ya umeme; asilimia 2.2 ni ya nishati nyinginezo.

**NENO LA DAKTARI**

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Mapafu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Pauline Chale, anasema wamekuwa wakiwahudumia wagonjwa waliopata athari za matumizi ya kuni na mkaa.

Anasema, kuna wanaotumia kinyesi cha wanyama na mabaki ya mimea kupikia, mfano kwa watu wanaotoka mkoa wa Kigoma wanatumia mabaki ya mawese wanapochuja mafuta. Ni mabaki wanayotumia kuwashia moto na hata vifuu, hutumia kutoa moshi mkali.

Dk. Chale Pauline anasema, ni moshi wenye athari kubwa katika mazingira na kwa afya ya binadamu, akiufafanua: "Ule moshi unaotoka utauona kwa macho kama wa kawaida, kitaalamu unaingiza kemikali 200 ambazo ni hatari kwa afya."

Anasema, kuna chembe ndogo zenye uwezo wa kuingia katika mfumo wa kupumua na mtu anapovuta na moshi, unaingia moja kwa moja katika mapafu na kuna madhara kiafya.

Anasema, mwilini binadamu ana ulinzi wa kuzaliwa, ambao mtu anapokuwa anapumua, anakuwa na kinga katika mfumo wa hewa.

"Ukiangalia kuna watu wengine wana vinyweleo puani. Vile vina kazi maalumu katika ulinzi wa njia ya kupumua. Kazi yake ni kuzuia vumbi. Huwa inazunguka kama fagio kutoa vumbi nje," anasema.

Anasema sumu hiyo inapoingia, huenda moja kwa moja kuua ulinzi uliopo dhidi ya magonjwa ya mapafu, hivyo pale ulinzi huo unapokufa, inakuwa rahisi kwa mtu kupata maambukizi. Hapo anataja idadi ya vifo vya watu kutokana na hali hiyo nchini ni kati ya watu 30,000 hadi 45,000 kwa mwaka.

"Ukiangalia hili tatizo ulimwenguni watu wanakuwa na shida, mtu anaishi kwa muda mrefu na matatizo na haya magonjwa yapo katika vifungo tofauti. Kuna haya magonjwa ya papo kwa hapo na yale ambayo yanakaa kwa muda mrefu," anasema

Anarejea wagonjwa walio nayo, tatizo wanalikuta kwa wingi kwa kinamama, kwa kuwa wao hutumia muda mrefu kupika, hali kadhalika watoto wadogo walio katika umri chini ya miaka mitano.

Dk. Pauline anaeleza madhara yake ni kwamba, watu huanza kuwashwa macho, ikiwa ni matokeo ya sumu anayopata akiwa katika mazingira ya kutumia nishati isiyo salama.

"Utakuta mtu anawashwa jicho hadi linakuwa jekundu. Huko Kanda ya Ziwa, wakiona mtu yupo hivyo wanamuita mchawi, wakati amepata madhara kupitia moshi au utamsikia mama anasema 'sioni'.

"Hii ni kwa sababu ile sumu inafyonza katika jicho, inakwenda kuharibu ule ute wa lenzi, hivyo mtu anaanza kupoteza kuona na mwisho wa siku anapata shida katika kuona,"anaeleza.

Pia, katika hilo anafafanua kwamba, kwenye mfumo wa hewa pale ukishaharibu vinyweleo, mtu utapata magonjwa ya papo kwa hapo, ikiwamo kukohoa.

"Utaona mtu anakohoa usiku, lakini hatoi makohozi. Ni kwa sababu, njia ya hewa inawasha na wengine wanapata vidonda katika koo," anaeleza

Mtaalamu huyo anafafanua kwamba, wagonjwa wa aina hiyo wakiwashwa kooni na kueleza vinawakereketa na hiyo, inatokana madhara ya kutumia nishati isiyo salama kiafya.

"Ataanza kuona pumzi ni ndogo atasema sipati pumzi vizuri ni kwa sababu inavyoingia katika mapafu yetu inafyonza mapafu, mwisho wa siku mtu anapoteza uwezo wa kujikinga na kuanza kukohoa ama kudai anapata 'numonia' ya mara kwa mara. Unaweza kupima, usione mdudu yoyote anayesababisha," a nasema.

Pia, mtaalamu huyo anataja inawezekana na akashangaa amepata ugonjwa wa kifua kikuu, ingawa hakukaa karibu na mgonjwa wa kifua kikuu.

Hapo Daktari Pauline, analifafanua jambo hilo limesababishwa na vimelea vinavyopita moja kwa moja bila kuzuiwa na 'askari walinzi' katika mfumo wa hewa kwa ajili ya kuwakinga.

Aidha, anasema mbali na sumu aliyoieleza kwa jina kemikali 200, kuna nyingine inayoweza kumsababisha mtu akapata saratani kwa njia ya hewa, ikiwemo ya koo kupitia hewa, au hata saratani za mapafu kwa njia hiyo.

"Watu wanadhani mtu akipata saratani ya mapafu ni amevuta sigara. Hawa mama zetu hawajawahi kuvuta sigara wala kufanya kazi viwandani, lakini unashangaa yupo katika ;listi' ya kupata saratani ya mapafu," anaeleza

Katika hilo Dk. Pauline anaendelea: "Ama utakuta mtu anakohoa mwaka mzima, anashindwa kupumua. Hayo ni baadhi ya magonjwa hawa wagonjwa tunao katika hospitali yetu ya Muhimbili.

"Yupo mgonjwa ambaye alikuwa katika Chumba cha Wagonjwa Mahututi (ICU) kwa siku 16 na gharama zake kwa siku ni Sh. 500,000. Ukiwa katika hiyo wodi, huyu mgonjwa hawezi kupumua, anahitaji mashine ya oksijeni na bahati mbaya alifariki," anatamka.

Pia, anafafanua kwamba, pale walipofuatilia kilichojiri kwa mgonjwa huyo tangu mwaka 2019, wakagundua chanzo ni kutumia nishati isiyo safi, hata ikamsababishia madhara hayo.

Anamtaja mgonjwa mwingine kutoka Kigoma, naye ana historia ya kutumia nishati mbadala, mabaki ya mawese, kwamba amekuwa akikohoa katika kipindi cha miaka miwili.

Dk. Pauline anasema, ni hali iliyomsababishia kukatwa kimeo na amewajulisha, licha ya kufanya hivyo, bado amejikuta anaendelea kukohoa mara kwa mara.

"Kukata kimeo haikuwa ni njia mbadala ya kumaliza tatizo lake. Tulilifanyia kazi, tukabaini mchawi aliyemsababishia kukohoa ni huo moshi wa nishati mbadala ya mawese," anasema Dk. Chale.

Anakiri, ni tatizo ambalo wananchi katika upande wa kuwatibu, sehemu mojawapo ni gharama kubwa, mfano kwa mgonjwa

INAENDELEA UK. 15



Mazingira yanayochangia mtumiaji kudhurika kiafya na moshi.



Michikichi ambayo imevunwa, iko katika hatua ya kubangua mbegu na maganda yanayobaki huwa yanatumika, hasa katika mikoa inayotumia michikichi, ikiwemo kuwa kuni. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

AFYA

AFYA YA AKILI

# Daktari bingwa asimulia jinsi inavyojificha kwa watoto miaka 10 hadi vijana miaka 19

**Na Elizabeth Zaya**

DAKTARI Bingwa wa magonjwa ya afya ya akili kutoka katika kitengo cha magonjwa hayo, Wizara ya Afya, Dk. Erasmus Mndeme, anasema kwamba tatizo la afya ya akili humuathiri zaidi mtu anapokuwa kati ya umri wa miaka 10 hadi 19.

Anaeleza kwamba, endapo mtu akipita katika hatua hiyo, uwezekano wa kupatwa na tatizo la afya ya akili ni mdogo kama ilivyo katika umri huo mdogo.

"Magonjwa yote ya akili ambayo tunayaona kwenye utu uzima wakiwamo hao ambao tunawaona huko barabarani wamezidiwa kabisa, yanaanza kwenye umri wa miaka 10 hadi 19,"anasema Dk.Mndeme.

"Ukiruka hapo ukiwa salama, hatari ya kuugua inapungua, ingawaje hata wakubwa wanaweza kuwa na tatizo la afya ya akili ambalo linaanzia ukubwani," anasema na kuendelea:

"Lakini, uwezekano wa wao kuugua unapungua kadri mtu anavyokuwa mtu mzima. Watu wazima wana magonjwa ya kiutu uzima, lakini mengi ya akili yanaanzia utotoni."

Anasema, watoto wenye umri wa miaka 10 mpaka 19, katika watoto saba, mmoja kati yao anakuwa na matatizo yenye afya ya akili na dalili za mtoto na mtu mzima, hazitofautiani sana.

"Isipokuwa, inategemea na aina ya ugonjwa na kuna magonjwa ya akili ni ya watoto tu na yale ambayo ni ya watu wazima. Na ukiangalia kwenye dalili, kila aina ya ugonjwa wa akili una dalili zake,"anasema Dk.Mndeme.

**DALILI ZA MTOTO**

Anataja baadhi ya dalili za watoto mwenye tatizo la afya ya akili kuwa ni kujitenga na wenziwe. Hapo anaeleza zaidi: "Mtoto mwenye dalili ya tatizo la afya ya akili hawezi kucheza kama ambavyo wenzake wanafanya, hata kama wako karibu naye."




Sehemu ya maadhisho ya Wiki ya Afya ya Akili, mwaka jana.
**PICHA: MAKTABA.**

Dalili nyingine anasema, ni mtoto kuwa na utundu kupita kiasi, kupiga wenzake bila ya sababu yoyote au kufanya vitendo visivyo vya kawaida.

"Namna ya kujua kama mtoto utundu umezidi, mfano wanacheza na watoto wenziwe halafu anafanya uharibufu wa vitu kwa haraka kwa muda mfupi.

" Yaani anagusa hiki anaacha anashika hiki, anafinya mwenzie, anapanda kwenye meza, yaani kabla hujamaliza unachofanya yeye ameshafanya mambo mengi kwa wakati mmoja," anaeleza Dk. Mndeme.

**DALILI ZA WOTE**

Dk. Mndeme anaeleza kwamba, baadhi ya dalili za wenye tatizo la afya ya akili kwa ujumla wake, ni pamoja na kupata hisia mbaya zisizo za kawaida, akifafanua: "Dalili za ugonjwa wa akili nazo huwa tunaziweka kwenye makundi, na za kwanza ni zile za kihisia.

"Unaweza kusikia mtu anakuambia anasikia sauti ambazo watu wengine hawasikii, au anaweza asikuambie hivyo, lakini badala ya kuongea kawaida, anaongea mwenyewe akiwa anajibu sauti anazozisikia yeye."

Anataja dalili nyinginezo za mtu mwenye tatizo la afya ya akili, ni kuona vitu ambavyo wengine hawavioni, hapo Dk. Mdeme anaifafanua: "Unaweza kumgundua kwa tabia zake zisizo za kawaida na namna anavyozungumza. Wakati mwingine atakuambia anaona mtu nyuma ya mlango, ukiangalia wewe huoni kitu.

"Kwa mfano anaweza kuanza kukimbia kwamba anaona kitu wakati wewe huoni au akakuambia anahisi anafuatiliwa. Kwa hiyo ili kuitwa kwamba ni ugonjwa wa akili, ni lazima iwe ni dalili ambayo ina tabia fulani hivi."

"Kwa mfano, unakuta watu wengine wanalala, lakini wewe hauna usingizi kabisa na hata kunapokucha hulali na unaendelea na shughuli zako kama kawaida.

"Unakuta mtu labda hata mchana alikuwapo na hakuwa na kazi yoyote, lakini na usiku pia inapofika halali, anaanza kufanya kazi akiwa na nguvu vilevile, hiyo tunaweza kuiweka kwenye kundi za dalili za tatizo la afya ya akili," anasema Dk.Mndeme, pia, akitaja kushindwa kupata usingizi usiku nayo ni miongoni mwa dalili za ugonjwa wa akili.

**WAZIRI UMMY**

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema kumekuwapo tabia ya Watanzania kuogopa kuzungumza masuala yanayohusiana na tatizo la afya ya akili, kwa kuogopa kuchekwa, kuanza kuzungumza bila kificho.

"Binafsi kama waziri, nimeona tuvunje ukimya, tuzungumze bila kificho kama taifa kuhusu suala la afya ya akili na kwamba ipo changamoto hiyo miongoni mwetu hususani ni kutokana na maendeleo ya kisayansi na teknolojia katika jamii.

"Kuna uhusiano mkubwa na wa karibu kati ya afya ya akili na ukuaji wa uchumi katika ngazi ya mtu mmoja mmoja, familia, jamii na taifa kwa ujumla," anasema Ummy.

Pia, anasema yapo magonjwa ya akili yanayoathiri na kusababisha mabadiliko katika kufikiri, kuhisi, kutambua na kutenda na hivyo kuleta mabadiliko ya kitabia na mwenendo ulio tofauti au usioendana na jamii husika kiimani, kimila, desturi na nyanja nyingine kwenye jamii.

Pia, anasema ugonjwa wa akili huathiri ufanisi wa mtu husika na uhusiano wake na kuathiri jamii inayomzunguka na anasema Tanzania inakadiriwa kuwa na watu milioni saba, wenye magonjwa mbalimbali ya afya ya akili, ikiwamo yanayotokana na dawa za kulevya.

Anasema magonjwa ya akili yapo kwa wingi Tanzania ni pamoja na sonona na kihoro, akifafanua kwamba zaidi ya watu milioni 1.5 wanaishi ugonjwa wa sonona na wengi wao wakiwa ni wanawake.

Kwa mujibu wa Ummy, vinavyochangia katika ugonjwa wa sonona ni kutokusema changamoto zako kwa watu, na anachoainisha: "Kwa hiyo kuna haja ya kuanza kulikubali bila aibu wala kificho tatizo la afya ya akili katika nchi yetu, lakini kubwa zaidi nataka tujikite kwenye kukinga zaidi, kipi tunaweza kufanya kama jamii kuhakikisha huduma za kinga zinapatikana,"anasema Ummy.

"Hivi sasa kuna tabia kwenye jamii kwamba eti Hospitali ya Mirembe ni kwa machizi, hili siyo sahihi, nchi zilizoendelea unaweza kupata changamoto ya maisha.

"Labda umeachana na mume au mke wako, au umefiwa na mume na mke, ndugu, jamaa na marafiki, umepoteza ajira, kuna sehemu unaweza kwenda na ukapata ushauri na ukarudi katika afya yako ya akili ya kawaida,

"Tanzania ukienda kufanya hivyo, Mirembe unaonekana chizi, mwendawazimu na huna maana katika jamii, ni lazima tubadilishe hii hali, ni lazima tuwekeze kwenye afya ya akili,"

Kwa mujibu wa Ummy, Tanzania inakadiriwa kuwa na watu milioni saba wenye magonjwa mbalimbali ya afya ya akili ikiwamo yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya.

# Bingwa tiba mapafu anyambua moshi kuni, mchikichi zinavyoua kimyakimya

**INATOKA UK. 14**

kuna dawa inayouzwa kwa bei Sh, 80,000 na kwa mwezi anatakiwa atumie nne, kiasi ambacho mtu wa kipato cha chini hamudu gharama hizo.

"Kuna baadhi ya wagonjwa ambao hawawezi kukaa bila kutumia oksijeni. Inambidi awe nyumbani huku akitumia pumzi, kwa sababu mapafu hayawezi kutengeneza pumzi.

"Inambidi atumie 'silinda' ya oksijeni ambayo kwa siku awe na Sh. 16,000, kama atatumia viwili itambidi awe na Sh. 32,000. Ni magonjwa ambayo yana gharama," anasema

**KONGAMANO KUELIMISHA**

Kutokana na hali hiyo, Wizara ya Nishati imetangaza kuandaa kongamano la nishati safi ya kupika, kuchunguza vikwazo vinavyodumaza matumizi ya nishati ya kisasa za kupika.

Waziri wa Nishati, January Makamba, anasema kongamano hilo la siku mbili, litafanyika kuanzia Novemba Mosi, jijini Dar es Salaam, linalenga kupendekeza mikakati ya kufanikisha upatikanaji wa nishati safi za bei nafuu na endelevu nchini.

Makamba anasema, wao kama wizara wanaamini tatizo la namna ya kupika ni kubwa kuliko wanavyolijadili na kulichukulia hatua, anasema Sera ya Nishati ya Mwaka 2015, inayosimamiwa na wizara inatoa maelezo mahususi kwa Wizara ya Nishati.

Ni suala analoeleza linachukua hatua za kuwawezesha Watanzania kupata nishati safi na salama na kwa bei ambayo wanaimudu.

Anayaeleza ni maelekezo ya kisera kwao na kwa bahati mbaya hayajafanyiwa kazi, hivyo wameanza kuyafanyia kazi maelekezo hayo ya kisera kwa lengo la kuokoa afya za Watanzania katika kutumia nishati safi.

Pia anasema mkakati wao baada ya miaka 10, Watanzania zaidi ya asilimia 80, wawe katika matumizi ya nishati safi ya kupika na kuondokana na moshi ambao unawaletea madhara katika afya zao na gharama za matibabu.

AFYA

# Unaujua ugonjwa Usonji, uhusiano wake na afya akili kwa mtoto?

## • Tabibu bingwa: Hauna dawa, ila unatibika

**Na Jenifer Gilla**

KUMEKUWAPO dhana tofauti katika jamii kuhusu watoto wenye tatizo la usonji, baadhi wakiamini ni ugonjwa wa akili uliotokana na imani ya kishirikina na unaosababisha mkosi au laana ndani ya familia.

Zao la sintofahamu hiyo, Nipashe imesonga hadi kwa daktari bingwa wa watoto wenye tatizo la ubongo na mfumo wa fahamu kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dk. David Kombo, anayehudumia watoto wenye tatizo hilo kupata ufafanuzi wake.

Dk. Kombo anasema, usonji ni tatizo kwa ukuaji (neurodevelopmental disorder) analozaliwa nalo mtoto, linalochangia kupata ugumu katika namna ya lugha na kuwasiliana, kujitenga na kutojichanganya na wengine.

Ni tabia au vitendo vya kujirudia, kama vile kuruka, kukimbia, kutingisha kichwa au mikono, kuzunguka au kupanda kwenye vitu kila mara, katika hali ambayo sio ya kawaida.

Mtaalamu huyo anafafanua kwamba mtoto anazaliwa na hali hiyo na mara nyingi, hugundulika pale anapofikisha umri wa kuanzia miaka miwili na kuendelea, kwa sababu baadhi ya dalili zake zinajitokeza kwa watoto wengine kama sehemu ya ukuaji wao.

Daktari huyo anazitaja dalili za mwanzo za tatizo hilo, ni kwamba mtoto analia kupita kiasi, kutokuwa na hisia au kuwa na hisia zilizopitiliza, kiasi ambacho mtoto anagoma hata ama kuchanwa au kunyolewa nywele na kupigishwa mswaki.

Vilevile, sio ajabu kubainika hata mtoto anapoitwa, anakuwa mgumu kuitikia na anaishia kutikisa kichwa, kuchezesha mikono na kutokuwa na uwezo wa kuongea maneno ya mwanzo, kama watoto wengine.

"Kwa kawaida mtoto tangu anapokuwa mdogo kabisa anaposikia sauti huwa anageukia upande inapotokea na anaanza kujua jina lake mapema. "Sasa kwa mtoto mwenye usonji, wakati mwingine unaweza kumuita jina na asiitikie kama vile si yeye unayemwita. Mtoto mwingine anaweza kuanza kuongea maneno ya mwanzo halafu akaacha kabisa," anasema Dk. Kombo.

Mtaalamu huyo wa afya ya watoto, anataja dalili nyingine kuwa ni mtoto kutochanganyika na wenzake, anapenda kucheza peke yake.

Pia wakati mwingine haonyeshi kama anaelewa anachoambiwa au kumsikiliza mtu anayemwita au kumwambia jambo.



Mama Salma Kikwete, alipokuwa na baadhi ya watoto wenye usonji.

### NI TATIZO?

Daktari huyo bingwa, ana ufafanuzi kwamba suala la usonji ni tofauti na kasoro za kiakili, ila inakuwa na ujirani na shida ya akili, kwa kuwa ni hali inayomfanya mtoto kutokuwa na uwezo wa kujifunza vitu haraka, kwa sababu ya changamoto katika mawasiliano.

Pia, anamtetea mtoto mwenye usonji, bado ana uwezo wa kujifunza kwa ufasaha jambo kwa kiwango bora zaidi, huenda kuliko mtoto asiye na hali hiyo.

"Watoto wenye usonji wanaweza kuwa na kipaji fulani au kufanya vizuri kwenye baadhi ya mambo kama vile muziki, sayansi au hesabu au kuchora na kadhalika.

"Wengi wanakuwa na kumbukumbu nzuri sana, anaweza kujua vitu ingawa itachukua muda mrefu kujifunza jambo hilo," anafafanua.

Anasema kuwa watoto hao wanapopatiwa elimu, wana uwezo wa kujifunza na kufanya kazi katika taaluma mbalimbali, hata kushika nyadhifa kubwa serikalini kama walivyo watoto wengine.

### MATIBABU YAKE

Tabibu Dk. Kombo, anasema kuwa usonji huwa hauna dawa au sindano ili mtoto apone, kwa hiyo wanachofanya madaktari ni kumsaidia mtoto mwenye tatizo hilo, kuweza kuhimili changamoto alizo nazo, ili aweze kuishi na jamii inayomzunguka.

"Mtoto mwenye usonji anapoletwa hapa kama hana ugonjwa mwingine wa ziada, hatumpi dawa yoyote. Tunamwanzishia matibabu ya kumsaidia kujitegemea, kuboresha mawasiliano, kushirikiana na kuhimili baadhi ya tabia tofauti alizo nazo, ili aweze kuishi na kupata haki zake za msingi kama watoto wengine, ikiwamo elimu," anaeleza.

Dk. Kombo anasema changamoto wanayokumbana nayo katika matibabu ni baadhi ya wazazi kuchelewa kuwapeleka watoto hao hospitali kwa sababu mbalimbali.

Hapo inajumuisha kutogundua tatizo la watoto wao mapema, kutokukubaliana na hali na wengine huanzia kwa waganga wa kienyeji au kwenye maombi, wakiamini kuwa mtoto amerogwa.

"Wapo watoto wanaletwa hapa wakiwa na miaka mitano, sita wakati huo mtoto tabia zake zinakuwa zimeshajengeka vibaya, kiasi ambacho ni vigumu kumsaidia kwa urahisi na kuathiri matokeo ya matibabu anayopewa. Pia, huwa tunapata ambao wanawahi na tunawasaidia mapema," anasema Dk.Kombo

Dk. Kombo anasema, mtoto mwenye usonji anapochelewa kupelekwa hospitalini, anakosa matibabu yanayomsaidia kukabiliana na changamoto zake, hivyo inakuwa ngumu kuchangamana na jamii inayomzunguka.

"Kwa hiyo mtoto huyo asipofundishwa na kuweza kukabiliana na changamoto zake, hatoweza kuchangamana na jamii inayomzunguka.

"Kwa maana hiyo, atajikuta anashindwa kupata haki zake za msingi kama vile elimu, kuabudu na kadhalika. Kwa mfano, asipoweza kuwasiliana atasaidiwa vipi pale anapokuwa na hitaji" anasema.



Watoto wenye usonji, wakiwa katika mjumuiko unaowahusu.
**PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### UHAMASISHAJI

Dk. Kombo anasema, kitengo chao kinatoa elimu kwa jamii kupitia vyombo vya habari na vijarida kuhusu hali hiyo, pia wanashirikiana na vikundi vya wazazi wenye watoto hao kufanya uhamasishaji katika matukio mbalimbali, ikiwamo Siku ya Usonji Duniani, inayofanyika Aprili kila mwaka.

Katika hilo, Dk Kombo anasema, kwa sasa mwitikio wa wazazi kuwapeleka watoto wao kliniki ni mkubwa, ikilinganishwa na miaka ya nyuma, hali inayoashiria kuwa jamii ina uelewa kuhusu hali ilivyo.

"Suala hili ni kama vile watu walikuwa wamelifumbia macho. Wengi walifikiria labda ni watoto ambao wakorofi, labda wamedekezwa, wengi walikuwa hawajui hata baadhi ya wataalamu wakati mwingine inakuwa ngumu kugundua kama huyu mtoto ana shida hii. Kwa hiyo, huu uhamasishaji umesaidia sana," anasema.

Anaeleza kwamba, kwa wiki wanafanya kliniki mara mbili mpaka tatu na katika kila kliniki wanapokea watoto wawili hadi wanne wapya wanaoletwa, hali anayoieleza ishara ya mwamko kutoka kwa wazazi wameshaelewa uhalisia wa hali hiyo.

### KUTOKA KWA MZAZI

Latifa Iddy (27), ni mama wa mtoto mwenye maradhi ya usonji, anakiri kwamba alikuwa akiamini hali hiyo ni tatizo la akili, mpaka pale inapotokea alipojifungua mtoto wa aina hiyo.

"Nimeamini zipo njia nyingi za kujifunza jambo, pengine nisingekuwa na mtoto wa hali hii hadi leo ningekuwa naamini kuwa usonji ni tatizo la akili. Ninavyomuona mtoto huyu ni tofauti na nilivyokuwa ninadhani, ni mtoto mwenye upendo na akielewa kitu hatokisahau," anasema.

Hata hivyo, Latifa anasema kuwa bado jamii inahitaji kuelimishwa kuhusu hali hiyo kwa kuwa watoto hao wanapitia changamoto ya kutengwa na jamii, ikiamini kuwa wana tatizo la akili hivyo wanaweza kuwadhuru.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linataja kati ya watoto 44, mmoja anazaliwa na hali ya usonji duniani, huku watoto wawili wa kiume wakiwa katika hatari ya kupata tatizo hilo mara nne zaidi ya mtoto wa kike.

AFYA

## SIKU YA MTOTO WA KIKE

# Jicho laangaza kasoro kuanzia ngazi za kiafya, saikolojia hadi mjumuiko

**Na Yasmine Protace**

INAPOZUNGUMZIWA Siku ya Mtoto wa Kike, ambayo ilikuwa tarehe 11 mwezi huu, mtazamo wake ni kuwatambua watoto wa kike, uwezo wao , ikiwamo kuzifahamu haki zao.

Haki za watoto wa kike zinatajwa ni pamoja na kupatiwa elimu, huduma za afya na kulindwa dhidi ya ubaguzi. Hadi sasa, haki za watoto hao wa kike zinajumuisha kuepushwa na ndoa za lazima .

Mwakilishi Mkazi kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na Idadi ya Watu (UNFPA,) Mark Bryan Schreiner, anasema wasichana wana haki na mamlaka ya kuamua kuhusu hatma ya maisha yao, ikijumuisha afya, tendo la ndoa na uzazi.

Mark anasema, kampeni tajwa inayowahusu kwa jina 'Girls Take Over' inaratibiwa na asasi ya Plan International Tanzania' inayoangaza wakala na uwezo wa uongozi wa wasichana.

Anaongeza kwamba, kaulimbiu ya kitaifa ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike mwaka huu ni: "Wakati wetu ni sasa - haki zetu, mustakabali wetu", kwa Kiswahili.

Hapo anaendelea kwa ufafanuzi: "Mada hii inawahimiza wasichana kuchukua haki zao za kibinadamu na kujenga mustakabali, ambao wanaweza kujiendeleza kwa uwezo wao kamili."

Mark, pia anasisitiza haja ya dharura kutoka mashirika ya maendeleo, washirika na jumuiya zinahitaji kupanua haraka uwekezaji na fursa za kupanga programu kwa wasichana, ili kuhakikisha wanamudu kutekeleza ndoto na kuongezeka usalama hadi kwa watu wazima, pasipo kumuacha yeyote nyuma.

Lingine analolitaja, linagusa mipango ya kitaifa ya serikali nchini kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake, akisema inalenga kumaliza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ifikapo mwaka 2030, kwa Tanzania na Zanzibar.

Anasema UNFPA ikiwa ni sehemu ya kutekeleza juhudi za Umoja wa Mataifa - inaunga mkono serikali ndani ya mfumo wa mipango na ahadi za kitaifa na kimataifa.

Kwa mujibu wa Mwakilishi Mkazi huyo, hiyo inaendana na Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu kwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, kujitolea kutokomeza ukatili wa kijinsia na mila za ukeketaji na ndoa za utotoni, ifikapo mwaka 2030.

Mark anaongeza kuwa, takwimu za Utafiti wa Afya ya Demografia Tanzania (TDHS) ya mwaka 2015/16, inatoa uwiano wa mwanamke mmoja kati ya watatu nchini, wanaolewa kabla ya kutimiza umri miaka 18.

"Zaidi ya hayo, msichana mmoja kati ya wanne,ama amejifungua au ni mjamzito; na msichana mmoja kati ya 10 amefanyiwa ukeketaji, huku kukiwapo tofauti kubwa za kikanda na zaidi ya wasichana watano kati ya 10 katika baadhi ya mikoa," anasema.



**CHANGAMOTO ILIVYO**

Mark anasema kwamba katika mazungumzo yao na wasichana, inagundulika hawataki kulazimishwa kuolewa, kuzaa wakiwa bado watoto, vilevile kukeketwa.

Kiongozi huyo wa UNFPA, anaelimisha kwamba katika ujenzi wa mwelekeo wa siku zijazo, wana mtazamo kuwapo hali ya wasichana kuwa na uwezo kamili wa kujitambua na kufurahia haki zao, katika matarajio yanayoendana na changamoto nyingi njiani.

Anajumuisha magumu hayo kuwa ni umaskini, imani za kijamii zenye mizizi mirefu njiani, kwamba zimedumu kuwa yanayomnyima msichana haki ya uhuru wa kimwili. Vilevile anataja orodha hiyo ya vikwazo, inabebwa na sauti ndogo katika kufanya uamuzi, kutolewa fursa zisizo sawa kwa wasichana kupata elimu na afya, hali kadhalika huduma za afya ya ngono, uzazi, haki za jumla, fursa za maisha na ajira.

**DIRA NA MWELEKEO**

Mark anaeleza dira ilivyo kwamba, maendeleo ya jumla huwa yanafanywa kupitia bidii za watendaji mbalimbali, maambukizi ya ukeketaji nchini Tanzania yamepungua kwa kiasi kikubwa, kutoka asilimia 15 za mwaka 2010 hadi asilimia 10 za 2016, kulingana na Utafiti wa Demografia na Afya Tanzania.

Anafafanua kuwa, ili kufikia malengo ya kuleta mazoea yenye madhara kufikia sifuri ifikapo mwaka 2030, jitihada za kuwawezesha wanawake na wasichana zinapaswa kuongezwa kwa kasi kubwa.

Mark anaeleza kwamba, hadi sasa UNFPA inaiunga mkono serikali ya Tanzania kutambua haki za wasichana na vijana, hapo akiziainisha kwa kutaja uimarishaji sera zinazozingatia vijana, kupanua programu zao.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkazi huyo, hilo linaweza kuwafikia vijana kwa taarifa na huduma za afya na uzazi, ikijumuisha kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji kijinsia na aina ya mazoea yenye madhara.

"Taarifa hizi ni muhimu kwa wasichana kufanya maamuzi sahihi kuhusu miili yao, maisha yao na maisha yao ya baadaye," anasema, akiongeza kuwa ushirikiano wao wa muda mrefu na serikali nchini, umesaidia kuanzishwa mifumo na miundombinu inayoendeleza usawa wa kijinsia kwa ujumla.

Katika hilo, anaeleza kwamba lengo lao mahsusi katika mtazamo huo ni kupitia programu tajwa, kuwasaidia wasichana na wenye ulemavu, waanaowezeshwa kijamii na kiuchumi, kufanikisha hatua hizo kikamilifu.



MAZINGIRA

# Mgodi dhahabu ulivyoungana na halmashauri kuvuta maji ziwani

**Na Mwandishi Wetu**



Tenki la maji kijijini Ilogi likiwa limekamilika tayari kwa kusambaza maji kwenye vijiji vingine katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

"MIILI yetu, miji yetu, viwanda vyetu, kilimo chetu na mifumo yetu yote ya maisha inategemea maji. Ni haki ya msingi ya binadamu na haipaswi mtu yeyote kunyimwa haki hiyo"

Ni kauli iliyokwishatolewa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres katika maadhimisho ya Siku ya Maji Duniani, ambayo huadhimishwa Machi 22 ya kila mwaka.

Anasema, hadi kufikia mwaka 2019, imekadiriwa watu bilioni 2.1 walikuwa wanaishi bila ya maji safi kutokana na sababu za kiuchumi, kijinsia, kidini, kiumri na hata kisasili.

Anaongeza kwamba, ongezeko la mahitaji pamoja na udhibiti duni mbovu wa raslimali ya majini, ni miongoni mwa sababu zinazochangia ukubwa wa tatizo la ukosefu wa majisafi na salama katika sehemu nyingi duniani, ingawa mabadiliko ya tabianchi yameongeza ukubwa wa tatizo hilo katika baadhi ya maeneo.

Guterres anasema kwamba ifikapo mwaka 2030 inakadiriwa watu milioni 700 huenda wakatawanyika isivyo kawaida duniani kote kutokana na upungufu mkubwa wa maji, endapo hatua madhubuti hazitachukuliwa.

Anatoa wito wa kuwepo ushirikiano wa wadau wote kukabiliana na changamoto ya ama upungufu au ukosefu wa maji duniani, hususan mabadiliko ya tabianchi, ili kuhakikisha wote walio hatarini wanapata huduma ya maji.

**HALI YA TANZANIA**

Wakati hali ya upatikanaji majisafi na salama ikitazamwa kwa mlengo huo duniani, nchini watendaji wa taasisi zote zilizopo chini ya Wizara ya Maji wametakiwa kuongeza ushirikiano ili kuweza kufanikisha malengo ya serikali ya kuwafikishia watanzania wote huduma ya maji ya uhakika.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi, Anthony Sanga, amewahimiza watendaji wa sekta ya maji, kuwa waadilifu na kutoa ushirikiano katika utekelezaji majukumu yao, kuhakikisha wote wanapata huduma ya maji safi na salama, kutosheleza mahitaji yao.

Aidha, akazitaka Mamlaka za Maji nchini kutatua kero na kumaliza changamoto zinazowakabili wananchi katika maeneo yao.

Pia, anafafanua uhimizaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kwamba umesaidia maeneo mengi ya vijijini kufikiwa na huduma ya maji tofauti na kabla ya kuanzishwa mamlaka hiyo.

"Kwa kiasi kikubwa kero ya maji vijijini imepungua na wananchi wengi wanapata huduma ya majisafi na salama, kwani wastani wa idadi ya watu wanaopata majisafi na salama vijijini imeongezeka kutoka asilimia 47 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 70.1 mwaka 2020,"ametamka Mhandisi Sanga.

Mijini, hali ya upatikanaji huduma ya maji imeongezeka kutoka asilimia 74 mwaka 2015 hadi kasilimia 84 mwaka 2020, baada ya kukamilika miradi 155 ya maji.

**DARASA KUTOKA MSALALA**

Halmashauri ya Wilaya ya Msalala mkoani Shinyanga, ni moja ya maeneo ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakikabiliwa na ukosefu wa huduma ya uhakika ya majisafi na salama.

Pia, kuna imani kwamba majini kuna mahitaji muhimu duniani na kiwango cha maendeleo ya jamii yoyote hutegemea uwepo wa maji ya kutosha na yenye ubora unaotakiwa.

Halmashauri ikiamini katika upatikanaji majisafi na salama, kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na usafi wa mazingira, ni muhimu katika kulinda afya za wananchi na kwamba kutumia maji ambayo si salama na uhaba wa maji, huchangia katika kusababisha milipuko na kuenea magonjwa kama kuhara na kipindupindu.

Katika taarifa yake kuhusu upatikanaji maji, Halmashauri ya Wilaya Msalala inakiri kwamba uhai wa viumbe, maendeleo ya kijamii na kiuchumi, haina uwiano sawa wa mgawanyo wa maji, kati ya sehemu moja na nyingine, katika majira mbalimbali.

Pia, lengo la halmashauri hiyo imekuwa kuhakikisha huduma bora za maji kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, inayoelekeza asilimia 85 ya wananchi wote vijijini kupata huduma ya maji kwa umbali usiozidi mita 400.

Kwa mujibu wa sensa yamwaka 2012, Halmashauri ya wilaya ya Msalala ilikuwa na wakazi 250,727, wakazi 129,376 sawa na asilimia 51.6 pekee ndiyo wanapata huduma ya majisafi na salama.

Ili kukabiliana na upungufu wa majisafi na salama, Halmashauri ya Msalala ikaja na wazo la kutekeleza mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, utakaopitia baadhi ya vijiji vya Halmashauri za Nyang'wale na Shinyanga Vijijini vikinufaisha zaidi ya watu 100,000.

**KAZI YA MGODI**

Mgodi wa Dhahabu wa Barrick Bulyanhulu uliopo katika Halmashauri ya Wilaya Msalala, ndio unaofadhili mradi huo wa maji kutoka Ziwa Victoria.

Kwa kuzingatia walakini huo wa upatikanaji majisafi na salama, mgodi huo wa Barrick Bulyanhulu uliamua kutenga shilingi bilioni 4.5 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji.

Ofisa Uhusiano wa mgodi huo, Anthony Sebastian, anasema ni muda mrefu mgodi huo umekuwa ukigharimia uchimbaji wa visima vya maji katika vijiji jirani, lakini maji yamekuwa yakipungua kila mara, kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Anabainisha kwamba takribani vijiji 14 vilivyopo katika Halmashauri za Msalala, Nyang'wale na Shinyanga, vinatarajia kunufaika na mradi huo pindi utakapokuwa umekamilika.

Anavitaja vijiji hivyo ni: Ilogi, Igudija, Kakola, Bushing'we, Kakola Namba 9, Lwabakanga, Lushimba, Kafita, Izunya, Mwamakiliga, Kharumwa, Nyugwa, Mwenge na Mahando.

Anasema, utekelezaji wa mradi huo wa maji umefika katika Kijiji cha Ilogi ukihudumia wananchi na kazi inayoendelea sasa ni kuchimba mitaro kwa ajili ya kufikisha huduma katika vijiji vingine vilivyo katika mpango huo.

Sebastian anasema, kama ilivyo malengo ya jumuiya za kimataifa kuhakikisha binadamu wote wanapata huduma ya majisafi na salama, mgodi wa Barrick Bulyanhulu uliona ni wakati mwafaka kushiriki katika utekelezaji wa azma hiyo.

"Matarajio ni makubwa sana miongoni mwa wakazi wa vijiji vinavyozunguka mgodi wa Barrick Bulyanhulu, kwani mradi utakuwa umepunguza kwa kiasi kikubwa kero ya muda mrefu ya ukosefu wa huduma ya maji,"anasisitiza.

Habiba Bashiru, ni Msimamizi wa Mradi wa Maji katika Kijiji cha Ilogi, ambako tayari wananchi wameanza kunufaika, anasema kijiji hicho kinacho chombo cha watoa huduma ya maji ngazi ya jamii, kinachofahamika Community Based Water Services Organization (CBWSO).

Anasema hivi sasa mradi huo unasimamiwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na utakapokamilika utakabidhiwa rasmi kwa chombo hicho cha watoa huduma ya maji ngazi ya jamii.

Akizungumzia hatua za ujenzi kijijini Ilogi, Habiba anasema kwamba kuna matenki makubwa yako mawili, moja limeshakamilika na lingine lenye ujazo kama huo linaendelea.

Kwa mujibu wa Habiba, matenki hayo kijijini Ilogi, ndiyo yatakayokuwa yanasambaza maji katika vijiji vingine vya Igudija, Bugarama na Bunango.

"Tunatarajia kabla ya mwaka huu kwisha nalo litakuwa limekamilika na kuanza kupeleka maji katika vijiji vingine vya jirani," anahitimisha Habiba.



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, alipokagua mradi wa maji wa Kakola-Bushingwe katika Halmashauri ya Msalala Wilayani Kahama, huku wananchi wa Kata ya Bulyanhuru wakishuhudia, mwaka jana. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

# Klabu za shule zinavyonusuru mabinti wa wafugaji ndoa, ukeketaji, ngono...

## • DC mstaafu Mkwasa awapa neno

**Na Christina Haule, Morogoro**

MKUU wa Wilaya Mstaafu, Betty Mkwasa, amezindua klabu ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mela iliyopo kijiji cha Mangae Wilayani Mvomero, inayomsaidia mtoto wa kike kujitambua kuwa na malengo na kujiepusha na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Betty, ambaye pia ni Mjumbe na Bosi wa Taasisi inayojihusisha na masuala ya kupinga ukatili wa kijinsia anasema kuzindua klabu za kijiamini na malengo shuleni, inasaidia kuwajengea uwezo wanafunzi wa kike kutambua haki zao na kuishi nazo.

Mkwasa anasema, klabu za wanafunzi shuleni zinawaweka watoto pamoja na kuwafundisha masuala ya kupinga ukatili wa kijinsia, ikiwemo kuolewa katika umri mdogo, ukeketetaji na kusumbuliwa na wanaume masomoni, pia majumbani, ufaulu wao ukiongezeka shuleni.

Anasema, klabu hiyo itafanya kazi vyema huku yeye akiwa mlezi ambaye atahakikisha inakuwa na katiba yake na kuwa klabu ya mfano mkoani Morogoro huku ikiwa na kauli mbiu ya 'niache nisome'.

Betty anasema elimu watakayoipata, itawasaidia wanafunzi wa kike kujiamini na kuwa na nguvu ya kutoa malalamiko yao ya matendo ya ukatili wa kijinsia wanayotendewa kwenye sehemu husika, ikiwemo kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa au Kijiji, Ofisa Mtendaji Kata, au Kijiji na hata polisi kwenye Dawati la Jinsia.

Betty ambaye pia awali alikuwa mwanahabari, anawaasa wanafunzi wa kike kujiwekea malengo mapema na kuhakikisha wanatimiza bila ya pingamizi la kijamii, sambamba na kuwa wajasiri.

Hata hivyo, anawaasa wazazi, wafugaji wa jamii ya kimasai ambao ndio huzuia watoto kwenda kusoma kuacha mara moja, tabia hiyo na kuwaacha wasome hadi elimu ya juu, badala ya kulazimishwa kuolewa na kukatisha ndoto zao.

### WADAU WAFUNGUKA

Mmoja wa wazazi ambaye ni mfugaji wa jamii ya Kimasai, Isack Kalaita (30), anasema kutokana na elimu wanayoendelea kuipata sasa, wameanza kubadilika na kuona umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike na kuiunga mkono yeye kama baba atahakikisha mwanawe anayepata elimu ya msingi sasa, anafika kidato cha sita.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule za Msingi Manage, Sekondari ya Mela na Melela wakiwa pamoja wakisubiri kupewa elimu ya ukatili wa kijinsia kwenye Uwanja wa Bodaboda, wilayani Mvomero, mkoani Morogoro. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE.**

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mela, Salehe Juma, anakiri kuwepo ukatili kijinsia kijijini hapo na anasema, kwa sasa umeanza kupungua, baada ya kufika asasi mbalimbali kutoa elimu na anapongeza jitihada za uanzishwaji wa klabu shuleni kunusuru mabinti.

Anakadiria miaka mitano nyuma, kulikuwapo changamoto za matukio ya ukatili kijinsia, kila mwaka ikiwemo ndoa za utotoni, ukeketaji na kurithiana mke kwa jamii ya wafugaji hao.

Juma anasema, changamoto hizo kwa sasa zimepungua kwa asilimia 70, akiamini atafuta asilimia 30 iliyobaki.

Pia, anataja ndoa katika umri mdogo mara nyingi imekuwa ikijitokeza kwa jamii ya wafugaji ambao kwa sasa nao wanaitikia wito wa kupewa elimu na kuanza kubadilika.

Kuhusu ukeketaji, anasema sasa inafanywa kwa usiri mkubwa, tofauti na zamani wafugaji hao waliwakusanya watoto zaidi ya 10 wa umri tofauti kutoka vijiji mbalimbali katika kijiji kimoja na mangariba wanaingizwa kwenye kijiji husika bila kificho, jambo ambalo sasa halipo.

Upande wa kurithiana wake baada ya mwanaume kufariki, anasema sasa limeanza kupungua, kwa sababu kinamama wameanza kuelimika na wanakataa hatua hiyo, sasa mwenendo kubadilika kuwa wakubaliane kwanza na kama mwanamke hataki, basi ndoa inasitishwa.

"Mwanzoni ilikuwa baada ya kufiwa na waume zao hawana chaguo hulazimishwa kuolewa na kaka au wadogo wa waume zao waliofariki," anasema Juma.

Anasema anapowahoji wanaoendekeza ukeketaji, wanadai ni kumuepusha mtoto wa kike na maradhi, sambamba na kumsaidia kuzaa salama.

Mmoja wa wanafunzi wa jamii ya kifugaji, Pendo Saitu (13) anasema hawezi kuruhusu vitendo vya ukeketaji, kwa sababu tayari ameshapata elimu ya kuzuia ukatili wa kijinsia na anajua mbinu za kufanya kujiepusha nayo.

### MWENYEKITI KAMPENI

Mwenyekiti wa Kampeni ya Kitaifa Kutokomeza na Kupinga Ukatili nchini kupitia Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA) mkoa wa Morogoro, Mirvan Machina, anasema vitendo vya ukatili wa kijinsia vinapaswa kupigiwa kelele, ikiwemo kuanzisha klabu za wanafunzi shuleni, kwani mtoto anaweza kufanyiwa ukatili hata akiwa njiani kwenda au kurudi shule.

Anawaasa wazazi kuwa wa kwanza kuwaepusha watoto na vitendo hivyo kwa kuacha kuwaandika majina yao nyuma ya masweta ya shule, kwa sababu yanasababisha kuitwa na watu wakatili kuwafanyia vitendo vya kinyama.


"Mtoto ana tabia ya kumzoea mtu anayejua jina lake mapema akiamini anamjua au anajuana na wazazi wake, kumbe sio kweli na anaweza kufanyiwa ukatili wa aina yoyote ile bila kujua" anasema Machina.

Mwanafunzi wa Kidato cha Kwanza Shule ya Sekondari Mela, Naifa Swamanga, anapongeza timu ya Arise and Shine kwa kuanzisha klabu ya wanafunzi shuleni kwao, akitaka wanafunzi wa kike na kiume waepukane na changamoto za ukatili kijinsia shuleni.

Swamanga, anasimulia usumbufu kimapenzi kwa wanafunzi sio kwa walimu wa kiume pekee, pia wapo walimu wa kike kutoka shule mbalimbali kwa sasa wana tabia ya kuwapenda wanafunzi wa kiume.

Anasema, klabu itasaidia kuwaandaa wanafunzi wa kike ki-

INANDELEA UK. 20



Mkuu wa Wilaya mstaafu, Betty Mkwasa.

# Klabu za shule zinavyonusuru mabinti wa wafugaji ndoa, ukeketaji, ngono...

INATOKA UK. 19

akili wakitambua kuwa wanastahili kuvaa mavazi yenye heshima na sio yenye ushawishi mbele ya wazazi wao wa kiume kwa sababu nao ni binadamu na wanatamaa kama wengine.

**USTAWI JAMII**

Ofisa Ustawi wa Jamii wilayani Ilemela, Mwanza, Christina Mwambola, anautafsiri ukatili wa kijinsia ni kitendo cha kiukatili anachofanyiwa mtu yeyote chenye kumuumiza kimwili, kisaikolojia, kingono, kiuchumi, kimila na desturi za eneo husika.

Awaasa wanafunzi wa kike kuhakikisha wanazingatia elimu wanayopata na watakayopata kupitia klabu inayoanzishwa, kupinga ukatili wa kijinsia na kuhakikisha hawaolewi katika umri mdogo.

"Wanafunzi jifunzeni kufunguka kueleza kwenye klabu bila woga matendo ya ukatili wa kijinsia, mnayofanyiwa majumbani sababu hata kama unafanyiwa ukatili na mtu wa ndani ya familia yako, awe baba au mjomba, ofisi ya ustawi itakuweka kwenye makazi maalum yaliyotengwa na serikali." anasema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Arise and Shine Foundation, Mary Mgawe anasema taasisi hiyo hutoa elimu ya ukatili wa kijinsia wa aina mbalimbali kwa wanawake na watoto kwenye mikoa mbalimbali Tanzania, ikilenga kuwawezesha watoto kupitia kongamano na vilabu.

Anasema, taasisi hiyo yenye makao makuu yake mkoani Morogoro, imejipanga kuungana na serikali sambamba na asasi zingine za kiraia katika kukomesha suala zima la ukatili wa kijinsia nchini.



Wanafunzi wa Mvomero katika nyendo zao. **PICHA: MTANDAO,**

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi maalum Dk. Doroth Gwajima, akizungumza kwenye kipindi cha Kumekucha ITV, anasema ukatili wa kijinsia ni dhana pana inayozungumzia ukosefu wa usawa popote pale kwenye jamii.

Anautaja Mpango wa Kutokomeza Ukatili kwa Wanawake na Watoto Tanzania, ulizinduliwa mwaka 2017/18 na ulibaini mwanamke mmoja kati ya watano alitoa taarifa ya kufanyiwa ukatili wa kingono katika maisha yake.

Pia, msichana mmoja kati ya watatu na mvulana mmoja kati ya saba naye, alifanyiwa ukatili wa kingono kabla ya umri wa miaka 18 na kulenga ifikapo mwaka 2022 Juni tatizo hilo liwe limepungua kwa aina yake.

Dk. Gwajima anasema, sheria zilizopo zinapaswa kutangazwa ili kuelimisha jamii ikiwemo sheria ya mwaka 2000, inayomlinda mtoto dhidi ya ukatili katika makuzi yake na wanapaswa kuwa na tabia ya kusikia wanavyoambiwa, kuamini na kufanyia kazi.

Anasema kamati zilizoundwa zinapaswa kusimama ikiwemo mashule kusimamisha mabaraza ya watoto ili waweze kufunguka katika maeneo mengine ili kutokomeza vitendo vya ukatili.

Kwa mujibu wa ripoti ya Umoja wa Mataifa UN ya mwaka 2019,kuhusu hali ya kimataifa ya kuzuia ukatili dhidi ya watoto, imebainisha kuwa nusu ya watoto wote duniani sawa na takribani watoto bilioni moja kila mwaka wanaathirika na ukatili wa kimwili, kingono au kisaikolojia, kujeruhiwa, kusababishiwa ulemavu na kifo kwa sababu nchi zimeshindwa kuzingatia mikakati iliyowekwa ya kuwalinda watoto.

Ripoti hiyo ilitolewa kwa pamoja na Shirika la Afya Duniani (WHO), la kuhudumia Watoto (UNICEF), Elimu Sayansi na Utamaduni UNESCO na mwakilishi maalum wa Katibu Mkuu kuhusu ukatili dhidi ya watoto na wanaharakati katika mapambano dhidi ya vurugu.

Kwa pamoja, inaashiria kuna kanuni nyingi na maadili mengi yenye mizizi miongoni mwa Watanzania vijana ambao ndiyo msingi wa kuunga mkono kampeni ya kupinga ukatili, haswa unaowalenga wanawake, ingawa kuunga mkono ukomeshwaji wa ukeketaji kunatia moyo. Ni muhimu kulikabili suala la kuhalalisha ukatili kijamii.

## CHEMSHABONGO NA -00 14 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com



Dondoo: Kulia
1. kwenye akili
5. ndege mweusi msafisha mazingira 8. aibu, fedheha
9. kuwa na hamu ya kitu
11.hutumika kuvulia samaki
14.bandari ya pili kwa ukubwa
17.mlowezi 18.lugha ya Pakistani
19.chomeka 20.umri wa watu
22.mji mkuu wa Peru
24.mjumbe wa Mungu 25.nswi
26.vunja kanuni za nchi 27.labda

Chini:
1. watoto wa ndege
2. sampuli
3. piga ramli
4. utokeaji usiotarajiwa
6. ukuta
7. bomu dogo la mkono
9. fanya kitu kivimbe
10.poromoka
12.chimbuko
13.lalia mayai kama kuku
15.shauku 16.kinyume cha nje
21.Baba 23.kanya

## Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

MLANGUZI IAN
NGONJERA FUO
ALAMA IASI
IKABU MDH
PANAMA ZAA
UPARA CHE
UPINZANI NUSA
PAKUA ONEA
ANASA RABA
AHERA AMU
CHAMANZI RAJ
DHARAU GAMU
MALENGO OSLO
NANGA NIA
RAHA GIA

A
M
U

Majibu toleo lililopita



| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | W | E | N | D | A | M | B | I | Z | E |
| A | | I | | | M | | | | | T |
| J | A | N | G | W | A | | | | | H |
| I | | A | | | Z | | | | | I |
| | | | M | T | O | | | | | O |
| M | B | A | B | A | N | E | | | | P |
| K | | M | A | N | I | L | A | | | I |
| U | | B | | D | | E | N | D | E | A |
| N | Y | I | K | A | | W | A | A | | |
| G | | W | | Z | | A | S | A | L | I |
| U | S | A | W | A | | | A | | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | T | O | T | O | | U | G | U | A |
| V | A | M | I | A | | F | A | R | U |
| U | M | B | A | | T | A | N | U | A |
| A | B | I | R | I | A | | D | | N |
| | A | | A | | J | U | A | N | A |
| D | A | U | | F | A | U | L | U | |
| A | | M | B | U | | Z | O | B | A |
| K | I | B | A | N | D | A | | I | |
| A | N | U | | G | | J | U | A | |
| R | I | A | K | A | | I | | | |



# Polisi yaanza kampeni ya elimu kwa wananchi kurejesha silaha

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZIKIWA zimebaki siku 11 kabla ya kumalizika kwa amri ya urejeshaji wa silaha haramu kwa hiari, Jeshi la Polisi mkoani Mbeya, limeanza kupita kwenye nyumba za ibada kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara ya kuendelea kumiliki silaha hizo.

Septemba, mwaka huu, serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ilitoa miezi miwili kwa wananchi wanaomiliki silaha haramu kuziwasilisha kwenye ofisi mbalimbali za serikali na vituo vya polisi.

Pia iliagiza jeshi hilo kufanya msako na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakaokutwa na silaha hizo baada ya muda huo kumalizika.

Juzi lilifanyika kongamano katika Kanisa la Mti wa Uzima jijini hapo ambalo kwa ajili ya kuwakutanisha waumini na vongozi wa Jeshi la Polisi walishiriki ili kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kurejesha silaha hizo.

Mwakilishi wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Sylvester Chimwaga, alisema wananchi wanapomiliki silaha isivyo halali, kuna hatari ya matukio ya uhalifu kuongezeka kwenye jamii.

Aliwataka wananchi kuhakikisha wanazitumia siku chache zilizobaki kuwasilisha silaha hizo ili zifanyike taratibu za kumilikishwa kihalali na kwamba baada ya siku hizo kukamilika, itafanyika operesheni maalumu ya kuzisaka.

**Kuna baadhi ya watu ndugu zao walikuwa wanamiliki silaha hizo lakini walifariki dunia na kuziacha silaha hizo. Sasa hizo silaha huwa wananchi wana tabia ya kurithishana kama ilivyo kwa mali zingine jambo ambalo si halali.**

Chimwaga alisema kwa mtu yeyote atakayekutwa na silaha hizo atachukuliwa hatua kali za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia ya kujimilikisha bila kufuata utaratibu.

"Kuna baadhi ya watu ndugu zao walikuwa wanamiliki silaha hizo lakini walifariki dunia na kuziacha silaha hizo. Sasa hizo silaha huwa wananchi wana tabia ya kurithishana kama ilivyo kwa mali zingine jambo ambalo si halali," alisema.

Chimwaga alisema silaha ambazo wamiliki wa awali walifariki dunia na zinamilikiwa na wanafamilia wengine, hivyo zinatakiwa kuwasilishwa kwa Jeshi la Polisi ili zifanyike taratibu za kumilikishwa kihalali.

Baadhi ya viongozi wa dini mkoani Mbeya, walisema kampeni hiyo ni nzuri na itasaidia kuwaepusha wananchi kuingia kwenye matatizo kwa maelezo kuwa hata wao viongozi wa dini watashiriki kwenye uhamasishaji.

Mwenyekiti wa Umoja wa Huduma za Kitume na Kinabii mkoa wa Mbeya, Suleiman Masawe, alisema Jeshi la Polisi lilitangaza msamaha kwa wananchi watakaosalimisha silaha hizo kwa hiari na hivyo wananchi wanatakiwa kuutumia vizuri msamaha huo.

Alisema msamaha huo unawapa nafasi pia viongozi wa dini kushiriki kwenye hamasa hiyo kwa maelezo kuwa msamaha ni sehemu ya ibada kwa mujibu wa dini.

"Tunalishukuru Jeshi la Polisi kwa kuamua kushirikiana na sisi kwenye zoezi hili, tutaendelea kuwahamasisha wananchi kurejesha silaha hizo maana wakati mwingine huwa wananchi wanakosa uelewa tu," alisema Masawe.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Oscar Ongere, alisema baadhi ya wananchi wanaomiliki silaha hizo kinyume cha sheria wanaweza wakahatarisha amani na utulivu mitaani kutokana na kutokuwa na mafunzo ya matumizi sahihi.

Aliliomba Jeshi la Polisi kuendelea kuhamasisha wananchi kupitia makundi mbalimbali ili siku zilizobakia zitumiwe vizuri na wananchi ambao bado hawajazisalimisha.

## Mkuu wa Mkoa ataka ufanisi programu kilimo

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SERIKALI mkoani Mbeya imewataka watekelezaji wa Miradi ya Programu ya Uboreshaji wa Mnyororo wa Thamani wa Kahawa, Chai na Mazao ya Bustani (AGRI-CONNECT), kuitekeleza kwa ufanisi ili wafadhili waone matokeo na waendelee kutoa fedha zao.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa agizo hilo wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Programu hiyo kilichofanyika wilayani Kyela ambapo alisema Umoja wa Ulaya (EU) unatoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Alisema wakati wa ziara ya kamati hiyo kwenye miradi mbalimbali inayotekelezwa na mashirika mawili ya HELVETAS na RIKOLTO, walishuhudia miradi hiyo ikiendelea kutekelezwa kwa kiwango kinachoridhisha.

Miradi hiyo, alisema inatakiwa kuendelea kutekelezwa kwa viwango hivyo ili wafadhili hao watakapokwenda kutembelea waone thamani ya fedha wanazotoa kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

Alisema walitembelea masoko mbalimbali ambayo yanajengwa na mashirika hayo mawili katika wilaya za Mbeya na Rungwe, viwanda pamoja na mashamba ya wakulima mbalimbali ambao wamesaidiwa na mashirika hayo.

"Programu hii ni muhimu tukaisimamia vizuri ili kuhakikisha inawasaidia wananchi, nilifurahi sana pale kwenye kiwanda cha kuchakata matunda na mboga pale uwanja wa ndege wa zamani, ni kiwanda cha kisasa ambacho kweli kitatusaidia," alisema Homera.

Alisema viongozi wa serikali wanatakiwa kufuatilia mara kwa mara miradi hiyo ili kuhakikisha inatekelezwa kwa viwango vinavyotakiwa na wahakikishe inawanufaisha wananchi wote.

Hata hivyo Homera aliwataka wananchi kuitumia vizuri miundombinu inayojengwa na mashirika yanayotekeleza miradi hiyo hasa barabara na viwanda ili kupata tija kwenye kilimo chao.

Alisema katika moja ya barabara zinazojengwa kwa kutumia fedha za programu hiyo, waliamua kumfukuza mkandarasi wa awali na kuajiri mwingine baada ya kubaini kuwa wa awali alikuwa mbabaishaji.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Rodrick Mpogolo (kushoto), Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune (katikati) na mmoja wa wanachama wa Chama cha Wakulima wa Vitunguu cha Skimu ya Umwagiliaji ya Igomelo, Wilaya ya Mbarali, wakiwa wameshika vitunguu wakati Kamati ya Ushauri ya Programu ya AGRI-CONNECT, ilipofanya ziara ya kukagua ghala lililojengwa na Shirika la HELVETAS, wilayani humo hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Posho walimu zatajwa udanganyifu mitihani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UCHELEWESHAJI wa posho kwa walimu wanaoteuliwa kusimamia mitihani katika shule za msingi na sekondari nchini, umetajwa kuwa chanzo cha uwapo wa udanganyifu kwenye mitihani hiyo na kukwamisha maendeleo ya sekta ya elimu.

Hayo yalisemwa juzi na baadhi ya walimu katika wilaya ya Mbeya wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) huku wakisema ucheleweshaji huo wa posho unasababisha walimu kuingia kwenye majaribu.

Mmoja wa walimu hao, Ombeni Hare, alisema walimu wanashindwa kupata fedha za kujikimu kwa wakati, hivyo kushindwa kupata mahitaji yao muhimu.

Alisema hali hiyo huwa inawafanya kuwa na maisha magumu, hivyo kuwa na uwezekano wa kuingia kwenye vishawishi vya kushiriki kuvujisha mitihani.

"Kwa hiyo hali hii inaweza ikawa miongoni mwa vyanzo vya kuharibika kwa elimu yetu. Tunaiomba serikali iwe inatuwahishia posho hizo ili kuepuka mazingira kama haya," alisema Ombeni.

Naye Mwalimu Joel Kaluka alisema walimu wanapopangiwa vituo vya kusimamia mitihani huwa wanakuwa na imani kwamba watapata fedha kwa ajili ya kuendeshea maisha ya familia zao, hivyo wanapokosa fedha hizo huwa wanakata tamaa.

Alisema wakati mwingine huwa ni rahisi kushawishika na kuanza kushiriki kwenye uvujishaji wa mitihani jambo ambalo alisema huwa linatokea sio kwa kupenda kwao.

"Mwalimu asipokuwa na hela na akashawishika kwa fedha, inakuwa ni rahisi kuingia kwenye vitendo hivi haramu vya kuvujisha mitihani jambo ambalo ni baya," alisema Mwalimu Kaluka.

Katibu wa CWT Wilaya ya Mbeya, Judith Mangi, alisema kitendo cha kuwapangia walimu vituo vya kusimamia mitihani bila kuwalipa kinawavunja walimu moyo na kusababisha ufanisi wa kazi kuwa mdogo kuliko vile ambavyo huwa inatarajiwa.

Alisema baadhi ya walimu huwa wanakwenda kwenye vituo hivyo kwa sababu ya kuwaogopa viongozi wao lakini sio kwa kupenda na hivyo akaiomba serikali kuangalia upya utaratibu huo.

Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Aliko Mbuba, alisema watahakikisha wanalishughulikia jambo hilo haraka ili kuepuka madhara yaliyoelezwa na walimu hao kwa maelezo kuwa ni haki yao.

Alisema watahakikisha walimu wanazipata stahiki zao kwa haki na kwa wakati ili wafanye kazi kwa moyo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alipiga marufuku walimu kupangiwa vituo hivyo vya kusimamia mitihani bila kulipwa stahiki zao.





# Utendaji mbovu Bodi ya Mazao Mchanganyiko waikwaza PIC

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC), imeonesha kutoridhishwa na utendaji kazi wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko (CPB) kwenye mambo mbalimbali kutokukua kimapato.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo baada ya kuhoji bodi hiyo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jerry Silaa, alisema wamepokea taarifa ya bodi lakini yapo mambo ambayo bado hayapo vizuri ni vyema wakajitathmini.

"Hesabu zao za mwaka 2020/21 yapo mengi ambayo ni chini ya malengo tuliyoweka kwenye uwekezaji wa mitaji ya umma, kigezo cha ukuaji wa mapato inapaswa shirika kila mwaka likue bila kupungua asilimia 10 ambapo wao wapo 33," alisema.

**Agosti mwaka huu Rais Samia alimteua mwenyekiti wa bodi ambaye anaonesha mwaka wa kufanya vizuri.**

Alisema matumizi yao yanatakiwa yasizidi kwa asilimia 50 lakini wapo asilimia 75.5.

"Kusema kweli bodi haifanyi vizuri na tumewauliza wapo kwenye biashara wanamiliki biashara kwa ukubwa gani hawafahamu, huwezi kuwa kwenye bahari unaogelea wala hujui kina cha bahari kimefika wapi," alisema.

Aidha, kamati hiyo ilimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa mwaka huu wa fedha 2022/23, bajeti ya kilimo imetengwa kwa kiwango kikubwa.

"Bajeti imeongezeka kwa Sh. bilioni 750, lakini kwa jitihada kubwa zilizofanywa na Waziri wa Kilimo Hussein Bashe, kuna kilimo cha mashamba makubwa, pembejeo tunaamini ni wakati wa bodi hii kujipanga,"alisema.

Pia alisema Agosti mwaka huu Rais Samia alimteua mwenyekiti wa bodi ambaye anaonesha mwaka wa kufanya vizuri.

"Tumetaka wakajipange kwenye utendaji, inafanya kazi kwa mazoea wakati hii ni bodi ya kibiashara, Watanzania wamewekeza kodi zao kwa bodi ili kuwe na tija, kazi yake inatakiwa kuhakikisha inanunua mazao kwa wakulima ili wasiuze kwa bei kandamizi," alisema.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange (kushoto), akiimba wimbo wa mshikamano pamoja na wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), wakati wa ufunguzi wa mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa TSC jijini Dodoma juzi. Kulia ni Katibu wa TSC, Paulina Mkwama. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Wataka watu kula vyakula vya asili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WADAU wa masuala ya lishe nchini wameishauri serikali kuweka mikakati ya kuhamasisha ulaji wa vyakula vya asili, ili kuimarisha afya za Watanzania.

Aidha, wamesema kuwa ulaji wa vyakula vya asili utasaidia kupunguza tatizo la kuongezeka kwa wingi kwa wagonjwa wa magojwa yasiyoambukiza kama sukari na shinikizo la damu.

Ushauri huo unakuja ikiwa Oktoba 16, mwaka huu Tanzania iliungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha kilele cha Siku ya Chakula.

Mmoja wa wadau hao, Christopher Dinoniz, akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo jana alisema ipo haja kwa serikali kuweka mikakati ambayo itasaidia kuhamasisha wananchi kutumia vyakula vya asili ili kuimarisha afya.

Alisema hivi sasa kumekuwapo na tatizo kubwa nchini la wagonjwa wa magonjwa yasiyoambukiza ambayo pia yanaipatia mzigo wa gharama kubwa za matibabu serikali.

"Katika maadhimisho ya mwaka huu ambayo yamefanyika kitaifa wilayani Bariadi mkoani Simiyu tumeona namna ambavyo kumekuwa na hamasa kubwa ya ulaji wa vyakula vya asili.

"Hivyo tunaiomba serikali kuona ni jinsi gani itasaidia kuwezesha matumizi ya vyakula vya asili kwa kuandaa maonyesho ambayo yatawekewa utaratibu katika ngazi ya wilaya au mikoa ili jamii kujifunza na kuachana na matumizi ya vyakula ambavyo vimekuwa vikiathiri afya za walaji, lakini kufundisha namna ya utunzaji wa mbegu kama ambavyo tulikuwa tukifanya zamani katika kilimo hai,"alisema.

Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza hivi karibu kwenye hafla ya utiaji saini mkataba wa usimamizi wa shughuli za lishe na tathmini ya sita ya mkataba wa lishe jijini hapo, alisema ufanyike utafiti kujua wamekosea wapi na kwanini kuwapo na lishe mbovu kwa vijana.

"Kwanini kunakuwa na gap (nafasi) tunakuwa na watoto ambao hawapo vizuri kiafya wa kike na kiume, je, haya ni masuala yaliyoingia ya mitindo nataka niwe sixpack, au niwe slim (kupunguza mwili) nisizidi kilo ngapi nataka sijui mbavu ikae hivi, kuna nini hapo."

"Kwanini watoto wetu wapo hivyo, wakifika wakati wa kuwajibika kuzaa kuongeza jamii wanahangaika, mara supu ya pweza, mara sijui, tuna tatizo na mnalijua mnalificha," alisema.

Alisema chakula kikuu kwa vijana ambapo wanakula chips zege na juisi wanajaza tumbo, bila kuangalia kama inawajenga nguvu ipasavyo.

"Haikatazwi kula chips na zege lakini waelewe wanachokila ni nini pamoja na ugumu wa maisha, na sisi tutengeneze mifumo ambayo hata akila chips na kuku, mafuta yaliyotumika ni yapi, tuhakikishe mafuta yanayotumika na hivyo vinavyotumika,"alisema.

# OCD ashauri NGO kujenga nyumba za kusitiri wasichana

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

MKUU wa Polisi Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, (OCD), Grace Salia amezitaka taasisi zisizo za kiserikali kushiriki ujenzi wa vyumba vya kujisitiri kwa ajili ya watoto wa kike ili kutatua tatizo la utoro pindi wanapokuwa katika siku zao za hedhi.

Aidha, amesema jamii inapaswa kupaza sauti kwa wananchi kupitia mikutano ya hadhara, ili kuisaidia serikali kupiga vita ndoa za ututoni na ukatili wa kijinsia.

Salia alibainisha hayo katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani yaliyofanyika wilayani humo.

Alisema utoro kwa watoto wa kike shuleni umekithiri kila mwezi kutokana na wanafunzi hao kukosa sehemu ya kujisitiri wakati wa siku za hedhi.

"Tunaomba taasisi mshirikiane na serikali kusaidia ujenzi wa vyumba vya faragha watoto wa kike wanapokuwa kwenye hedhi hawaji shuleni kuepuka aibu pale wanapochafuka na kuonekana," alisema Salia.

Alisema vyumba vya faragha ni muhimu sana kwa watoto wa kike hivyo wahakikishe sehemu hiyo inakuwapo, ili kuwasitiri na kuepusha kukosa masomo kwa siku kadhaa kila mwezi.

Mbali na hilo aliitaka jamii kuendelea kupaza sauti ili kupinga ndoa za ututoni katika maeneo mbalimbali wilayani humo.

Alisema jamii iendelee kupewa elimu na kuandaliwa kwa mikutano na matamasha, ili watoto wakike kuweza kujua haki zao za msingi ikiwamo kupata elimu mpaka ngazi ya vyuo vikuu.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Mlowa Barabarani, Irene Lameck, alisema wanafunzi wengi wa kike hupoteza siku kadhaa za mahudhurio darasani kila mwezi kutokana na kukwepa aibu.

"Tumekuwa tukikwepa aibu kwa wanafunzi pale inapotokea tumechafuka ndio maana ifikapo siku hizo mtu anaamua kukaa nyumbani," alisema Ramecky.

Alisema ili kutatua changamoto hizo marekebisho ya sheria ya ndoa kandamizi dhidi ya watoto wa kike yafanyike, elimu itolewe kwa jamii kuhusu afya ya uzazi na jamii kuacha mila na desturi zinazowakandamiza watoto wa kike.

Kutokana na hilo alisema wanaomba Dawati la Jinsia pamoja na kamati ya MTAKUWWA kutoa elimu juu ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia, kutengeneza timu kwa ajili ya kupinga ukatili na kufuatilia bajeti katika kata.

# M-mama kupunguza vifo vya wajawazito, watoto

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga nchini, Serikali ya Zanzibar kwa kushirikiana na Kampuni ya Vodacom Tanzania PLC na wadau wengine wanatarajia kuzindua programu ya M-mama itakayohudumia visiwani humo.

Programu hiyo inatarajiwa kuzinduliwa Januari 12, mwakani wakati wa sherehe za Mapinduzi.

Akizungumza wakati wa kikao kazi kilichofanyika Mjini Unguja mwishoni mwa wiki, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Zanzibar, Dk. Fatma Mrisho, alisema matayarisho yote yamekamilika na kinachosubiriwa ni uzinduzi wa programu hiyo itakayookoa maisha ya wajawazito na watoto wachanga wanapopata dharura.

"Nichukue fursa hii kuwapongeza Vodacom na wadhamini ambao ni Vodafone kwa kutoa pesa na kuhakikisha mradi huu unafika

**Tulipokea msaada wa Sh. bilioni 34.9 ili kuanzisha programu hii, imeonesha mafanikio makubwa sana katika mikoa ya Shinyanga, Geita, Morogoro na Lindi, na hapa tunavyoongea mwezi ujao tutazindua mradi huu katika mikoa ya Tanga na Dodoma.**

visiwani, ni hatua nzuri maana itaokoa kinamama na watoto waliokuwa wakipoteza maisha kwa kukosa huduma ya usafiri wanapopatwa na dharura," alisema Dk. Mrisho.

Alisema katika kusaidia utoaji wa huduma za dharura, serikali imetoa magari ya kubebea wagonjwa wa dharura, pia Vodacom na washirika wa mradi watakuwa na magari yanayomilikiwa na wanajamii ili kusaidia ubebaji wa wagonjwa magari yanapokuwa mbali na eneo alipo mgonjwa.

Kadhalika, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikithamini michango inayotolewa na wadau mbalimbali hususani katika sekta ya afya, M-mama itakuwa ni sehemu muhimu ya kuokoa maisha ya kinamama wajawazito na watoto wachanga, hasa kwa vile imeshaonesha mafanikio katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

Meneja Mawasiliano wa Vodacom Tanzania PLC, Alex Bitekeye, alisema nguzo mojawapo ya kampuni hiyo ni ujumuishwaji wa wote na kupitia sekta ya afya waliona kuna umuhimu wa kusaidia kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga hasa kupitia mradi huo.

"Tulipokea msaada wa Sh. bilioni 34.9 ili kuanzisha programu hii, imeonesha mafanikio makubwa sana katika mikoa ya Shinyanga, Geita, Morogoro na Lindi, na hapa tunavyoongea mwezi ujao tutazindua mradi huu katika mikoa ya Tanga na Dodoma," alisema.

Akizindua programu hiyo jijini Dodoma, Agosti mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alisema serikali imeagiza magari ya kubeba wagonjwa 233 yatakayopelekwa mikoa yote nchini.

Alisema pia serikali imeagiza magari 242 ya uratibu huku akieleza kuwa ni matumaini yake yatakwenda kuongeza nguvu katika mpango wa M-mama ili kuwawahisha watoto na kinamama hospitalini.



Naibu Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Shabaan Ali Othman (kulia), akipokea zawadi ya kuku jogoo, kutoka kwa wakazi wa shehia ya Kinooni, Kijiji cha Kiboje jana, baada ya kutimiza ahadi ya kuwafikishia umeme kijijini hapo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wafanyakazi vituo vya afya wakumbushwa uadilifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAFANYAKAZI wa Hospitali ya Wilaya ya Kusini Unguja iliyoko Makunduchi na vituo vya afya vilivyoko wilayani humo wametakiwa kufanya kazi kwa uadilifu wanapowahudumia wananchi na kuwapo kazini muda wote wa kazi.

Wito huo ulitolewa jana na Naibu Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan Khamis Hafidh, katika ziara ya kushtukiza aliyoifanya kwa kushirikiana na timu ya ukaguzi wa huduma za afya kuangalia utendaji wa kazi kwa wafanyakazi wa hospitali na vituo hivyo vya afya.

Alisema bado utendaji wa kazi kwa baadhi ya hospitali na vituo vya afya hauridhishi kutokana na baadhi ya wafanyakazi kuchelewa kufika na kuondoka mapema kazini na kusababisha huduma za afya zinazotolewa kukosa ubora na malalamiko.

Alisema kuwa kutokana na hali hiyo, serikali kupitia Wizara ya Afya haitosita kumchukulia hatua za kiutumishi mfanyakazi ambaye atakiuka sheria za kazi na kuwataka wafanyakazi hao kufanya kazi muda wote ili kutoa huduma zenye ubora kwa wananchi.

Aidha, aliuagiza uongozi wa hospitali ya wilaya kufanya jitihada ili huduma zote za afya katika hospitali hiyo zitolewe ikiwamo dawa na vipimo ili kuondoa usumbufu kwa wananchi.

Alisema, uongozi wa wizara na wakaguzi wataendelea kufanya ziara za mara kwa mara katika hospitali zote na vituo vya afya vyote Unguja na Pemba kuangalia namna ya utoaji wa huduma za afya kwa wananchi pamoja na masuala ya dawa na vifaa tiba.

Kwa upande wao wafanyakazi wa hospitali ya wilaya hiyo na wa vituo vya afya waliahidi kutoa huduma bora kwa wananchi na kufuata kanuni za utumishi kama inavyotakiwa na kuahidi upungufu wowote kushughulikiwa ili huduma ziwe zenye ubora.

# Waandishi wa habari watakiwa kuhamasisha chanjo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAANDISHI wa habari wametakiwa kushirikiana na masheha na viongozi wa dini kuhamasisha jamii umuhimu wa kupata chanjo ya UVIKO-19 na kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

Mkufunzi kutoka Shirika la Internews Kanda ya Zanzibar, Shifaa Said Hassan, aliyasema hayo juzi wakati akifunga mafunzo kwa kamati ya uhamasishaji wa chanjo ya UVIKO-19, iliyowashirikisha masheha, jamii, viongozi wa dini na watu wa afya yaliyoandaliwa na Internews yaliyofanyika Mjini Zanzibar.

Alisema chanjo hiyo ni muhimu katika kujikinga na ugonjwa huo na Zanzibar kama sehemu ya dunia iliathirika na ugonjwa huo.

Shifaa alibainisha kuwa ni wazi kuwa ugonjwa huo ni hatari duniani na umeleta athari kubwa katika nyanja zote za kiuchumi na kushuhudia vifo vingi.

Aliwataka wanahabari kutumia nafasi yao kuendelea kuihamasisha jamii kushajihisha wananchi umuhimu wa chanjo hiyo.

Naye mkufunzi Ali Haji Mwadini, aliwataka wanahabari kutumia nafasi zao kuendelea kuhamasisha jamii umuhimu wa kupata chanjo ili kujikinga na ugonjwa huo.

Akisoma taarifa mjumbe wa kamati ya mafunzo ya Internews, Amina Makame Haji, Ofisa wa Afya kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, alisema kuna umuhimu mkubwa kwa wanahabari kuhamasisha umma kuhusu UVIKO-19.

Alisema chanjo hiyo imeanza rasmi tangu mwaka 2021 na hadi sasa inaendelea lakini bado lengo kuu halijafikiwa na ipo haja ya kuhamasisha jamii umuhimu wa chanjo hiyo.

Alibainisha kwamba taarifa zilizokuwapo Wizara ya Afya zinaonesha asilimia waliopata chanjo imefikia 51 ambayo ni sawa na watu 372,841 na malengo ifikapo Desemba 2022 inatarajia iwe imefikia idadi ya asilimia 70 ambayo ni sawa na watu 745.481.

Amina alisema hali hiyo inaonesha kuwa wanajamii hawana mwamko mkubwa wa kuchanja chanjo hiyo na kusababisha watu wengi kutokuwa na kinga dhidi ya maradhi hali inayotia wasiwasi ya kuwa maradhi hayo yanaweza kuibuka tena na kuongeza maambukizi ya maradhi hayo.

Waliihamasisha jamii na kuelimisha wananchi kuachana na dhana potofu zinazohusiana na chanjo ya maradhi hayo.

Kasongo Omar Kasongo, Sheha wa Shehia ya Mwakaje, alisema wanaendelea na kazi ya kuhamasisha wananchi kuchanja ili kukabiliana na ugonjwa huo, lakini bado jamii imekuwa na usiri katika kuchanja.

"Tunaendelea kuhamasisha jamii kupitia mikusanyiko mbalimbali ya watu lakini bado kazi kubwa inahitajika ili jamii kuhamasika kuchanja," alisema.





# DC ataka wanaume kutokimbia familia kwa ugumu wa maisha

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amewataka wanaume wilayani hapo kutozikimbia familia zao kutokana na ugumu wa maisha unaochagizwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mboneko amesema licha ya kuwa katika kipindi hiki ambacho hali ya hewa si nzuri kutokana na ukosefu wa mvua, wanaume wasitumie mwanya huo kuzikimbia familia huku akiwasihi kutunza chakula walicho nacho ili kukabiliana na baa la njaa.

**Baadhi ya wananchi waliomba serikali kufuatilia na kudhibiti mfumuko wa bei ya vyakula ili kushusha ongezeko la gharama za maisha.**

Mboneko alitoa wito huo kwa nyakati tofauti wakati wa mikutano ya hadhara kukagua shughuli za maendeleo, ambapo aliwataka wahifadhi vyakula walivyo navyo ili wasije wakakumbwa na baa la njaa.

Alisema ukosefu wa mvua unaweza kusababisha upungufu mkubwa wa chakula hatua inayosababisha wanaume kuzikimbia familia zao, hivyo kuwataka kutunza chakula ili kuepusha ukosefu wake wilayani humo.

Pia aliwataka maofisa kilimo wilayani humo kutoa elimu ya kilimo bora kwa wananchi, pamoja na kulima mazao yanayostahimili ukame, kutokana na hali ya hewa kuonyesha kutakuwa na uchache wa mvua.

Katika hatua nyingine, Mboneko aliwataka maofisa kilimo kuorodhesha majina ya wakulima wote, ili kupata mbolea ya ruzuku ambayo itawasaidia katika msimu wa kilimo mwaka huu na kupata mavuno mengi.

Baadhi ya wananchi waliomba serikali kufuatilia na kudhibiti mfumuko wa bei ya vyakula ili kushusha ongezeko la gharama za maisha kwa wananchi.




Mganga Mkuu Mkoa Mwanza, Dk. Thomas Rutachunzibwa (wa pili kulia), akifungua mafunzo ya siku moja kwa waandishi wa habari jijini Mwanza jana, kuhusu namna ya kuandika kwa weledi habari za Uviko-19 , tathmini ya chanjo ya Uviko-19 na uhuru wa kupata taarifa chini ya mradi wa 'Boresha Habari'. **PICHA: NEEMA EMANUEL**

# RC aagiza kukamatwa aliyetoweka na mamilioni ya AMCOS Geita

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Martine Shigella, ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani Geita kumsaka kiongozi wa Chama cha Ushirika AMCOS wilayani Nyang'hwale, anayedaiwa kutoweka na fedha za malipo ya wakulima wa pamba msimu uliopita zaidi ya Sh. milioni 10.

Shigella alitoa agizo hilo juzi kwenye kikao cha Bodi ya Pamba kilichofanyika mjini hapo na kuwashirikisha wakulima maarufu wa zao hilo, maofisa ushirika na wanunuzi.

Alisema haiwezekani ushirika uwafanye wakulima kuwa masikini ikiwa matarajio ya serikali ni kuona ushirika unainua wakulima badala ya kuwaumiza, huku akitaka hamasa zaidi kwenye zao la pamba.

"Nimesikia hapa Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwale anasema kuwa kuna wakulima wanadai fedha ya msimu uliopita kufuatia kiongozi mmoja wa AMCOS kutoweka na fedha hiyo naliagiza Jeshi la Polisi limsake popote alipo ili wakulima wapate haki yao." Alisema.

Kuhusu kushuka kwa bei ya pamba, Shigela aliahidi kuwashirikisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) kunusuru soko la zao hilo, huku akiwataka wakurugenzi watendaji wa halmashauri kuwekeza kwenye zao la mkakati lenye tija kwenye maeneo yao.

Agizo la kiongozi huyo linakuja baada ya Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwale, Jamhuri Wiliam, kukieleza kikao kuwa wakulima wanadai fedha za msimu uliopita zaidi ya Sh. milioni 10.

Awali mkuu huyo wa wilaya, akichangia wakati wa kikao hicho, alisema katika wilaya hiyo wakulima bado wanadai fedha zao baada ya kiongozi mmoja kutoweka na fedha ya malipo yao.

"Wakulima Nyang'hwale wanadai mamilioni ya fedha zaidi ya Sh. milioni 10 za msimu uliopita hii ni kutokana na kiongozi mmoja wa AMCOS ambaye jina lake limehifadhiwa kutoweka na fedha hiyo," alisema.

Sharifu Ntundu, mkulima wa pamba kutoka Chato Bukombe AMCOS alisema kuwa kinachosababisha uzalishaji wa zao la pamba kushuka kila mwaka mkoani humo ni baadhi ya wanunuzi wa zao hilo kutokuwa waadilifu na wazalendo.

"Vilevile unakuta wakulima wa zao hilo hatupatiwi mikopo kama ilivyo kwa wakulima wenzetu wa zao la tumbaku wanaoaminiwa na kukopeshwa fedha na taasisi, tunaomba bodi ya pamba kusimamia kikamilifu ili wakulima wengi wakimbilie zao hili," alisema Ntundu.

Meneja wa Chama cha Ushirika Wilaya Chato mkoani hapo, Berino Msigwa, alisema msimu uliopita walinunua marobota 3,980 kati ya hayo, wameuza 3,000 na bei kwenye soko la dunia imeshuka wanahofia kuuza kwa bei ya hasara zaidi.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba Tanzania ambaye ni Meneja wa Bodi hiyo Kanda ya Ziwa, Jones Bwahama, alisema jukumu la kutafuta soko la pamba liko Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na kazi ya bodi ni kusimamia na kwamba bodi hiyo imejipanga kusambaza mbegu za pamba katika msimu mpya wa kilimo.

# Wananchi watakiwa kujenga utamaduni wa kupima afya

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WANANCHI mkoani Mwanza, wametakiwa kuwa na desturi ya kupima afya mara kwa mara hususani magonjwa yasiyoambukiza, kuzingatia taratibu za kujikinga ikiwamo kunawa mikono mara kwa mara, kuepuka misongamano, kutakasa mikono na kula chakula bora ili kuimarisha kinga ya mwili.

Hayo yameelezwa na Mganga Mkuu Mkoa Mwanza, Dk. Thomas Rutachunzibwa, wakati akifungua mafunzo ya siku moja kwa waandishi wa habari kuwajengea uelewa katika uandishi wa habari za Uviko-19 , uhuru wa kupata taarifa chini ya mradi wa 'Boresha Habari' ulioratibiwa na Chama cha Wanahabari Mkoa Mwanza (MPC) kwa ufadhili wa Shirika la Internews Tanzania na USAID.

Alisema katika mapambano dhidi ya Uviko-19 hadi Oktoba mwaka huu wananchi milioni 1.6 wamepata chanjo kamili sawa na asilimia 87 katika vituo 356 kuanzia Agosti 3, 2021 huku lengo la mkoa likiwa ni kuchanja watu milioni 1.8.

Alisema mafanikio hayo yanatokana na taarifa na elimu inayotolewa na vyombo vya habari huku akiwaomba waandishi wa habari kuhamasisha zaidi wananchi kuwa na desturi ya kupima afya hususani magonja yasiyoambukiza kama walivyosaidia kufanikisha utoaji wa chanjo ya UVIKO-19.

"Niwaombe waandishi msibweteke katika hili kwa kudhani Uviko-19 umeisha na kwamba bado upo ingawa umeshuka hivyo ni vyema kuendelea kuchukua tahadhari," alisema Dk. Rutachunzibwa.

Akizungumza kwenye mafunzo hayo, Mratibu wa elimu ya afya kutoka ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa Mwanza, Renard Mlyakado, alisema toka ugonjwa huo uingie nchini tayari imerekodi kesi 39, 679 za Uviko-19 na vifo 845.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mwanza (MPC), Edwin Soko, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwafundisha waandishi namna ya kuandika habari kwa weledi hasa habari za takwimu.

Alisema katika semina hiyo ya siku moja mada tatu zitawasilishwa ikiwamo ya namna bora ya kuandika habari za uviko-19 kiuweledi na nafasi ya chombo cha habari kwenye kuripoti habari za uviko-19 na uhuru wa habari.

Naye mwezeshaji wa mafunzo hayo, Deus Bugaywa aliitaka jamii kutoamini taarifa za upotoshaji dhidi ya chanjo hiyo huku akiwataka waandaaji kuandaa maudhui yenye afya kwa jamii.

HABARI KIMATAIFA

# Ukraine yadai Russia imefilisika kijeshi

**KYIV, Ukraine**

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy, amesema Russia kwa kutumia ndege zisizo na rubani za Iran kuyashambulia maeneo ya nchi yake, kunaweka wazi kuwa imefilisika kisiasa na kijeshi licha ya miongo kadhaa ya uwekezaji katika sekta ya ulinzi.

Kiongozi huyo alisema amebaini kuwa mashambulizi ya Russia ya hivi karibuni kwenye miundombinu yake yamefanyika kwa kutumia ndege zisizo na rubani zilizopewa jina "kamikaze" zilizotengenezwa na Iran.

Ukraine na washirika wake wa Magharibi wamekuwa wakiituhumu Iran kutoa ndege hizo.

Utawala wa Tehran umekanusha madai hayo na kusema hayana msingi lakini wakibaini kuwa tayari kwa mazungumzo na Ukraine.

Russia kwa upande wake ilisema haikuwa na taarifa iwapo ndege hizo zilitumiwa au la.

**Kamanda wa Russia akiri hali ni tete.**

Kamanda mpya wa vikosi vya Russia nchini Ukraine, Sergei Surovikin, amesema amebaini kuwa hali ni tete kwa vikosi vyake kufuatia shinikizo la vikosi vya Ukraine vinavyodhamiria kuyakomboa maeneo ya Mashariki yaliyokuliwa na Russia.

Kauli hiyo ni ishara ya kuwepo kwa wasiwasi wa Russia katika uwanja wa vita, takriban miezi minane tangu kuanza uvamizi wake.

Surovikin alisema hali ni ngumu huko Kherson na kubaini kuwa vikosi vya Ukraine vinaishambulia kwa makusudi miundombinu na majengo ya makazi.

Ukraine na Russia zimekanusha kuwalenga raia.

Kherson ni moja ya maeneo yanayokaliwa kimabavu na Russia na ni eneo la kimkakati kwa maana ndio njia ya kuelekea rasi ya Crimea na karibu na mto Dnipr.

**Ujerumani yamtimua mkuu wa mtandao**

Mkuu wa usalama wa mtandao wa Ujerumani amefutwa kazi baada ya madai ya kuwa karibu na Russia kupitia chama alichosaidia kuanzisha.

Arne Schönbohm alikuwa ameongoza Mamlaka ya Shirikisho la Usalama wa Mtandao (BSI) na iliyoshtakiwa kwa kulinda mawasiliano ya serikali tangu 2016.

Vyombo vya habari vya Ujerumani vimemshutumu kwa kuwa na uhusiano na watu wanaohusika na idara za ujasusi za Russia. Wizara ya mambo ya ndani inachunguza tuhuma zinazotolewa dhidi yake.

Lakini ilithibitisha kuwa alifukuzwa kazi mara moja. Schönbohm alikuwa amechunguzwa baada ya uwezekano wake wa kuwa na uhusiano na kampuni ya Russia kupitia jukumu la awali na aligunduliwa na Jan Böhmermann, mtangazaji wa moja ya vipindi maarufu vya televisheni vya usiku wa manane nchini Ujerumani.

Kabla ya kuongoza BSI, Schönbohm alikuwa amesaidia kuanzisha na kuendesha Baraza la Usalama la Mtandao Ujerumani, chama cha kibinafsi ambacho kinawashauri wafanyabiashara na watunga sera kuhusu masuala ya usalama wa mtandao.

Inasemekana alidumisha uhusiano wa karibu na chama hicho na alihudhuria sherehe zao za kuadhimisha miaka 10 mnamo Septemba.

Mmoja wa wanachama wa chama hicho alikuwa kampuni ya usalama wa mtandao iitwayo Protelion, ambayo ilikuwa kampuni tanzu ya kutoka Russia iliyoripotiwa kuanzishwa na mwanachama wa zamani wa KGB inayoheshimiwa na Rais Vladimir Putin.

Protelion alifukuzwa katika chama hicho mwishoni mwa juma lililopita, na Baraza la Usalama la Mtandao Ujerumani lilisema madai ya kuhusishwa na ujasusi wa Russia sio ya kweli.

Msemaji wa Waziri wa Mambo ya Ndani Nancy Faeser, alionekana kuthibitisha kwamba kufukuzwa kwa Schönbohm kumekuja kutokana na ripoti za hivi karibuni iliyofichuliwa na kujadiliwa sana kwenye vyombo vya habari.

Msemaji huyo aliongeza kwamba imani ya umma katika kutoegemea upande wowote na kutopendelea kwa uongozi wake kama rais wa wakala muhimu zaidi wa usalama wa mtandao wa Ujerumani imeharibiwa.

*DW*

## Mtoto wa rais Uganda agoma kunyamazishwa

**KAMPALA, Uganda**

MTOTO wa Rais wa Uganda na Mkuu wa zamani wa jeshi la ardhini, Jenerali Muhoozi Kainerugaba amesema hakuna mtu ambaye atakayeweza kumnyamazisha asifanye lolote.

Kauli ya Muhoozi imekuja siku chache baada ya baba yake rais Yoweri Museveni, kuagiza aache kutoa maoni yake kuhusu masuala ya serikali kwenye ukurasa wa Twitter.

Rais Museveni, aliamua kutamka agizo hilo baada ya Jenerali Kainerugaba kuweka ujumbe kwenye ukurasa wake wa Twitter wiki mbili zilizopita akitishia kuivamia nchi jirani ya Kenya.

Kutokana na ujumbe huo tata, rais Museveni aliomba radhi kwa umma na kufanya mikutano ya kidiplomasia ili kuthibitisha uhusiano huo.

Siku ya Jumatatu, alisema jenerali huyo ataepuka kuzungumza kuhusu nchi nyingine na siasa za upendeleo za Uganda kwenye Twitter.

Lakini katika saa chache baadaye, Jenerali Kainerugaba alishangaa kama marufuku hiyo ilikuwa aina fulani ya mzaha.

Jenerali Kainerugaba anajulikana kwa tweet zake zenye utata, zikiwemo za kuunga mkono uvamizi wa Russia nchini Ukraine, na waasi wa Tigray wanaopigana na serikali ya Ethiopia.

**BBC**



Wahudumu wa afya wa Ukraine wanamtunza mtoto ambaye alizaliwa na mama aliyeathirika na mabomu katika hospitali kuu ya Kyiv. **PICHA: THE NEW YORK TIMES**

## Jeshi la Mali laua wanamgambo 50

**BAMAKO, Mali**

VIKOSI vya kijeshi vya Mali vimesema kuwa vimewaua wanamgambo 50 katika mashambulizi ya anga yaliyofanywa katika eneo la Tessalit kaskazini mwa mkoa wa Kidal, shirika la utangazaji la serikali ORTM liliripoti.

Mashambulizi hayo yalielekezwa kwenye makundi ya wapiganaji.

"Tulifanikiwa katika operesheni kama ifuatavyo: magaidi 50 waliuawa, magari matano ya kivita yaliteketezwa na pikipiki 35 za magaidi hao kuharibiwa,"

"Ninawaomba wakazi wa eneo hilo waendelee na shughuli zao za kawaida," alisema kanali Ibrahim Samassa, kamanda msimamizi wa eneo la Gao.

Mashambulizi hayo ya anga yametokea siku moja baada ya vilipuzi viwili kugonga msafara wa walinda amani wa Umoja wa Mataifa na kuua wanajeshi wanne wa Chad na kujeruhi wengine wawili.

Jeshi, likisaidiwa na mamluki wa Russia na makundi ya wanamgambo wa ndani, limekuwa likipambana na makundi ya kijihadi katikati na kaskazini mwa Mali.

Wanamgambo wa Kiislamu wanaojiita jimbo la Sahel wameongezeka kaskazini mwa Mali tangu tangu mwezi Agosti, majeshi ya Ufaransa yalipoondoka.

Jeshi la Mali limeongeza operesheni tangu Desemba mwaka jana wakati mamluki wa Russia walipotumwa nchini humo.

*BBC*

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**ANSELMINA .A. GONGO** anatangaza kupotea kwa cheti cha taaluma cha kidato cha nne chenye index namba **S1406-0003** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **JAMHURI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/KIJ/RB/409223/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JULIUS AMANI MELIYO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye usajili namba **T 806 CMC,** CHASSIS NAMBA: **NCP600161798,** ENGINE NAMBA: **2NZ1955647.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/408889/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WASIM SHAHZAD AHMED** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI AINA YA FORD EVEREST YENYE NAMBA ZA USAJILI **T332CLF** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI
**ARU/ARU/RB/409877/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ANENIAS JOHN MASSAWE** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC788 ABN**. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.TAARIFA YA POLISI **ARU/ARU/RB/169027/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BEST NORTHERN TANZANIA LTD** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T681 AJW, CHASSIS NAMBA HZJ0019671** na ENGINE NAMBA: **IHZ0114727**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:**
**ARU/ARU/RB/409652/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RACHEL MICHAEL PHILIPO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA LEXUS** yenye usajili namba **T813 DFC ,** CHASSIS NAMBA: **JTJHF31U200008697,** ENGINE NAMBA: **Z453GM.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**DAR/OST/RB/408541/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA Mkoa TANGA**
**Usimamizi wa mirathi Na 201 , 2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU RAMADHANI ALI KIWANDA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA AHAMADI HAMISI MSAMI**

**TANGAZO**

**( kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano woowte/ maslahi yoyote na Mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 Mwezi 10 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Imetolewa leo Tarehe 19 Mwezi 10 Mwaka 2022

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA mkoa TANGA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 198,2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU OMARI SALIM SARAI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALITOLETWA NA FATUMA MZEE SUDI**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 26 mwezi 10 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Imetolewa leo tarhe **18 Mwezi 10 mwaka 2022**

HAKIMU

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**INAYOKETI DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA RUFAA YA MADAI NA. 52 YA 2019**

**RUKIA MUSSA ALLY.................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**UTESHI MOHAMED SUNGURA.........MJIBU RUFANI**

**KWA: UTESHI MOHAMED SUNGURA – POPOTE WALIPO**

Mnajulishwa kwamba shauri la Rufaa ya Madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii leo hapa Dar es Salaam tarehe 28/10/2022 saa tatu kamili asubuhi (3:00). Mnapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hutahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria basi rufaa itasikilizwa bila ya uwepo wako.

Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 11/10/2022.

G. H. HERBERT
Kny: MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI

JBK ADVOCATES RECEIVED 13 OCT 2022

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# AIRTEL AFRIKA KIMEELEWEKA TAMASHA THE VOICE AFRICA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI inayoongoza kwa kutoa huduma bora za mawasiliano pamoja na huduma za fedha kwa njia ya simu za mkononi katika nchi 14, Airtel Afrika ilitangaza kudhamini tamasha kabambe la mashindano ya wasanii na wanamuziki linalojulikana kama The Voice Africa ambalo lilizinduliwa rasmi jijini Lagos, Nigeria hapo jana.

Tamasha la The Voice Africa ni shindano la muziki na burudani namba moja duniani linaloonyeshwa kwenye runinga katika zaidi ya nchi 180. Tamasha hili limejizolea umaarufu na kuwa na mafanikio makubwa kupitia The Voice Nigeria.

Kupitia mafanikio hayo Airtel Afrika imeungana na waandaji wa msimu wa tatu na wanne, FAME Studios Afrika, kufanikisha tamasha hilo litakalotoa zawad kwa washiriki katika nchi 14 ambazo Airtel Afrika inafanya biashara.

Msimu huu wa The Voice Afrika utaonyeshwa moja kwa moja kwa mamilioni ya Waafrika kupitia Airtel TV, vituo vya kurusha matangazo bure pamoja na chaneli za kulipia kwa nchi 14 barani Afrika.

Mkurugenzi Mtendaji Airtel Afrika, Segun Ogunsanya, alisema, "Kama wafanyabiashara tunaendeshwa na dhamira ya kuwezesha na kubadilisha maisha ya watu wetu, na hii inakamilika kwa kufungua fursa mbalimbali ili waweze kukua. The Voice Africa inatupa jukwaa la kusaidia na kugundua vipaji vya muziki kwa vijana wa Kiafrika na kuwawezesha kufikia malengo yao. Naamini tamasha hili litaleta burudani yenye msisimko mkubwa na kuunganisha wanafamilia na wateja wetu wote barani Afrika."

Mkurugenzi Mtendaji wa FAME Studios, na Mtayarishaji Mtendaji The Voice Afrika, Akini Salami alisema, "Tunayo furaha kwa kuanzisha tamasha la The Voice Africa msimu wa kwanza na hasa kwa wakati kama huu ambao kuna ongezeko la kukubalika kwa muziki wa Afrika duniani. Mpango huu umetokana na shauku ya kuonyesha vipaji vya Kiafrika kwenye jukwaa la kimataifa na kujenga mustakabali wa Afrika kutambulika zaidi kupitia burudani. Tunatarajia msimu huu wa kwanza utakuwa wa kusisimua na wenye burudani ya aina yake, msimu ambao utawaacha mashabiki na wapenzi wa kipindi hiki wakitamani zaidi."

Naye Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano cha Airtel Tanzania, Beatrice Singano, alisema "Watanzania naomba tuchangamkie fursa hii ili kuitangaza nchi yetu kupitia burudani, muziki wetu sasa unamchango mkubwa katika kujitambulisha na kuitangaza nchi kimataifa, sasa uwepo wa tamasha hili la The Voice of Afrika ni jukwaa jingine la kuipaisha burudani yetu, pamoja na kuitangaza nchi yetu ili kuunga mkono jitihada za Rais, Samia Suluhu Hassan katika kuitangaza nchi kupitia sanaa kama alivyofanya yeye kupitia Royal Tour.

Singano alitaja nchi nyingine zitakazoshiriki katika tamasha hilo ni Tanzania, Nigeria, Niger, Zambia, Kenya, Malawi, Madagascar, Shelisheli, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Chad, Rwanda, Gabon na Uganda

Aliwataka wasanii kujitokeza kujiandikisha kwa njia ya mtandaoni (www.thevoice.afrika.com) na kufuatiwa na majaribio ya kutumbuiza yatakayofanyika baadaye mwaka huu huku akiongeza fainali itafanyika baadaye mwakani.




Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Airtel Tanzania, Beatrice Singano, akizungumza kuhusiana na Tamasha la The Voice Africa alisema mwisho wa wasanii chipukizi kutuma video fupi kwa ajili ya kufanyiwa usahili ni Novemba 6, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbio za Mbuzi mambo yaiva

**Na Mary Geofrey**

KLABU ya Rotary Oysterbay inatarajia kukusanya zaidi ya Sh. milioni 70 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwamo sekta ya elimu, kupitia tamasha la mbio za mbuzi litakalofanyika Novemba 5, mwaka huu.

Rais wa Rotary Oysterbay, Krutin Shah, alisema hayo jijini Dar es Salaam, wakati akielezea maandalizi ya tamasha hilo litakalohusisha wadau mbalimbali wa maendeleo.

Shah alisema tamasha hilo ambalo limedhaminiwa na Kituo cha Luninga cha EATV linafanyika kwa mara ya tatu tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018 kwa kuzingatia maeneo muhimu sita yaliyopewa kipaumbele na Rotary Oysterbay. Alisema kupitia tamasha hilo, washiriki ambao ni watu wazima na watoto watapata burudani mbalimbali kupitia michezo iliyoandaliwa.

"Mashindano ya mwaka huu yaliyopewa kauli mbiu inayosema, 'Sherehekea tamaduni mbalimbali duniani', yatawavutia mashabiki wapya pamoja na washiriki," alisema Shah.

Naye Meneja Miradi wa mbio hizo, Mathew Hellela, alisema tamasha hilo litakuwa na burudani ya kutosha na vionjo mbalimbali vya kufurahisha kila mtu na wanafamilia watakaoshiriki.

## Tabia Mwita mgeni rasmi Tanzanite Festival

**Na Shufaa Lyimo**

WAZIRI wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Mwita anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika Kongamano la Michezo kwa Wanawake (Tanzanite Festival) litakaloanza leo jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Ofisa Habari wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Najaha Bakari, alisema kongamano ambalo litafuatiwa na michezo mbalimbali litashirikishirikisha timu za wanawake kutoka Kenya, Uganda, Zambia, Malawi na wenyeji Tanzania.

"Kesho (leo) tunatarajia kufungua Kongamano la Wanawake na michezo mbalimbali itachezwa, tutatumia uwanja wa Benjamin Mkapa na Uhuru, tunawaomba wanawake wajitokeze kwa wingi, hakuna kiingilio," alisema Najaha.

Aliitaja michezo itakayochezwa ni pamoja na riadha, ngumi za ridhaa na za kulipwa, karate, michezo ya jadi, kabbadi na soka.

Alisema tamasha la mwaka huu limeboreshwa ukilinganisha na tamasha lililopita kwa ajili ya kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu katika michezo ili kujenga afya zao.

## JKU FC yaendelea kuchezea vichapo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya JKU imeendelea kufanya vibaya katika mechi za Ligi Kuu Zanzibar, ambapo juzi ilifungwa bao 1-0 na Mlandege ambapo imepoteza mchezo wa nne mfululizo kwenye ligi hiyo.

Kocha Mkuu wa JKU, Sheha Khamis, alisema ni kawaida katika ligi timu kupata matokeo mabaya na wakati mwingine kuvuna matokeo mazuri.

Khamis alisema wachezaji wake wanajituma na kufanya vibaya kwa timu yake haimaanishi wachezaji wake wameshuka kiwango ila inatokana na matokeo ya mchezo.

"Hiki ni kama kipindi cha mpito kwa timu, kufungwa mechi nne mfululizo sio matokeo mazuri, tumeanza vizuri michezo ya kwanza lakini michezo hii tumefanya vibaya," alisema Khamis.

JKU yenye pointi 10 iko katika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa ligi hiyo baada ya kushinda mechi tatu, sare moja na kufungwa michezo minne.

## ZISIKUPITE

### JORGINHO APANDISHA DAU

KIUNGO wa kati wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 30, anatafuta nyongeza ya mshahara wa hadi pauni 150,000 kwa wiki kabla ya kusaini mkataba mpya na klabu hiyo. ***(Evening Standard)***

### LEAO KUPEWA MKATABA

AC Milan wanashinikiza kuharakisha mazungumzo juu ya mkataba mpya na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 23 huku klabu ya Manchester United ikionyesha nia ya kumwinda. ***(Express)***

### MILAN MAMBO SAFI

MLINZI wa kati wa Inter Milan na Slovakia, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 27, anaweza kusaini mkataba mpya licha ya kunyatiwa na Chelsea. ***(Evening Standard)***

### DAVID ANUKIA CHELSEA

KLABU ya Chelsea ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Lille, raia wa Canada, Jonathan David mwenye umri wa miaka 22, Januari. ***(Jeunes Footeux, via football.london)***

### BESIKTAS YAKANUSHA

KLABU ya Besiktas imekanusha uvumi unaozagaa mtandaoni wanalazimika kumchezesha nyota aliyesajiliwa kwa mkopo Everton, Dele Alli, mwenye umri wa miaka 26, baada ya kiungo huyo wa kati raia wa England kurejea kutoka katika jeraha la paja. (Liverpool Echo)

### MASHABIKI WAMTAKA MESSI

KIKUNDI kidogo cha mashabiki wa Barcelona kimeenda mahakamani kuhusu uhamisho wa mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi kwenda Paris St-Germain mwaka 2021. Mawakili walifika mbele ya Hakimu Mkuu katika wa Mahakama ya Ulaya na kuhoji uhamisho wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 ulivunja sheria. ***(Guardian)***

### GALLAS AMKATAA MARTINELLI

MLINZI wa zamani wa Arsenal, William Gallas amesema mshambuliaji wa sasa wa Washikabunduki hao, Gabriel Martinelli mwenye umri wa miaka 21, bado hajatosha kuhamia Real Madrid. ***(TalkSPORT)***

### EDU AWINDWA ULAYA

MKURUGENZI wa Ufundi wa Arsenal, Edu anasakwa na klabu nyingine za Ulaya lakini kiungo huyo wa zamani wa Arsenal "amezingatia kwa asilimia 100" jukumu lake katika kikosi cha London Kaskazini. ***(Fabrizio Romano)***

### DE PAUL ATAJWA JUVENTUS

KLABU ya Juventus wanavutiwa na kiungo wa kati wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Argentina, Rodrigo De Paul mwenye umri wa miaka 28. ***(Calciomercato)***

### COSTA AKARIBIA UNITED

KLABU ya Manchester United wanapigiwa upatu kuwa vinara kumsajili mlinda mlango wa Timu ya Taifa ya Ureno na Porto mwenye umri wa miaka 23, Diogo Costa. ***(Diario de Noticias, via TeamTalk)***

### UNITED YAMBANA DALOT

MANCHESTER United wanatarajiwa kurefusha mkataba wa Diogo Dalot ili kuwazuia Barcelona ambao wanamwinda mlinzi huyo Mreno mwenye umri wa miaka 23. ***(ESPN, via Mirror)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# JOTA KUKOSA FAINALI ZA KOMBE LA DUNIA

**Mreno huyo anakuwa mchezaji wa pili muhimu wa Liverpool ambaye...**

**LIVERPOOL, England**

DIOGO Jota atakosa fainali za Kombe la Dunia zinazotarajiwa kufanyika hivi karibuni huko Qatar baada ya kupata jeraha "baya sana" la misuli katika ushindi wa Liverpool dhidi ya Manchester City.

Mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno alitolewa nje kwa machela dakika za lala salama katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Anfield Jumapili iliyopita.

Habari ni mbaya kwa Jota, Ureno na Liverpool, ambao michezo yao ijayo pia ataikosa.

"Kwa kweli si habari njema. Ndiyo, atakosa Kombe la Dunia," alisema kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika juzi.

"Ni jeraha kubwa sana, misuli ya ndani. Sasa inabidi tupate nafuu. Mchakato unaanza hivi. Huo ni uchunguzi wa kwanza ambao ulikuwa wazi.

"Ni habari za kusikitisha sana kwa kijana, kwetu, na kwa Ureno."

Klopp alisema Jota hangehitaji kufanyiwa upasuaji kwenye jeraha hilo lakini "tunazungumza kuhusu miezi" kuhusiana na kuachishwa kazi kwake.

"Sitaki kuweka namba juu yake. Ndiyo, itakuwa ndefu," Klopp alisema.

Alieleza Jota alikuwa ameichukua habari hiyo kimawazo.

"Ni Diogo na kwa kushangaza yuko sawa, hadi sasa. Ni mvulana mwerevu sana na anayetafakari sana. Nadhani alijua wakati tulipombeba kutoka uwanjani," Klopp aliongeza.

"Nilipotoka tulipishana baada ya mchezo na alitarajia kilichotokea. Nadhani katika wakati huo alijua ni jambo gumu na linaweza kuwa na athari kubwa kwenye ndoto zake za Kombe la Dunia."

Jeraha la Jota pia linaifanya Liverpool kukosa mchezaji mwingine muhimu wa kushambulia, huku Luis Diaz akiwa tayari nje ya uwanja hadi baada ya Kombe la Dunia.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,042,0

MECHI KALI
ARSENAL
VERSUS
PSV EINDHOVEN
1 | 1.55
X | 4.26
2 | 5.30

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# POGBA AIPA MATUMAINI JUVENTUS NA UFARANSA



**TURIN, Italia**

NYOTA wa Juventus, Paul Pogba, amerejea katika mazoezi ya klabu hiyo baada ya kukaa nje ya uwanja kwa muda mrefu kutokana na majeraha yaliyokuwa yakimsumbua.

Pogba, mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United hakuwahi kushiriki mechi yoyote ya kimashindano na klabu yake hiyo mpya baada ya kupata majeraha ya goti lake la kulia ambayo yamekuwa yakimsumbua kwa muda mrefu.

Kurejea kwa Pogba katika kiwanja cha mazoezi ni habari nzuri kwa Juventus chini ya Kocha, Massimiliano Allegri kwa sababu timu hiyo imekua ikifanya vibaya.

Urejeo wa kiungo huyo unaweza kuwa sehemu ya kuleta uhai kwa timu hiyo.

Pia kupona kwa Pogba ni furaha pia kwa Timu ya Taifa ya Ufaransa ambapo zimebaki wiki tano kabla ya kuanza kwa michuano ya Kombe la Dunia nchini Qatar.

Ufaransa ambao ni mabingwa watetezi michuano hiyo walikuwa wakimhitaji kiungo huyo kwa kiwango cha juu ili kuimarisha safu ya kiungo.

Kocha wa Ufaransa, Didier Deschamps ameonyesha kufurahishwa na urejeo wa kiungo huyo baada ya majeruhi ya muda mrefu.

# Neymar ampongeza Benzema

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR ampongeza chaguo "linalostahili" la Karim Benzema kama mshindi wa Ballon d'Or, baada ya nyota huyo wa Real Madrid kubeba tuzo hiyo Jumatatu.

Lakini mshambuliaji huyo wa Paris Saint-Germain alikosoa kumaliza katika nafasi ya nane kwa mchezaji mwenzake na Benzema, Vinicius Junior.

Neymar anaamini mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alitakiwa kuwa katika nafasi tatu za juu.

Benzema alitawazwa kuwa mchezaji bora zaidi duniani kwa msimu wa 2021-22 katika hafla iliyofanyika mapema wiki hii, akimrithi mchezaji nyota wa PSG, Lionel Messi huku pia akimshinda, Sadio Mane wa Bayern Munich.

"Benzema alistahili," aliandika mshambuliaji huyo kwenye Twitter.

"Sasa, kwa Vini Jr kuwa wa nane - haiwezekani! Kiwango cha chini kwake ni nafasi ya tatu bora!"

Baada ya msimu mgumu zaidi wa maisha yake ya ndani hadi sasa msimu uliopita, Neymar anaonekana kurejea katika kiwango chake bora msimu huu, akiwa na mabao tisa na asisti saba kwenye Ligue 1 hadi sasa.



026,796/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/10/22 | 17:00 | Everton vs Crystal Palace | 2.46 | 3.19 | 2.89 |
| 02. 22/10/22 | 17:00 | Sunderland vs Burnley | 2.88 | 3.23 | 2.45 |
| 03. 22/10/22 | 17:00 | Sheffield Utd vs Norwich City | 2.55 | 3.25 | 2.75 |
| 04. 22/10/22 | 17:00 | Millwall vs West Bromwich | 2.78 | 3.23 | 2.53 |
| 05. 22/10/22 | 17:00 | Reading vs Bristol City | 2.40 | 3.24 | 2.94 |
| 06. 22/10/22 | 20:00 | Niort vs Dijon | 2.73 | 3.18 | 2.68 |
| 07. 22/10/22 | 21:30 | Arminia Bielefeld vs St. Pauli | 2.89 | 3.44 | 2.33 |
| 08. 23/10/22 | 14:30 | Karlsruher SC vs Fortuna Dusseldorf | 2.34 | 3.43 | 2.89 |
| 09. 23/10/22 | 16:00 | Wolverhampton vs Leicester | 2.25 | 3.38 | 3.08 |
| 10. 23/10/22 | 16:00 | Clermont Foot vs Brest | 2.41 | 3.27 | 2.87 |
| 11. 23/10/22 | 16:00 | Troyes vs Lorient | 2.42 | 3.37 | 2.78 |
| 12. 23/10/22 | 17:15 | Betis vs Atletico Madrid | 3.08 | 3.23 | 2.32 |
| 13. 23/10/22 | 17:30 | CS Maritimo vs FC Arouca | 2.59 | 3.24 | 2.69 |
| 14. 23/10/22 | 19:30 | Girona vs Osasuna | 2.58 | 3.08 | 2.83 |
| 15. 23/10/22 | 20:00 | GD Chaves vs Gil Vicente | 2.45 | 3.34 | 2.79 |
| 16. 23/10/22 | 21:45 | Lille vs Monaco | 2.46 | 3.52 | 2.63 |
| 17. 23/10/22 | 21:45 | Roma vs Napoli | 2.83 | 3.47 | 2.36 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 20/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4061 | Tuzlaspor vs Bursa Yildirim Spor | 1.08 | 9.75 | 13.65 |
| 14:30 | 3996 | Sepahan Esfahan vs Teraktor Sazi | 1.93 | 2.96 | 4.08 |
| 15:00 | 1082 | Kifisias vs OFI Crete | 4.77 | 3.41 | 1.67 |
| 15:00 | 1260 | Yeni Malatyaspor vs Agrispor | 1.28 | 5.47 | 7.42 |
| 15:00 | 4642 | FC Otelul Galati vs CS Mioveni | 2.61 | 3.05 | 2.57 |
| 15:30 | 1411 | FCM Baia Mare vs Argesul Pitesti | 3.50 | 3.16 | 2.01 |
| 16:00 | 1967 | Cremonese vs Modena | 1.76 | 3.82 | 4.06 |
| 16:00 | 2680 | Arab Contractors vs Ghazl EL Mahallah | 2.22 | 2.63 | 4.07 |
| 16:00 | 3156 | Inter Stars vs Bujumbura City | 2.78 | 2.78 | 2.63 |
| 16:00 | 3371 | Ethiopia Electricity vs Legetafo Legedadi | 2.35 | 2.96 | 2.96 |
| 16:00 | 3830 | Nikolaos vs Almyros | 2.23 | 3.12 | 3.03 |
| 17:00 | 1631 | Dynamo Kiev vs FC Metalist Kharkiv | 1.26 | 5.23 | 8.72 |
| 17:00 | 4310 | Olympique de Beja vs US Monastir | 2.71 | 2.62 | 2.86 |
| 17:30 | 4357 | Giresunspor vs Amasyaspor | 1.01 | 13.62 | 26.26 |
| 18:00 | 4116 | Karabakh vs Turan Tovuz | 1.17 | 6.20 | 11.63 |
| 18:00 | 5911 | Sochi vs Ural Yekaterinburg | 1.87 | 3.61 | 3.46 |
| 18:30 | 1351 | TPS Turku vs Lahti | 2.78 | 2.78 | 2.63 |
| 18:30 | 1464 | ES Bafing vs Sporting Gagnoa | 4.88 | 2.88 | 1.83 |
| 19:00 | 1687 | Sampdoria vs Ascoli | 1.54 | 4.07 | 5.56 |
| 19:00 | 5892 | AEK Athens vs PAS Giannina | 1.28 | 4.77 | 8.95 |
| 19:30 | 1985 | Royal Antwerp vs Oostende | 1.56 | 4.17 | 5.16 |
| 19:45 | 4169 | ZSV Sportlust 46 vs Utrecht | 20.41 | 9.33 | 1.06 |
| 19:55 | 3303 | Vojvodina vs Red Star Belgrade | 9.40 | 5.60 | 1.27 |
| 20:00 | 1311 | Hammarby vs Sirius FK | 1.24 | 5.44 | 8.94 |
| 20:00 | 1407 | Degerfors vs IFK Goteborg | 2.47 | 3.44 | 2.47 |
| 20:00 | 1792 | Kalmar vs Mjallby | 1.64 | 3.50 | 4.86 |
| 20:00 | 4242 | El Daklyeh vs Talaea El Gaish | 4.96 | 3.47 | 1.71 |
| 20:00 | 4975 | Arsenal vs PSV Eindhoven | 1.55 | 4.26 | 5.30 |
| 20:00 | 5149 | Almeria vs Girona | 2.55 | 3.19 | 2.75 |
| 20:00 | 5384 | Malmo vs Djurgardens IF | 2.02 | 3.41 | 3.22 |
| 20:30 | 1081 | Al Sareeh vs Shabab Al Ordun | 3.55 | 3.46 | 1.89 |
| 20:30 | 1833 | Zenit St Petersburg vs Kryliya Sovetov | 1.29 | 5.05 | 7.78 |
| 20:30 | 4659 | Gaziantep BB vs Sariyer | 1.05 | 9.74 | 21.43 |
| 21:00 | 1706 | Bassam vs ASEC Mimosas | 5.43 | 3.64 | 1.56 |
| 21:00 | 2519 | Osasuna vs Espanyol | 2.07 | 3.31 | 3.51 |
| 21:00 | 3201 | OFC Oostzaan vs Sparta Rotterdam | 9.71 | 7.19 | 1.17 |
| 21:00 | 3230 | Universitatea Cluj vs CFR Cluj | 3.08 | 2.98 | 2.28 |
| 21:00 | 3852 | Dongen vs VVV Venlo | 9.56 | 6.44 | 1.19 |
| 21:00 | 4280 | Rkav Volendam vs HV & CV Quick | 2.63 | 3.07 | 2.53 |
| 21:15 | 4780 | Sporting Cristal vs Atletico Grau | 1.25 | 5.26 | 9.34 |
| 21:30 | 1423 | FC Basel vs FC Zurich | 1.88 | 3.68 | 3.68 |
| 21:30 | 3168 | Fulham vs Aston Villa | 2.78 | 3.22 | 2.44 |
| 21:30 | 3943 | Grasshoppers vs Servette Geneva | 3.09 | 3.54 | 2.13 |
| 21:30 | 4295 | Wiener SC vs Austria Vienna | 15.55 | 7.97 | 1.10 |
| 21:45 | 4765 | Zulte Waregem vs Anderlecht | 4.77 | 4.17 | 1.60 |
| 22:00 | 1135 | Bologna vs Cagliari | 1.69 | 3.87 | 4.47 |
| 22:00 | 3013 | HHC Hardenberg vs PEC Zwolle | 7.21 | 5.26 | 1.30 |
| 22:00 | 4606 | Vicenza vs Mantova | 1.43 | 4.21 | 7.42 |
| 22:00 | 4739 | Barcelona vs Villarreal | 1.54 | 4.35 | 5.29 |
| 22:15 | 2997 | Leicester vs Leeds | 2.24 | 3.42 | 2.93 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MO BOXING YADHAMIRIA KUWAPAISHA MABONDIA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya kuandaa ngumi za kulipwa ya MO Boxing imepania kuendeleza mchezo huo hapa nchini kwa kiwango cha juu na hatimaye kufanya vizuri kwenye mapambano ya kimataifa.

Mpaka sasa MO Boxing imeandaa pambano moja la ngumi za kulipwa lililofanyika Septemba 30, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam na kushirikisha mabondia kutoka nchi sita tofauti.

Pambano hilo lilikuwa la kihistoria kutokana na kushirikisha mabondia wenye viwango vya juu ikiwamo kuleta mabondia kutoka Mexico ambao walipigana katika ardhi ya Tanzania kwa mara ya kwanza chini ya udhamini wa mfanyabiashara maarufu, Mohammed Dewji 'Mo'.

Mabondia wengine walitoka nchi za Ghana, Namibia, India na Falme za Kiarabu (UAE).

Siku hiyo, Mtanzania, Ibrahim Class hakuwaangusha Watanzania kwa ushindi wa knockout (KO) dhidi ya Gustavo Alan Pina katika raundi ya tisa katika pambano la uzito wa Super Feather ambapo Mkurugenzi wa Masoko wa Kampuni ya MeTL, Fatema Dewji, alikuwa mgeni rasmi.

Haikuwa rahisi kwa Class kushinda kwani alipata upinzani mkali na kuzawadiwa pikipiki aina ya Boxer kutoka kwa kampuni ya MeTL -Bajaj division ambao ilikuwa wadhamini. Wadhamini wengine walikuwa Azam TV, Boxer, Mo Xtra, Mlimani City, KCB Bank, White Sands Resorts na Otapp.

Dewji aliliambia gazeti hili MO Boxing Promotions imepania kuinua vipaji mbalimbali kwa kuandaa mapambano mengi ya ngumi za kulipwa nchini na pia nje ya Tanzania kwa ubora wa hali ya juu.

Alisema lengo kubwa ni kuifanya Tanzania kuwa kituo cha ngumi za kulipwa Afrika kwa kuandaa mapambano mbalimbali yatakayoshirikisha mabondia nyota.

"Tanzania inaweza kuwa nchi pekee maarufu kwa mchezo wa ngumi za kulipwa katika bara la Afrika na njia ya kufanya hivyo imeanza kuonekana kutokana na mapambano yaliyopita," alisema Dewji.

Haikuwa rahisi kwa Class kuibuka kidedea kutokana na upinzani alioupata na kufanya azawadiwe pikipiki aina ya Boxer kutoka kwa MeTL-Bajaj division ambao walikuwa wadhamini pamoja na Azam TV, Mo Xtra, Mlimani City, Benki ya KCB, White Sands Resorts na Otapp.



Mwamuzi wa ngumi za kulipwa nchini, Pendo Njau (wa pili kushoto), akimnyanyua mkono bondia, Ibrahim Class baada ya kumchapa kwa KO, Gustavo Pina kutoka Mexico. Kushoto ni Mkurugenzi wa Masoko wa MeTL, Fatema Dewji ambaye alikuwa mgeni rasmi katika pambano hilo. **PICHA: MAKTABA**

# Rais Samia asema

INATOKA UK. 32

"Tutaendelea kupambana kama ambavyo tumefanya katika mechi zilizotangulia, tunajua hakuna mechi rahisi, timu zote zimekuja hapa kushindana, kikubwa ni kuendelea kurekebisha makosa yetu na kuingia tukiwa bora zaidi kuwakabili Colombia," Shime alisema.

Serengeti Girls itaikabili Colombia iliyokuwa kinara katika Kundi C katika mchezo utakaochezwa keshokutwa wakati Marekani wataivaa Nigeria huku Brazil wakiikaribisha Ujerumani na Japan wataonyeshana ubabe dhidi ya Hispania.

Tayari Serengeti Girls imeshajihakikishia zawadi ya Sh. milioni 40 kutoka kwa Shirika la Bima la Taifa (NIC), ambalo lilitoa ahadi na endapo itafika nusu fainali itawapatia Sh. milioni 80 huku wakitinga fainali wataondoka na kitita cha Sh. milioni 100.

# Simba, Yanga

INATOKA UK. 32

tokana na ubora wa kikosi chao na matokeo mazuri waliyopata katika michezo yao ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Ni mechi muhimu kwa sababu kila mmoja wetu anahitaji kupata pointi tatu, hatutakwenda uwanjani kwa kuwadhurau wapinzani wetu kwa sababu tuliwahi kuwafunga katika mechi zetu tulizocheza hivi karibuni," alisema kocha huyo.

Alisema wanafahamu Simba wako imara na wanaendelea kujiimarisha kwa ajili ya kuwapa furaha mashabiki wao katika mchezo huo na kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo ambapo sasa wako juu kwa tofauti ya mabao ya kufunga.

"Tunataka kupanda kileleni lakini kikubwa kuhakikisha tunajiweka imara kutetea taji la ubingwa, hatutaki kupoteza taji hili," aliongeza Nabi.

Michezo

Alhamisi Oktoba 20, 2022
Nipashe



UKURASA 29

## Jota kukosa fainali za Kombe la Dunia



Kikosi cha Serengeti Girls kilichoanza katika mechi ya Kundi D ya Fainali za Kombe la Dunia (U-17), dhidi ya Canada iliyochezwa juzi jioni nchini India. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1 na matokeo hayo yaliipeleka hatua ya robo fainali Serengeti Girls. **PICHA: TFF**

# SIMBA SC, YANGA HAKUNA KULALA

## Mnyama atabiriwa makubwa, Nabi akiendelea kusaka dawa...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI mjumbe wa Bodi ya Simba, Crescentius Magori, akisema timu hiyo ina uwezo wa kutinga fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika endapo watasajili nyota wawili au watatu wapya wa kiwango cha juu katika dirisha dogo la usajili, Yanga imetamba mambo yatakuwa mazuri kuelekea mechi yao dhidi ya Club African ya Tunisia.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Magori alisema Simba ni timu ambayo kila baada ya muda fulani au miaka kadhaa imekuwa ikifanya maajabu kwenye soka la Afrika, hivyo wala haitakuwa mara ya kwanza kufanya vyema kwenye michuano ya msimu huu.

Magori alisema kwa sasa Simba ina wachezaji wenye uwezo mkubwa na uzoefu katika michuano hiyo, hivyo inahitaji kuongeza nguvu kidogo ili kuweka mambo sawa.

"Hii timu Januari tukiongeza nguvu kwa kuongeza wachezaji wawili, watatu hivi kuziba mapungufu madogo yaliyopo, basi tunaweza kufika nusu fainali au fainali kabisa kwa sababu ina wachezaji wazoefu na wenye uwezo wa kucheza michuano hii, ni kuongeza nguvu kidogo tu," Magori alisema.

Hilo pia lilibainishwa na Rais wa Heshima wa klabu hiyo, Mohamed Dewji, ambaye aliandika kwenye mtandao wake wa kijamii kuhusu kufanya mabadiliko katika maeneo ambayo yana udhaifu ndani ya kikosi hicho.

"Familia yangu ya Simba, mwanzoni mwa msimu wa ligi, niliandika miaka mitano iliyopita imekuwa ya mafanikio. Bajeti iliongezeka mara tano, tulishinda makombe mengi ya ndani na tuliweka alama kimataifa kwa kufika robo fainali tatu za michuano ya Afrika. Najivunia kusema tupo katika orodha ya klabu bora 12 Afrika. Hii imekuwa mara ya kwanza Simba kuwa na mwendelezo mzuri katika miaka 86 ya historia yetu. Hakuna kurudi nyuma, tunatakiwa kufanya mabadiliko katika maeneo ambayo tuna madhaifu na kwenda mbele. Mapambano yanaendelea," alisema Mo Dewji.

Habari za ndani zinasema huenda Simba inajipanga kunasa nyota wapya wakigeni watatu ikiwa nafasi moja ya Dejan Georgijevic aliyevunja mkataba huku Wanigeria wawili, Nelson Okwa na Victor Akpan wakidaiwa kupelekwa kwa mkopo timu nyingine, taarifa za awali zinasema Okwa atarejea kwenye timu yake ya zamani Rivers United.

Licha ya kufahamu itakutana na Waarabu wa Tunisia katika mechi ya mtoano ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ameweka wazi akili na nguvu zao kwa sasa wamezielekeza katika mchezo wao dhidi ya Simba utakaochezwa Jumapili.

Kaze alisema mechi hiyo haikuwa rahisi kutokana na makosa ambayo yanafanywa na safu yao ya ulinzi.

Kocha huyo alisema makosa hayo yamewagharimu lakini wanajipanga kuyamaliza kabla ya kukutana na Simba kwa ajili ya kuhakikisha wanaendeleza ubabe.

"Tumepoteza na kutolewa katika Ligi ya Mabingwa Afrika, tunaenda kufanyia kazi mapungufu yetu ili kujiandaa vyema na mechi ijayo dhidi ya Simba, tunataka kupata matokeo mazuri, kuendelea pale tulipoishia," alisema Nabi.

Aliongeza wanaiheshimu Simba ku-

INAENDELEA UK. 31

## Rais Samia asema Serengeti Girls inamfurahisha sana

**Na Saada Akida**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema amejisikia furaha sana baada ya Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), kutinga hatua ya robo fainali katika fainali za Kombe la Dunia zinazoendelea huko nchini India.

Serengeti Girls imesonga mbele katika fainali hizo baada ya kumaliza kwenye nafasi ya pili katika Kundi D baada ya kujikusanyia pointi nne nyuma ya mabingwa watetezi na vinara wa kundi hilo, Japan waliofikisha pointi tisa.

Bosi huyo namba moja wa Tanzania alisema Serengeti Girls wameweka historia na wamefanya jambo kubwa kupeperusha vyema bendera ya nchi.

"Mmenifurahisha sana watoto wangu (Serengeti Girls) kwa kuandika historia ya kufuzu kuingia robo fainali ya michuano ya Kombe la Dunia kwa wanawake chini ya miaka 17 nchini India. Mmefanya jambo kubwa kwa nchi yetu Tanzania na ninawatakia kheri katika hatua ya robo fainali," alisema Rais Samia.

Naye Kocha Mkuu wa Serengeti Girls, Bakari Shime, alisema ushindi wa timu hiyo ni wa Watanzania wote na wanapaswa kujivunia kwa mafanikio hayo huku akiwaomba waendelee kuiombea dua njema iendelee kufanya vyema katika hatua inayofuata.

Shime alisema Watanzania wote wanatakiwa kufurahia mafanikio hayo na aliwapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kufanya kazi waliyopewa na taifa lao.

"Tumekuja kwa niaba yao, tusingeweza kucheza wote, tumecheza kwa niaba yao, tumeshinda tufurahi sote. Ni nchi ambayo imeshinda, kila Mtanzania anapaswa kujivunia na watuombee Mungu kwa hatua inayofuata," alisema Shime.

Kocha huyo alisema mechi hiyo ilikuwa ngumu lakini walijitolea kwa nguvu kutetea taifa lao na kutoka nyuma hadi kusawazisha bao.

"Wachezaji wetu wamejitolewa kwa nguvu sana, wametoka nyuma wakiwa wamefungwa hadi kurudisha bao, ni fahari kuona tumetimiza malengo yetu ya msingi tuliyokusudia kuhakikisha tunavuka hatua ya maikundi, ni fahari kwangu mimi, wachezaji na watanzania wote," alisema Shime.

Aliongeza sasa wanarudi kwenye mazoezi kwa ajili ya kujipanga kuwakabili Colombia kwenye hatua hiyo ya robo fainali.

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002